# ILANI YA UCHAGUZI, 2020

## THE CIVIC UNITED FRONT

## (CUF - Chama Cha Wananchi)




INAKULETEA

HAKI SAWA NA FURAHA KWA WOTE!

cufuchaguzi@gmail.com

Yaliyomo


1. SEHEMU YA KWANZA....4
1.1. Kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa....8
1.2. Kufuta Umasikini Katika Nyanja Zote....8
1.3. Kutokomeza Njaa na Kuhakikisha Lishe Bora kwa Wajawazito na Watoto....9
1.4. Kutoa Huduma Bora ya Afya na Kudhibiti Vifo vya Wajawazito na Watoto....10
1.5. Kuwahudumia Wazee Waliolitumikia Taifa Letu....10
1.6. Kuwasaidia Walemavu na Kuwawezesha Kupata Elimu na Ajira....10
1.7. Usimamizi wa elimu bora na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasilino....11
1.8. Kusimamia maendeleo ya kiuchumi nchini....11
1.9. Usimamizi makini katika sekta ya kilimo na maendeleo ya viwanda....12
1.10. Kuimarisha miundo mbinu na kuhamasisha uwekezaji....13
1.11. Kuimarisha Mazingira ya Uwekezaji, Kufanya Biashara na Ujasiriamal....13
1.12. Usimamizi wa rasilimali za Taifa na Nidhamu ya matumizi ya fedha za umma....13
2. SEHEMU YA PILI....15
2.1. KATIBA....15
2.2. UTAWALA WA SHERIA....17
2.3. IDARA YA MAHAKAMA....18
2.4. HAKI ZA BINADAMU....19
2.5. UONGOZI MADHUBUTI WA UTUMISHI WA UMMA....23
2.6. VIONGOZI WA KUCHAGULIWA....24
2.7. VIONGOZI WA KUTEULIWA....25
2.8. MATUMIZI YA SERIKALI....25
2.9. MAPAMBANO DHIDI YA UFISADI NA RUSHWA....28
2.10. ULINZI NA USALAMA....30
2.11. MAMBO YA NCHI ZA NJE....32
3. SEHEMU YA TATU....34

3.1. UCHUMI....34
3.1.1. HALI YA MAISHA YA MTANZANIA KWA UJUMLA NA SEKTA MUHIMU ZA UCHUMI....34
3.1.2. SEKTA MUHIMU ZA UCHUMI - KILIMO....45
3.1.3. UFUGAJI....51
3.1.4. UVUVI....53
3.1.5. MAENDELEO YA VIWANDA NA AJIRA RASMI....56
3.1.6. SEKTA ISIYO RASMI....63
3.1.7. MISITU....64
3.1.8. MADINI....67
3.1.9. UTALII....71
3.1.10. SEKTA YA FEDHA NA HUDUMA ZA KIBIASHARA....74
3.1.11. MASOKO YA MITAJI NA HISA....80
3.1.12. HUDUMA ZA BIMA....82
3.1.13. HIFADHI YA JAMII....84
3.1.14. MATUMIZI YA BANDARI....86
3.1.15. MAPATO YAKODI....89
3.1.16. MTANDAO WA MAWASILINO....93
3.1.17. RELI NA BARABARA....94
3.1.18. USAFIRI WA MAJINI....100
3.1.19. USAFIRI WA ANGA....101
3.1.20. HUDUMA ZA SIMU, NUKUSHI (FAX), POSTA, NA MTANDAO (INTERNET)....102
3.1.21. HUDUMA ZA UZALISHAJI MALI....105
3.1.22. ELIMU....117
3.1.23. AFYA....137
3.1.24. ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI....145
3.1.25. MAENDELEO YA MAKUNDI YA JAMII....149
3.1.26. MICHEZO NA BURUDANI....164

# 1. SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Kwa mara nyingine tena ifikapo Oktoba 2020 wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tutapiga Kura kuchagua Rais, Wabunge, Wawakilishi na Madiwani wa nchi yetu. Huu utakuwa ni Uchaguzi Mkuu wa sita (6) kufanyika nchini chini ya mfumo wa vyama vingi. Tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wakati nchi yetu ikiwa njia panda, Watanzania wamechoshwa na hadaa na ngulai za CCM.

Umasikini unaongezeka, ajira zimetoweka, ufisadi na rushwa bado havijatoweka na Mafisadi waliostahili kufikishwa Mahakama ya Ufisadi leo wanajisafisha kwa tendo la kubadili vyama tu. Serikali ya CCM imeshindwa kuboresha maisha ya Mtanzania. Hali ya maisha imezidi kuwa ngumu mpaka vjana wameanzisha msamiati mpya wa "Vyuma Vimekaza". Wafanyakazi wana hali mbaya kutokana na serikali kushindwa kuboresha mishahara na stahiki zao nyingine kuendana na kupanda kwagharama za maisha.

Ufisadi na rushwa zinaendelea kuimarika nchini na CCM imegawika mapande mapande. CCM kila uchao inazidi kuhama kutoka kuwa chama cha siasa na kuelemea zaidi kuwa chama Dola. Ni ukweli usio na shaka kwamba bila dola CCM itasambaratika. Watanzania tutajuta ikiwa tutaruhusu ufisadi mkubwa wa wizi wa kura na kuipa fursa CCM ya kuendelea kutawala. CCM haina dira ya kuongoza nchi na kusimamia utawala bora. Kama marehemu Rais Mkapa alivyoeleza kwenye kitabu chake CCM bado inajiona kama iko katika mfumo wa Chama kimoja. CCM Haina lengo la kujenga mfumo wa demokrasia ya wananchi.

Uongozi wa awamu ya tano umeshindwa kuwashirikisha watu wengine katika uchambuzi wa sera, kubaini matatizo na upimaji utekelezaji. Unafanya maamuzi kwa kukurupuka. Hautabiriki. Rais Magufuli mwenyewe kaeleza maamuzi yake yanategemea ameamkaje.

Mara kwa mara Serikali ya awamu ya tano imekuwa haifuati sheria na taratibu. Utekelezaji wa mambo makubwa unaanza kutekelezwa bila fedha za utekelezaji kuidhinishwa na Bunge. Ndani ya serikali hata Baraza la Mawaziri hakuna mijadala iliyo huru na wazi. Uoga kuwa wakati wowote unaweza kutumbuliwa umetawala. Kauli ya Rais Magufuli alipokuwa anamuapisha Waziri mpya wa Viwanda na Biashara alisema pamoja na mambo mengine "Prof. Kabudi na Mpango hawasemi tu. Kama pumbavu kwenye simu wametukanwa sana. Wamenizidi umri. Pumbavu inakuja haraka haraka yenyewe. Hii kazi siyo ya kubembelezana ni lazima tuipeleke kijeshi."

Kauli kama hii dhidi ya Mawaziri waandamizi inaashiria kuona majadiliano ya wazi bila woga ambao ndiyo msingi wa demokrasia siyo nyezo bali ni kikwazo cha maendeleo. Katika mazingira haya Mawaziri hawawezi kumshauri Rais bila woga hasa katika mambo ambayo wanajua msimamo wa Rais uko tofauti na fikra zao.

Serikali za CCM zimeshindwa kutumia utajiri mkubwa tulionao wa rasilimali na maliasili ya taifa kwa manufaa ya wananchi wote na badala yake leo Tanzania imeendelea kuwa omba omba wa kimataifa. Kumbuka jinsi tulivyonyukana na hata kutamani kuuana kwa sababu ya Mkopo wa Bilioni 500 kutoka Benki ya Dunia katika kipindi cha Januari na Aprili 2020. Mapato ya ndani hayakidhi kulipia matumizi ya kawaida pamoja na kulipia madeni ya ndani na ya nje. Kimsingi bajeti ya maendeleo inategemea mikopo na misaada.

Malengo ya Maendeleo Endelevu yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa mwaka 2015 yana nia ya kufuta umaskini katika nyanja zake zote ifikapo mwaka 2030, kwa kutekeleza kwa vitendo haki za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kimazingira. Inatia moyo sana kwamba hata kabla ya Jumuiya ya Kimataifa kuyakubali na kuyatangaza Malengo ya Maendeleo Endelevu, tayari ***sera za CUF za haki Sawa na furaha kwa Wote*** zilishajikita katika kufanikisha malengo hayo haraka iwezekanavyo.

Hivyo basi, Ilani ya CUF, pamoja na mambo mengine inafafanua, sanjari na kupendekeza hatua stahiki, ili kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030.

Malengo haya ni kuwa ifikapo 2030 tuwe na Tanzania ambayo:-

1. Haina umaskini
2. Wananchi hawana njaa. Wanapata chakula cha kutosha na lishe bora
3. Wana huduma za msingi za afya na ustawi bora
4. Watoto wanapata elimu bora na wananchi wana fursa ya kujiendeleza kielimu katika maisha yao yote.
5. Kuna usawa wa jinsia. Haki za wanawake zinalindwa.
6. Wananchi wote wanapata maji safi na salama na wanaishi katika mazingira masafi
7. Wananchi wanatumia nishati safi na salama kwa sayari yetu, lakini yenye gharama nafuu
8. Wananchi wanapata ajira stahiki kutokana na Uchumi unaokua vizuri na kwa kasi
9. Inaendeleza Viwanda vya kisasa, Inachochea ubunifu na Inajenga Miundombinu yenye kukidhi haja
10. Inanyanyua pato la mwananchi wa kawaida kwa kasi ili kupunguza tofauti za mali na vipato kati ya Wananchi
11. Inaendeleza Miji bora kwa vigezo vya kisasa
12. Ina Matumizi na uzalishaji wenye kukidhi mahitaji ya kiuchumi ya Wananchi na Taifa.
13. Imechukua hatua za kuhuisha na kulinda Mazingira
14. Inalinda uhai wa viumbe wa Majini - mito, maziwa na bahari
15. Inalinda uhai wa viumbe wa Juu ya ardhi - misitu, wanyama na viumbe wengine
16. Ina Amani, Haki, Furaha na Taasisi za kiutawala zilizo bora na imara
17. Inashirikiana kwa karibu na Jumuia ya kimataifa kufikia malengo.

Wachambuzi wengi wa maendeleo ya uchumi na jamii wanaamini kuwa kuongezeka kwa furaha ya wananchi kwa ujumla wao ndiyo kipimo mahsusi cha maendeleo ya uchumi na jamii. Mambo muhimu yanayowafanya wananchi kuwa na furaha ni pamoja na jamii inayojaliana, yenye uhuru, yenye ukarimu, yenye kuaminiana, ambayo watu wake wana afya njema, ambayo watu wake wana kipato kizuri, na yenye utawala bora.

Tangu mwaka 2012, Taarifa ya Furaha Duniani - World Happiness Report imekuwa ikitolewa kila mwaka kusaidia kazi za Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Viongozi wa Juu kuhusu Maisha Bora na Furaha. Taarifa ya Furaha Duniani - **World Happiness Report 2020** inaonyesha kuwaTanzania ni nchi ya 148 kati ya nchi 153 kwa kuwa na furaha duniani. Watanzania hatuna furaha kwa sababu ya ***hali ngumu ya maisha, huduma mbovu za afya, mazingira ya kutoaminiana, uvunjifu wa haki za binadamu na ukosefu wa uhuru na utawala bora***

Watanzania wenye kutafakari mambo kwa kina wameweka matumaini yao kwa Chama cha CUF na misingi ya sera zake ya "Haki Sawa na Furaha kwa wote" na "Kujenga uchumi imara unaoongeza ajira na utakaoleta neema na tija kwa wote".

Nchi yetu imerudi katika Mfumo wa Vyama Vingi muda mrefu sasa na CCM imeendelea kutawala.Wananchi wanaendelea kuteseka kwa kuona matatizo yao yakizidi kuongezeka bila kuchukuliwa kwa hatua za msingi kuyatatua. Hali hii imewafanya wananchi wengi - hasa vijana na wanawake - kuwa na shauku kubwa ya kuona utawala wa nchi yetu unabadilishwa kwa amani, kupitia sanduku la kura.

CUF kwa kutambua nafasi yake katika kuyaongoza mabadiliko yanayohitajika, hususan kutokana na mjengeko wake wa kuwa kweli ni Chama cha kitaifa chenye kukubalika na chenye mtandao mpana katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano, imeibuka na sera zilizojikita katika msingi na kauli mbiu ya HAKI SAWA NA FURAHA KWA WOTE. Msingi huu ni Dira ya mabadiliko na ndiyo kitovu cha ILANI yetu ya uchaguzi. Msingi huu chini ya Serikali ya CUF utaibeba

Tanzania mpya inayojali haki sawa kwa wote na kuwahakikishia wananchi wote FURAHA. Mambo muhimu yaliyobebwa na Ilani hii ni haya yafuatayo:-

### 1.1. Kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa

Nchi yetu imejaa ufisadi, ubinafsi, migawanyiko, kuumizana, ubaguzi, kutokuaminiana, chuki, kukata tamaa na huzuni. Haya ni majeraha yanayohitaji kutibiwa na kuwarejeshea wananchi matumaini. Tumefikia hapa tulipo kutokana na Tanzania kukosa taasisi imara za kusimamia uendeshaji wake. Taasisi zilizoko uimara wake ni wa kinadharia kuliko wa uhalisia. Katika mazimgira haya mustakabali wa nchi umekuwa ukitegemea zaidi haiiba na matakwa ya rais aliyeko madarakani kuliko taratibu za kitaasisi. CUF inataka nchi iwe na taasisi imara zinazounda mfumo madhubuti ambao utahakikisha kuwa nchi iko salama bila kujali ni chama gani kiko kwenye nadaraka.

Kuunda mfumo huu kunahitaji nguvu ya pamoja na ushirikishwaji wa kila Mtanzania. Kwa sababu hii CUF inapendekeza serikali ya umoja wa kitaifa. Serikali hii jumuishi itakuwa na jukumu la kujenga mfumo unaohitajika.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa chini ya CUF itaweka misingi ya kuhakikisha kuwa taifa linakuwa na Demokrasia ya kweli. Serikali ya umoja wa kitaifa itakamilisha mchakato wa kupata katiba mpya yenye misingi imara ya demokrasia na utawala bora. Katiba ambayo pamoja na mambo mengine itatenganisha kikamilifu mamlaka na nguvu za mihimili mbalimbali, italinda misingi ya ushindani wa kisiasa, itapanua na kukuza haki za kiraia, na itahakikisha uwepo wa uhuru wa kutosha wa vyombo vya habari na fursa ya kujieleza.

Tunahitaji kuwa na katiba nzuri inayompa kila Mtanzania uhuru wa kweli wa kuchagua na au kuchaguliwa. Tunahitaji kuwa na Muungano wa Watanganyika na Wazanzibari usio na mashaka ndani yake kwa pande zote mbili. Tunahitaji Umoja wa Kitaifa wa kweli ambapo ubaguzi wa aina yoyote iwe ni wa jinsia, rangi, dini au ulemavu utakuwa ni jinai inayoadhibiwa kwa

mujibu wa sheria. Aidha tunahitaji kuwa na katiba inayojilinda isivunjwe na wanasiasa walioko madarakani kwa ajili ya maslahi yao binafsi na maslahi ya makundi wanayoyashabikia.

Katiba ya sasa haikidhi vigezo vinavyohitajika ili kuchochea maendeleo ya demokrasia nchini mwetu. Chini ya Sera za HAKI SAWA NA FURAHA KWA WOTE, serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaandaa utaratibu unaofaa wa kupata Katiba Mpya ya wananchi.

### 1.2. Kufuta Umasikini Katika Nyanja Zote

Ukuaji wa uchumi wa Tanzania haujaambatana na kasi kubwa ya kupungua kwa watu masikini. Idadi ya watu masikini kwa kutumia kipimo cha taifa cha umasikini (mtu mzima kutumia shilingi 50,000/ au zaidi kwa mwezi) imeongezeka toka watu milioni 12.3 mwaka 2011 na kufikia watu milioni 14 mwaka 2018. Kwa kutumia kipimo cha kimataifa cha umaskini, Watanzania zaidi ya milioni 27 ni masikini.

Utafiti uliofanywa na serikali mwaka 2016 kuhusu umaskini wa watoto (Child Poverty in Tanzania) ulibaini kuwa asilimia 74 ya watoto wa Tanzania wanaishi katika mazingira ya umaskini kwa tafsiri pana inayojumuisha lishe, afya, hifadhi iliyo salama, elimu, mazingira, maji na makazi.

### 1.3. Kutokomeza Njaa kwa Wote na Kuhakikisha Lishe Bora kwa Wajawazito na Watoto

Kuhakikisha kuwa kila mwananchi anakuwa na uwezo au kuwezeshwa kupata milo mitatu kwa siku. Hatua za makusudi zitachukuliwa kuhakikisha kuwa kinamama wajawazito na watoto wachanga wanapata lishe bora itakayowasaidia watoto kujengeka vizuri katika viungo vya mwili, kinga ya mwili na ubongo, ili waweze kushiriki kikamilifu katika kujielimisha na kujiendeleza.

## 1.4. Kutoa Huduma Bora ya Afya na Kudhibiti Vifo vya Wajawazito na Watoto

Kuhakikisha kuwa Bajeti ya Wizara ya Afya inapanda na kufikia asilimia 15 ya Bajeti ndani ya miaka 10 ijayo. Ongezeko la bajeti litawezesha katika kuandaa miundombinu ya kisasa, wataalam, vifaa tiba na vipimo vya kutosha kwa maradhi yote. Aidha ongezeko la bajeti litawezesha kutenga fungu maalum kwa ajili ya kukabili maradhi ya milipuko kama COVID-19 kwa kadri yatakavyojitokeza. Ili kuhakikisha kuwa kila raia ana haki na anapata huduma za msingi za afya, Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha asilimia 70 ya Watanzania wote wana Bima ya Afya ifikapo 2025 na asilimia 100 ifikapo 2028. Hatua maalumu zitachukuliwa kuhakikisha kuwa huduma za uzazi bila malipo zinapatikana kwa kila mama mjamzito ili kupunguza vifo vingi vinavyotokea ambavyo vinadhibitika.

## 1.5. Kuwahudumia Wazee Waliolitumikia Taifa Letu

Kuweka utaratibu wa kitaifa wa hifadhi ya wazee itakayohusisha jamii nzima kuwalea wazee wetu ambao wengi wao baada ya kulitumikia Taifa letu kwa muda mrefu wanaishi katika dimbwi la umasikini wa kutisha. Hatua kwa hatua kila mzee atakuwa na haki ya kulipwa kila mwezi fao la uzee kwa ajili ya afya na hifadhi yake.

## 1.6. Kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu Kupata Elimu na Ajira

Serikali itakayoongozwa na CUF itatenga fungu maalum la kuwawezesha watu wenye ulemavu wapate elimu, matibabu na vifaa vya kuwapunguzia dhiki ya ulemavu walionao na pamoja na kutoa mafunzo stahiki waweze kuajirika na kuajiriwa katika fani mbali mbali kwa mazingira bora zaidi kuliko ilivyo sasa. Hii inatokana na ukweli kwamba zaidi ya asilimia 10 ya watanzania wote ni watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu wana mahitaji ya msingi sawa na watu wengine na wana mahitaji ya ziada kulingana na aina ya ulemavu walionao. Watu wenye ulemavu watashirikishwa kikamilifu kupata suluhisho

timilifu la changamoto zinazowakabili kwa kuwa CUF inaamini mfumo shirikishi kwa kila hatua.

### 1.7. Usimamizi wa elimu bora na matumizi ya teknolojia ya habari na mawasilino

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa watoto wote wa Tanzania wanakuwa na haki ya kupata elimu bora ya msingi, elimu ya sekondari na elimu ya juu. Kila raia atahimizwa kujiendeleza kielimu hasa kwa kutumia vizuri teknolojia ya habari na mawasiliano. Serikali ya umoja wa kitaifa itakayoundwa na CUF itatoa kipaumbele maalum katika kuwaendeleza kielimu wasichana na kujenga misingi imara ya kuendeleza elimu za hisabati, sayansi na teknolojia. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kwamba ifikapo 2025 asilimia 50 ya Shule za Umma nchini zinakuwa na Uwezo wa Kufundisha wanafunzi wake kwa njia ya TEHAMA na asilimia 100 ifikapo 2028. Hili litawezesha wanafunzi wengi kuendelea na masomo hata pale shule zitakapofungwa kwa dharura kama tulivyojifunza kupitia janga la CORONA.

### 1.8. Kusimamia maendeleo ya kiuchumi nchini

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itajenga uchumi wa kisasa wenye ushindani wa kitaifa na kimataifa na utakaohimili misukosuko ya utandawazi, unaokuwa kwa kasi bila kuharibu mazingira, na ambao utakuwa na manufaa kwa wananchi wote. Kukua kwa uchumi kunahitaji uongozi imara na utawala makini, mikakati na mipango mizuri ya maendeleo na utekelezaji mzuri wa mikakati na mpango hiyo. Kujenga mazingira mazuri ya kuwekeza, kufanya biashara na ushirikiano wa kimataifa bila kuathiri uhuru wa nchi yetu. Kuweka misingi ya utawala bora na utekelezaji wa sera utakaohakikisha kuwa uchumi unakuwa kwa asilimia 8 – 10 kila mwaka kwa miaka kumi ijayo na kufanikisha kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu mwaka 2030.

### 1.9. Usimamizi makini katika sekta ya kilimo na maendeleo ya viwanda

Dira ya Mabadiliko ya CUF inakipa kilimo nafasi ya pekee katika mikakati ya kukuza uchumi na hivyo kuwaondolea umasikini wananchi wengi na hasa wa vijijini, na kuhakikisha Taifa linakuwa na chakula cha kutosha na ziada ya kuuza nje ya nchi. Katika miaka mitano ijayo, bajeti ya sekta ya kilimo itakayoandaliwa na serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itakuwa kati ya asilimia 10-15 ya bajeti yote, na italenga katika kuimarisha maeneo yafuatayo:

- Utafiti na elimu kwa wakulima na huduma za ugani;
- Upatikanaji wa mbolea na pembejeo nyingine kwa bei nafuu;
- Kurahisisha upatikanaji wa zana za kilimo ikiwa ni pamoja na matrekta;
- Masoko ya uhakika ya ndani na nje ya nchi;
- Bei nzuri kwa wakulima;
- Kutengeneza barabara za vijijini; na
- Kusambaza umeme vijijini kwa kutumia nishati mbadala kama vile gesi iliyogunduliwa nchini, biogas inayotokana na mabaki ya mimea na vinyesi vya mifugo, jua na upepo.

Wakulima watahamasishwa kutumia TEHAMA kupata taarifa za masoko ya mazao na pembejeo, hali ya hewa na mafunzo ya kilimo bora. Dira ya mabadiliko ya CUF inakusudia kuasisi Mapinduzi ya kweli ya kilimo nchini, yatakayoongeza uzalishaji na tija kwa kuijenga upya sekta ya maendeleo ya viwanda. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF intaweka mkakati madhubuti wa kuanzisha na kuendeleza viwanda vinavyotumia malighafi ya ndani ya nchi na kuajiri watu wengi - kama vile viwanda vya nguo na mavazi, viatu na bidhaa za ngozi, vifaa vya matumizi ya nyumbani na vifaa vya umeme na elektroniki.

### 1.10. Kuimarisha miundo mbinu na kuhamasisha uwekezaji

Mafaniko ya kiuchumi kwa Taifa lolote lile hutegemea mfumo wa kisera na uwekezaji wa serikali katika sekta muhimu. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itawekeza kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha miundo mbinu - biarabara, reli, bandari, mawasiliano, nishati, maji, elimu na afya. Hiii itasaidia kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika shughuli za uzalishaji na biashara.

### 1.11. Kuimarisha Mazingira ya Uwekezaji, Kufanya Biashara na Ujasiriamali

Mazingira ya kufanya bishara Tanzania ni magumu sana. Kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia ya mazingira ya kufanya biashara ya mwaka 2020 – (Doing Business 2020), Tanzania ni nchi ya 141 kati ya nchi 190. Rwanda ni nchi ya 38 na Kenya ni nchi ya 56. Idadi ya kampuni mpya zinazosajiliwa kila mwaka zimepungua kutoka 8,890 mwaka 2015 na kufikia 5,278 mwaka 2018. Ili mazingira ya biashara nchini yawe rafiki zaidi na yenye gharama nafuu inabidi kuwepo na utashi wa kisiasa tokea uongozi wa juu wa nchi. Ni lazima uongozi wa juu wa nchi uridhike kuwa kuwa sekta binafsi ni muhimili muhimu wa uchumi wa nchi. Serikali isiwabughudhi wafanyabiashara na wawekezaji, alimuradi sekta binafsi inaheshimu na kufuata sheria za nchi. Kauli za vitisho na kuingilia kati shughuli za kibiashara kama ulivyofanyika kwenye ununuzi wa korosho kunapunguza imani ya sekta binafsi kuwa unaweza kuwekeza na kufanya biashara kwa taratibu na kanuni zinazotabirika.

### 1.12. Usimamizi wa rasilimali za Taifa na Nidhamu ya matumizi ya fedha za umma

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itajenga mfumo mzuri wa usimamizi na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, itaondoa misamaha holela ya kodi na itabana myanya ya ukwepaji wa kodi ikiwa ni pamoja na kupunguza idadi na viwango vya kodi na tozo mbalimbali. Aidha, itahakikisha kwamba

sekta ya madini inachangia asilimia 30 ya thamani ya mauzo ya madini kwenye mapato ya serikali. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itapambana na rushwa na ufisadi kwa kuweka mfumo imara wa kutambua viashiria na itahakikisha kuwa maliasili na rasilimali za Taifa zinatumiwa kwa umakini mkubwa na kwa manufaa ya wananchi wote.

Mimi binafsi kama Mgombea wa Urais kwa tiketi ya CUF nawaahidi Watanzania nikichaguliwa kuwa Rais nitajiwekea lengo la kuijengea heshima nchi yangu kwa kuimarisha utawala bora na uadilifu na kukuza uchumi unaotoa ajira kwa wingi na kuleta neema kwa wananchi wote. Kazi hii nitaifanya kwa uadilifu wa hali ya juu na kuhakikisha kuwa kwa mara ya kwanza Rais wa Tanzania atakapostaafu ataingia kwenye nafasi bora ya kupata tuzo ya Mo Ibrahim inayotolewa kwa kuongoza nchi vizuri kwa kuheshimu na kulinda haki za binadamu, kupambana na ufisadi kwa mafanikio, kukuza uchumi na kuutokomeza umasikini.

**HAKI SAWA NA FURAHA KWA WOTE: TANZANIA YENYE FURAHA INAWEZEKANA**

**Prof. Ibrahim Haruna Lipumba, Mgombea Urais wa CUF**

## 2. SEHEMU YA PILI

### MISINGI MIKUU YA UONGOZI WA NCHI

Katiba, Utawala wa Sheria, Mahakama, Haki za Binadamu, Uongozi Madhubuti wa Utumishi wa Umma, Mapato ya kodi na Nidhamu ya Matumizi ya Serikali, Mapambano dhidi ya Rushwa, Ulinzi na Usalama, na Masuala ya Mambo ya Nchi za Nje.

### 2.1. KATIBA

- Katiba ni SHERIA na ni mkataba maalum baina ya viongozi wa nchi na Raia wake. Raia wana jukumu la kuamua ni nani miongozi mwao akabidhiwe mamlaka ya kuongoza Serikali kwa maslahi ya Taifa zima. Katiba inapaswa kukusanya na kuelekeza mambo yote ya msingi na huku ikiwa na sifa ya kudumu kwa muda mrefu bila ya kuhitaji kufanyiwa marekebisho kila uchao.

- Katiba inatakiwa kukusanya masuala yote yanayowaunganisha wananchi wote bila kujali itikadi za vyama au tofauti nyingine zozote zile miongoni mwao. Katiba bora ni ile inayoandaliwa ikilenga kuboresha maisha ya watu wote, na kulinda haki zote za raia, na kuyapa fursa sawa makundi yote, na mtu mmoja mmoja aliyeko ndani ya nchi bila upendeleo.

**Hali ilivyo sasa**

Katiba tuliyonayo haikidhi matakwa ya wakati wa sasa.

- Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoandikwa mwaka 1977 ni katiba iliyotungwa katika kipindi cha mfumo wa chama kushika hatamu na ilikuwa na malengo ya wakati huo. Ni Katiba ambayo haikuwahusisha wananchi wakati wa kuandaliwa kwake. Maoni

yaliyokusanywa na tume za Jaji Nyalali na Jaji Kisanga hayakuzingatiwa katika jitihada za kuiboresha ili iendane na wakati. Katiba tuliyonayo haikidhi matakwa ya demokrasia ya wakati wa sasa na inawanyima raia haki ya msingi ya kuwania uongozi bila kupitia chama chochote cha siasa. Katiba tuliyonayo ina mikanganyiko mingi kiasi cha kujitokeza haja na ulazima wa kuandikwa upya.

- Kumekuwepo na malalamiko kutoka pande zote mbili za Jamhuri juu ya Muundo na utekelezaji wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Pamoja na jitihada zilizochukuliwa za kujaribu kuyapatia ufumbuzi matatizo na kasoro au kero hizo bado hakujapatikana ufumbuzi wenye kuleta tija na kuimarisha Muungano wetu, bali kuongeza mashaka zaidi. Hata hivyo marekekbisho yote ambayo yamekwisha fanyika hadi sasa kwenye katiba iliyopo hayajazingatia uwepo wa tatizo hili. Kwa kiasi kikubwa katiba haiheshimiwi na kufuatwa ipasavyo isipokuwa pale tu maslahi binafsi au ya makundi fulani yanapojitokeza.

- Sote tunakumbuka Mchakato wa Kupata Katiba Mpya ulioendeshwa kwa gharama kubwa katika Awamu ya Nne ya Uongozi wa nchi yetu ambao haukufika mwisho. Katiba ya Wananchi iliyotokana na Kazi nzuri iliyofanywa na Tume ya Jaji Joseph Sinde Warioba imewekwa kapuni na hakuna kilichozungumzwa kuhusu Katiba kwa miaka yote mitano ya Uongozi wa Rais John Pombe Magufuli. Matumaini ya kupata Katiba Mpya yametoweka kabisa chini ya uongozi wa sasa wa CCM.

**Msimamo wa CUF baada ya Uchaguzi Mkuu**

**Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa** mchakato wa uandaaji wa katiba mpya ya wananchi utafufuliwa katika kipindi cha miezi mitatu baada ya serikali kuapishwa. Katiba ya wananchi itaandaliwa kwa kushirikisha wadau wote katika mjadala wa kitaifa; ikiwa ni pamoja na wataalamu wa katiba, vyama vya siasa, madhehebu mbalimbali ya dini, wakulima, wafanyakazi, taasisi zisizokuwa za kiserikali, wananfuzi, na

makundi mbalimbali ya jamii kama wenye ulemavu, wastaafy, vijana, wanawake, wazee, na kadhalika. Mjadala huu utajikita katika kuboresha Rasimu ya Katiba ya Tume ya Jaji Warioba

- Maoni yatakayokusanywa katika mjadala huu ndiyo yatakayokuwa msingi mkuu wa maandalizi ya rasimu ya katiba mpya na kuzingatia matakwa ya misingi ya demokrasia ya kweli na uendeshaji wa nchi hapo baadaye kwa chama chochote kitakachopewa ridhaa ya kuongoza nchi. Katiba mpya itapatikana katika kipindi cha Bunge la mwaka 2022 na uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2024 na Uchaguzi Mkuu ujao wa mwaka 2025 utafanyika nchini tukiwa na Katiba Mpya.

- Katiba mpya itabainisha wazi kuwa Makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964 ndiyo sheria mama ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzanaia. Mantiki ya Makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964 ni kuwa na serikali tatu (3).

## 2.2. UTAWALA WA SHERIA

Utawala wa Sheria ni kuendesha mambo kwa kuheshimu, kulinda na kufuata Katiba na Sheria nyingine za nchi. Utawala wa sheria hauna huruma kwa mtu yeyote atakayekwenda kinyume na matakwa ya Sheria, Kanuni na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria. Katika Utawala wa Sheria hakuna atakayekuwa juu ya Sheria. Utawala wa sheria unamfanya kila mwananchi aziheshimu sheria na kuzifuata kwa ukamilifu wake.

### Hali ilivyo sasa

- Kuna kudorora kwa juhudi za kufuata utawala wa sheria toka ngazi za kitaifa hadi ngazi za wilaya, kata na mitaa/vijiji ambako hali ni mbaya zaidi. Watu wengi wasio na hatia wamepotea bila serikali kutoa taarifa za uchunguzi wa kupotea kwao. Matumizi ya vitisho, mabavu, na ukatili wa hali ya juu ni vitu vinavyokomaa na kuanza kuzoeleka ndani ya nchi yetu. Ni kawaida sasa wananchi kubambikiziwa kesi huku wakinyimwa

haki zote za msingi za mtuhumiwa kinyume na matakwa ya sheria. Viongozi wa serikali katika ngazi zote sasa wamekuwa kama miungu watu dhidi ya wananchi na raia wa kawaida.

- Katiba na Sheria nyingine za nchi zimekuwa zikifuatwa tu pale ambapo panaonekana kuna maslahi binafsi ya watawala.

**Msimamo wa Serikali ya CUF baada ya Uchaguzi Mkuu**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafuta sheria zote kandamizi na kuhakikisha haki za kila raia zinalindwa. Kupitia katiba ya wananchi serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaweka mazingira ya kuheshimu kikamilifu Utawala wa Sheria na ulinzi wa haki za binaadamu. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaongozwa kwa kufuata katiba na sheria kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

## 2.3. IDARA YA MAHAKAMA

Hali ilivyo sasa

Idara ya mahakama imekuwa ikilalamikiwa sana kwamba kupitia idara hiyo haki hazipatikani kirahisi. Pamekuwepo na ucheleweshwaji mkubwa wa kusikiliza kesi na kupelekea watuhumiwa kukaa mahabusu kwa muda mrefu. Malalamiko ya wananchi ni kuwa vitendo vya rushwa na ufisadi bado vimekithiri katika mahakama zetu.

Kwa upande mwingine maslahi ya watendaji wa idara ya Mahakama ni duni na mahakama zetu zimekuwa na tatizo la muda mrefu la kuwa na vitendea kazi visivyokidhi haja ikiwa ni pamoja na uchache wa majengo - tena mengi kati ya hayo yakiwa chakavu. Hakuna matumizi ya kutosha ya teknolojia ya kisasa ya usikilizaji wa kesi na ufuataliaji wa mwenendo wa mashtaka. Mahakama kutokana na muundo wake inakosa uhuru kamili wa kuiendesha idara hiyo.

**Msimamo wa Serikali ya CUF baada ya Uchaguzi Mkuu**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kwamba unaandaliwa mfumo wa mahakama utakaompa haki kila mwananchi kwa kufanya yafuatayo:

- Itaihakikishia idara ya mahakama uhuru wa kutosha katika kuendesha na kutoa maamuzi yake. Ili suala hili liwe wazi na lisilo na utata wowote, katiba itatamka wazi kuwa mahakama ndio taasisi yenye uamuzi na usemi wa mwisho juu ya suala lolote la kisheria.

- Itaandaa Katiba itakayotamka wazi kuwa ni ukiukwaji wa Katiba kwa Serikali kuvunja agizo, amri, au hukumu yoyote ambayo imeshapitishwa na mahakama.

- Itaanzisha mfumo wa kuajiri majaji, wasajili wa mahakama na mahakimu kupitia kamisheni ya ajira ya watendaji wa mahakama huku ajira za majaji na wasajili wa mahakama kuu na mahakama ya rufani zikihitaji kuthibitishwa na Bunge.

- Itaboresha maslahi ya watendaji wa Idara ya Mahakama kwa ujumla, kuongeza ajira ya watendaji zaidi wenye uwezo na kuanzisha mfumo wa kisasa wa matumizi ya Teknolojia katika uendeshaji wa kesi.

- Itafanya Marekebisho ya Sheria ili makosa madogomadogo yasiwe na hukumu za vifungo, na badala yake yawe yanalipiwa faini tu au kufanya kazi yoyote ya maendeleo itakayoamuliwa na mahakama iwapo mtuhumiwa atakuwa hana faini ya kulipa.

## 2.4. HAKI ZA BINADAMU

Uvunjifu na ukiukwaji wa Haki za binadamu ni tatizo kubwa nchini Tanzania. Hakuna chombo huru chenye nguvu cha kusimamia haki za binadamu. Tume ya haki za binadamu haina nguvu za kuweza kupambana na wavunjaji wa haki za binadamu. Wengi wa hawa ni watendaji wakuu wa serikali ambao wanalindwa na mfumo uliopo.

**Hali ilivyo sasa**

Kumekuwepo na mapungufu makubwa katika upatikanaji wa haki za banaadamu hapa Tanzania. Wakulima, wafugaji, wafanyakazi, wafanya biashara na wananchi wengine wamekuwa wahanga wakubwa wa hali hii. Mfano wa hali hii ni pale serikali ilipoamua kuzuia mauzo ya zao la korosho kwa wanunuzi binafsi misimu miwili iliyopita. Kitendo hiki kiliwaingiza wakulima wa korosho kwenye hasara kubwa na mpaka leo hakuna fidia yoyote inazungumziwa kuwafidia wakulima hao. Mfano mwingine ni pale serikali ilipoamua kuvamia na kupora fedha za wafanya biashara waliokuwa wanamiliki maduka ya kubadilishia fedha. Hadi leo hatma ya fedha zilizoporwa haijulikani. Mfano mwingine ni ule wa serikali kujimilikisha mafao yaliyotolewa na serikali ya Uingereza kwa waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ni wazi kabisa serikali haina mpango wowote wa kulipa stahiki za wafanyakazi hao ukizingatia kwamba ni zaidi ya miaka 30 sasa tangu mafao hayo yaliponyakuliwa na serikali huku sehemu kubwa ya wafanyakazi hao wakipoteza maisha siku baada ya siku. Ubambikiaji wa kesi na ucheleweshaji wa kusikilizwa kesi husika nao ni mfano mwingine wa jinsi haki za wananchi zinavyobakwa. Kwa mfano, ni zaidi ya miaka saba sasa tangu mashaikh wa UAMSHO wakamatwe na kuwekwa ndani. Hadi sasa upelelezi wa kesi aeti haujakamilika ili kesi ianze kusikilizwa!

Watanzania wengi wasio wanachama wa vyama vya siasa vilivyosajiliwa hawana haki ya kushiriki katika siasa kikamilifu kwa kuwa hawawezi kugombea nafasi yoyote ile ya uongozi wa kisiasa hadi wadhaminiwe na chama cha siasa kilichosajiliwa.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

Ni dhamira ya dhati ya Serikali itakayoundwa na CUF kurejesha thamani ya utu na haki za kila Mtanzania nchini. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha inasimamia mchakato wa kuwa na Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuhakikisha ndani ya Katiba hiyo kuna TUME

HURU YA HAKI ZA BINADAMU yenye uwezo wa kusimamia haki za Watanzania.

- Tume itakuwa na jukumu la kuchunguza ukiukwaji wa maadili na haki za binadamu na kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kurudisha haki hizo kwa walionyimwa na kuwafikisha mahakamani wale wote watakaoonekana kuwa na makosa ya uvunjaji wa haki hizo.

- Tume itakuwa na haki ya kuwaita na kuwahoji watuhumiwa wa uvunjifu wa haki za binadamu, bila kuomba ridhaa kwa mtu au Taasisi yoyote, ikiwa ushahidi ulioko mbele yake utaonyesha kwamba ni muhimu kufanya hivyo au baada ya kuombwa kufanya hivyo na mwathirika au mwakilishi wa muathirika.

- Tume itakuwa huru - bila kuwa na mfungamano wowote wa kisiasa, na wajumbe wake watapatikana kwa kuteuliwa kutokana na Mapendekezo yatakayotokana na Mchakato utakaobainishwa na Katiba Mpya na hatimae kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania.

- Tume itakuwa madarakani kwa muda wa miaka mitano na kila mwaka itapeleka taarifa ya kazi zake katika Bunge ambako zitawasilishwa na zitajadiliwa. Wajumbe wa Tume ya Haki za Binadamu watakaa madarakani kwa vipindi visivyozidi viwili au kama itakavyopitishwa na Bunge.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF Itaanzisha sheria itakayoibana serikali juu ya mwenendo wa kujitwalia kwa nguvu maeneo mbalimbali ya wananchi bila kuingia katika majadiliano ya kina na hatimaye kufikia makubaliano na wananchi wa eneo husika.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaanzisha sheria itayokataza vyombo vya dola kutumiwa na wanasiasa au maafisa wenyewe wa

vyombo hivyo kushambulia wananchi wanaoandamana au kugoma kwa njia za amani. Aidha wananchi watakuwa na haki ya kulalamika kwa njia mbalimbali za amani ikiwemo maandamano, mikusanyiko, na migomo.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaanzIsha sheria itakayowataka waajiri wote kuwa na mikataba ya ajira na wafanyakazi wao.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa Katiba Mpya inaeleza wazi kuwa vyombo vya habari baada ya kujisajili kama kampuni na kupata leseni ya biashara havitasajiliwa na taasisi nyingine yoyote ya serikali wala kuwekewa mipaka ya kijiografia katika utendaji na usambazaji wa shughuli zake ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF iItahakikisha kuwa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakuwa na kipengele kinachoruhusu mtu yeyote kuwa mgombea katika nafasi yoyote ya uchaguzi bila kipitia chama cha siasa.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa masuala ya haki za binadamu yanakuwa ni sehemu ya mtaala ya somo la uraia shuleni katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari kwa madhumuni ya kukuza uelewa juu ya haki za binadamu tangu awali ili vijana wakue katika utamaduni wa kuthamini wajibu na haki zao na za watu wengine.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itawaelimisha Watanzania na kusambaza Tangazo la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, na HATI ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika juu ya Haki za Binaadamu na Haki za Watu

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF iItafuta Sheria zote zenye chembechembe za Ukandamizaji wa Haki za Binadamu.

## 2.5. UONGOZI MADHUBUTI WA UTUMISHI WA UMMA

Nchi ambazo zimefanikiwa kukuza uchumi kwa kasi ya juu na kuwa na maendeleo kwa muda mrefu zimefanya hivyo kwa kuwa na uongozi adilifu wenye dira na ulio imara katika uamuzi, utekelezaji na kujifunza kutoka kwenye makosa waliyoyafanya nyuma na kujirekebisha. Uongozi wa nchi unawajibika kubuni sera kwa kuzingatia uhalisia na hali ya uchumi wa nchi, fursa zilizopo na vikwazo vinavyoikabili nchi katika kukuza uchumi wake. Uongozi makini utakaoweza kuchochea maendeleo ya muda mrefu unapaswa kuwa na subira, uwe na dira na mipango ya muda mrefu na ujikite katika lengo la kukuza uchumi utakaoleta neema kwa wananchi wote. Imethibitishwa kwamba maendeleo ya nchi yetu yamekuwa yakiathiriwa mno na matatizo ya viongozi na wafanyakazi wa serikali kutozingatia kwa kiasi kikubwa kanuni, sheria na uwajibikaji.

**Hali ilivyo sasa;**

Uwajibikaji na nidhamu kwa baadhi ya maofisa wa serikali bado viko chini. Huduma inayoweza kutolewa kwa saa chache inaweza kuchukua miezi kadhaa kupatikana. Matakwa ya kisiasa yameingilia sana mfumo wa upatikanaji wa watendaji wakuu katika utumishi wa umma, na wizi na ubadhirifu wa fedha za umma vimekuwa vikiendelea kwa muda mrefu bila kuchukuliwa hatua stahiki. Tumefikia mahala taasisi za umma za kuiwajibisha serikali kama Bunge kuwageuka wananchi na kutumika kufunika ubadhirifu unaofanywa na viongozi wa serikali. Sote tunakumbuka jinsi Mkaguzi na Mdhibiti mkuu wa Hesabu za Serikali aliyestaafishwa kabla ya muda, Profesa Musa Assad, alivyoingia katika mgogoro mkubwa na Bunge pale alipolikumbusha Bunge wajibu wake katika kuisimamia serikali. Wabunge wa CCM, kwa kutumia wingi wao ndani ya Bunge waliwasaliti

waliowatuma na kusimama kidete kutetea ubadhirifu uliokuwa unafanywa na serikali ya chama chao.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

- CUF itaunda serikali ya Umoja wa Kitaifa itakayoleta viongozi kutoka nyanja mbalimbali bila kujali itikadi zao za kisiasa. Hili litafanyika ili, pamoja na mambo mengine, kuhakikisha kuwa kila Mtanzania mwenye uwezo anapewa nafasi ya kuiletea nchi yake maendeleo na kusimamia vyema nidhamu na uwajibikaji katika utumishi wa umma kwa manufaa ya taifa letu.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaimarisha usimamizi kwa kuanzisha idara maalumu ya msimamizi mkuu wa huduma za serikali (Inspector General of Government Services), ambayo itakuwa na jukumu la kuchunguza na kufuatilia utendaji kazi wa vyombo vya Serikali, pamoja na kushughulikia malalamiko ya wananchi ili kuhakikisha maafisa wa vyombo vya serikali wanatenda kazi zao kwa ufanisi bila usumbufu kwa wananchi. Ofisi hii itafuatilia kila penye kulalamikiwa na maamuzi yatafanywa kwa kutumia vigezo kufanikisha malengo ya taifa.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itabadili mfumo wa kuwapata watendaji wakuu wa serikali. Pamoja na kuweka utaratibu wa usimamizi mzuri wa shughuli za serikali, itaweka utaratibu wa kuhakikisha serikali inapata watendaji wakuu wenye uwezo na walio bora.

## 2.6. VIONGOZI WA KUCHAGULIWA

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa ili kupata viongozi bora kuanzia Serikali kuu hadi Serikali za mtaa, chaguzi zote zinakuwa huru na za haki. Chaguzi zote zitasimamiwa na Tume ya Uchaguzi ya Taifa iliyo huru na yenye kutenda haki. Katiba mpya itaainisha namna ya

Wajumbe wa Tume Huru watakavyopatikana na ni lazima wathibitishwe na Bunge. Mwenyekiti wa Tume atachaguliwa kwa kura na Wajumbe wenzake kila baada ya miaka mitano au muda mwingine wowote ule utakaowekwa na katiba mpya.

## 2.7. VIONGOZI WA KUTEULIWA

Serikali ya CUF itahakikisha kuwa Katiba inaweka bayana jukumu la uteuzi wa viongozi waandamizi unaofanywa na Rais na kuthibitishwa na Bunge kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

- Rais atakuwa na jukumu la kuteua Baraza la Mawaziri la Muungano, Makatibu wakuu wa Baraza hilo, Mwanasheria Mkuu, Msimamizi Mkuu wa shughuli za Serikali na Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama vya Jamhuri ya Muungano.

- Rais pia atateuwa wakuu wa Mikoa na Wilaya wa Tanzania Bara hadi hapo Serikali ya Tanganyika itakapoundwa ambapo jukumu la uteuzi wa viongozi hao litahamia kwa Rais wa Serikali ya Tanganyika.

- Tume ya Ajira Serikalini itatoa mapendekezo ya uteuzi wa watendaji wakuu wengine wote katika idara, Mamlaka, na Tume za kudumu za Serikali baada ya nafasi husika kutangazwa na usaili kwa waombaji kufanyika. Rais atateua watendaji kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume. Aidha tume hii itahusika na kutoa mapendekezo ya uteuzi wa Bodi za mashirika mbali mbali ya Umma kwa kuzingatia vigezo vya kitaalamu na uzoefu.

## 2.8. MATUMIZI YA SERIKALI

Kasi ya maendeleo inategemea sana mipango mizuri inayo chagua vipaumbele vya kuewekeza mtaji uliopo.

**Hali ilivyo sasa**

**Matumizi mabaya ya fedha za umma**

Kiasi kikubwa cha fedha za walipa kodi bado zinatumiwa na serikali kugharamia matumizi ambayo hayana manufaa kwa taifa au miradi ambayo inaweza kutekelezwa na sekta binafsi au mashirika ya umma yanayoendeshwa kibiashara. Serikali ya CCM ina maradhi sugu ya kushindwa kutambua maeneo ya kupewa kipaumbele kwenye matumizi yake. Iko mifano mingi lakini hii michache ifuatayo inatosheleza kutumika kama kielelezo:

- Kitendo cha Serikali kutumia zaidi ya shilingi bilioni 1,350 kununulia ndege 11 zikiwemo Boeing Dreamliner 3, wakati idadi ya vitanda katika hospitali zetu haitoshelezi mahitaji na hakuna huduma bora za afya kwa Watanzania kwa ujumla, hakikuwa sahihi.

- Hakuna nidhamu katika utekelezaji wa bajeti. Tatizo la muda mrefu la bajeti ya Tanzania ni kuwa makadirio ni makubwa kuliko utekelezaji. Makadirio ya mapato ni makubwa kuliko hali halisi. Bajeti ya Maendeleo haitekelezwi kama ilivyopangwa. Maamuzi yanayohitaji matumizi ya fedha za serikali yanafanywa bila kuzingatia matumizi yaliyoidhinishwa na Bunge na kupitishwa kwenye bajeti. Uamuzi wa serikali kuhamia Dodoma ulianza kutekelezwa mwaka wa bajeti 2016/17 bila kutengewa fedha katika bajeti iliyopitishwa na Bunge.

- Sekta ya Kilimo ambayo ndiyo yenye kuajiri watu wengi haipewi kipaumbele. Katika miaka mitano ya uongozi wa awamu ya tano, kilimo kimetengewa chini ya asilimia 2 ya matumizi yote ya serikali. Mwaka 2003 nchi za SADC zilikubaliana kutumia alau asilimia 10 ya bajeti za serikali kwenye sekta ya kilimo. Tanzania haijafikia hata nusu ya lengo hilo.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itatumia fedha za wananchi kwa umakini na imedhamiria kupunguza kwa kiasi kikubwa gharama za kujiendesha ili fedha zitakazookolewa zielekezwe zaidi kwenye kujenga miundombinu ya maendeleo hasa barabara, reli, umeme, maji, bandari na Tekinolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); pamoja kuboresha huduma za jamii ikiwa ni pamoja na Elimu na Afya, kuasisi mapinduzi ya kilimo yatakayochochea ukuaji wa sekta ya viwanda na kuanzisha miradi mipya ya maendeleo yenye tija ya juu. Pamoja na mambo mengine hatua zifuatazo zitachukuliwa ili kufanikisha malengo haya:

    - Kuwa na Serikali ndogo yenye wizara zisizozidi 15.

    - Kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na kujenga mtandao utakaounganisha idara zote za Serikali ili kuongeza ufanisi katika utendaji.

    - Kupunguza matumizi yasiyo ya lazima. Ili kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima utaratibu wa 'zero budgeting' utafuatwa ambapo kila kipengele cha matumizi kinakuwa kimeelezwa uhalali wake kabla ya kukubaliwa.

    - Kupungaza Marupurupu na Mafao ya Viongozi. Katika mfumo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, uwezekano wa kuwa na viongozi wakuu wengi wastaafu ni mkubwa sana, na hivyo kulisababishia taifa kuwa na mzigo mkubwa katika kuwahudumia. Mathalani, kwa sasa Serikali za CCM (Muungano na Zanzibar) zinahudumia viongozi wakuu wastaafu wasiopungua thelathini kwa gharama ya mabilioni ya fedha kila mwaka. Ili kupunguza mzigo kwa Wananchi katika

kuwahudumia wastaafu hao, Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaandaa sera mahsusi ya viwango na muda maalum wa malipo usiozidi miaka 10 tangu kiongozi kustaafu. Baada ya muda huo mfuko wa kawaida wa huduma za jamii kwa wafanyakazi wa Serikali utatumika.

## 2.9. MAPAMBANO DHIDI YA UFISADI NA RUSHWA

### Hali ilivyo sasa

- Ufisadi na Rushwa siyo tu kwamba ni adui wa haki, lakini pia ni adui mkubwa wa maendeleo. Rushwa ni saratani inayoua uchumi na kuwanyima wananchi haki ya maisha na maendeleo. Pamoja na hatua zilizochukuliwa katika awamu zilizopita za serikali, rushwa bado imekithiri nchini. Katika awamu ya tano, ufisadi mpya umejitokeza wa kutumia dola kurubuni Wabunge na Madiwani wa vyama vya upinzani kuhamia CCM na kuwahakikishia kuwa watagombea nafasi walizoziacha kwa tiketi ya CCM na watashinda.

- Mapambano dhidi ya Rushwa na Ufisadi baina ya 2015 na 2020 yalipambwa na matukio ya kilichoitwa "Utumbuaji Majipu" na kuanzishwa kwa Mahakama ya Mafisadi. Hata hivyo utaratibu wa kushughulikia kadhia za Rushwa na Ufisadi haziridhishi wala hazioneshi haki ikitendeka. Watuhumiwa wa Ufisadi na Uhujumu Uchumi wamekuwa wakisota Mahabusu muda mrefu kwa kutopewa dhamana na kesi zimekuwa zikichukuwa muda mrefu sana bila kusikilizwa na kuhukumiwa. Utaratibu wa kuwataka washitakiwa/mahabusu wakiri makosa ili waruhusiwe kulipa fedha ili kuachiwa huru si utaratibu wa haki. Kwa upande mmoja utaratibu huu unaondoa hofu kwa MAFISADI PAPA kwa kuwa wanajua wakishitakiwa watajikomboa kwa kulipa sehemu ya walichowaibia wananchi. Kwa upande mwingine utaratibu huu unaweza kuwalazimisha wananchi wasio na hatia waamue kukiri makosa ili walipe fedha kwa kuwa muda

wanaokaa mahabusu ni mrefu mno na mwenendo wa kesi zao hautabiriki.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

Chanzo kikubwa cha rushwa ni ukosefu wa haki uliopea katika mifumo mbalimbali ya uendeshaji, ukiritimba wa madaraka, mishahara midogo ya watendaji Serikalini, maamuzi yasiyofuata taratibu na kutowajibishwa kwa wanaoshiriki katika vitendo vya rushwa. Vita dhidi ya rushwa itafanikiwa ikiwa visababishi vitaondolewa. Pamoja na mambo mengine, ili Kupambana na rushwa ni lazima tujenge mazingira ambayo yatatuhakikishia kuwa ‘MANYANGUMI' ya rushwa na ufisadi yanashughulikiwa kwanza kabla ya kwashughulikia ‘vijidagaa'. Ili kukabiliana na ufisadi katika sura zake zote Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua zifuatazo:

- **Itaiongezea nguvu Taasisi ya kupambana na Rushwa:**

Katiba mpya itaipa nguvu za kisheria Taasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuwajibika kwa Bunge badala ya Serikali. Mabadiliko haya yatalenga katika kuipa kinga dhidi ya hujuma zinazoweza kufanywa na Serikali kuvuruga shughuli zake za kiuchunguzi pale shughuli hizo zitakapoonekana kuwalenga baadhi ya maofisa wa Serikali au walio karibu na maafisa wa Chama kinachotawala. Pia TAKUKURU itapewa mamlaka ya kupeleka kesi mahakamani bila kuomba idhini toka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai (DPP).

- **Itawatangaza wanaotiwa hatiani kwa vitendo vya Rushwa:**

Wahalifu wote wa vitendo vya rushwa wanaotiwa hatiani watatangazwa hadharini kupitia vyombo vya habari vya Serikali.

- **Itabadili Muundo na Utendaji Serikali:**

Mabadiliko ya muundo na utendaji Serikalini kama yalivyoelezewa katika sehemu nyingine za Ilani hii yamelenga katika kuondosha ukiritimba wa madaraka na kuweka utaratibu wa wazi zaidi wa kiutendaji. Mabadiliko haya yatakuwa silaha muhimu katika kubomoa mazingira ya rushwa.

- **Itaboresha maslahi ya Wafanyakazi:**

Marekebisho ya mishahara ya watumishi wa Serikali yatasaidia kwa kiwango cha juu kufifisha rushwa katika ngazi za chini na kati za utendaji Serikalini.

- **Itafanya marekebisho ya kisera katika sekta mbalimbali:**

Marekebisho ya kisera katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii na kuandaa mfumo mzuri wa uchumi unaotoa tija na neema kwa wananchi wote, kwa kuzingatia upunguzaji wa gharama za maisha, utapunguza ushawishi kwa wananchi kujitumbukiza katika vitendo vya rushwa na ufisadi. Kwa mfano, sera ya kutomiliki zaidi ya kiwanja kimoja cha makazi katika mji mmoja, bila ya kuwa na sababu maalum, kutapunguza kwa kiasi kikubwa rushwa na ufisadi wa kutisha unafanyika katika sekta ya ardhi.

## 2.10. ULINZI NA USALAMA

Suala la Ulinzi na Usalama wa Taifa linapaswa kupewa uzito unaostahili. Kwa muda mrefu sasa serikali ya CCM imeshindwa kutekeleza wajibu wa kuhakikisha kuwa vikosi vyetu vya Majeshi ya Ulinzi na Usalama -JWTZ, Polisi, Magereza, Zimamoto, Uhamiaji na JKT vinaimarika na kuwa vya kisasa zaidi.

### Hali ilivyo sasa

Vikosi vyetu vya majeshi hivi sasa vimeathiriwa na ukosefu wa vifaa vya kutendea kazi, mafunzo duni na maslahi yasiyoridhisha. Makazi ya askari wetu bado si ya kuridhisha na yanakwenda kinyume na haki za msingi za binadamu. Mishahara na marupurupu mengine ya askari si yenye kukidhi haja ukilinganisha na wito na maadili ya kazi zao. Askari wengi wastaafu

wanaishi maisha yanayokatisha tamaa kutokana na kutokuwepo na mipango madhubuti ya kuuenzi muda walioutumia kulitetea taifa letu. Huduma za uokoaji nchini ziko katika hali mbaya kabisa. Udhaifu mkubwa uliojionesha wakati wa kushughulikia majanga kama ya MV Nyerere, mafuriko ya Mkoa wa Lindi, ajali ya lori la mafuta ya petroli Morogoro ni kielelezo halisi cha hali hii.

**Dira ya mabadiliko ya CUF**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kwamba Vikosi vya ulinzi na usalama vinapatiwa mafunzo bora na vifaa vya kisasa ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa vyombo vya usafiri, vyombo vya mawasiliano, na sare vinatosheleza mahitaji ili viweze kukidhi haja ya ulinzi dhidi ya mashambulizi ya ardhini, baharini na angani; na viweze kuimarisha usalama wa raia na mali zao.

- Kikosi cha wanamaji cha polisi (police marine) kitaimarishwa ili mbali ya kutoa msaada kwa kikosi cha jeshi la wanamaji dhidi ya mashambulizi ya baharini pale yatakapotokea, kiweze pia kuboresha doria katika ukanda wote wa pwani na kwenye maziwa makuu kwa madhumuni ya kutoa msaada kwa vyombo vya kiraia vya uvuvi na usafirishaji wakati wa matatizo (rescue operations), na kuzuia uharamia wa majini, biashara ya mihadharati na magendo ya rasilimali za Taifa kutolewa nje ya mipaka ya nchi bila kufuata utaratibu.

- Askari wa vikosi vyote nchini watalipwa kima cha chini cha mshahara unaokidhi mahitaji ili waweze kutekeleza majukumu na wajibu wao kwa ufanisi na kujituma. Aidha, askari wetu wote watapatiwa makaazi ya kuheshimika na kupewa mafunzo ya kutosha juu ya wajibu, sheria na maadili ya kazi yao ili matendo ya askari kuwaonea raia na kuvunja haki zao za msingi yasijitokeze.

- Kikosi cha Zima Moto kitahuishwa, kupanuliwa na kuimarishwa ili kiweze kutoa huduma za uokoaji kikamilifu. Hii itakuwa ni pamoja na

kuongeza idadi ya askari, kutoa mafunzo ya kisasa yanayohusiana na shughuli zote za uokoaji na kukipatia kikosi hicho vifaa vya kisasa kabisa vya uokoaji.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itapitia upya viwango vya pensheni za wastaafu kutoka vikosi vya ulinzi na usalama, na kusimamia kuona kuwa wanapata haki zao stahiki bila ya kusumbuliwa.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaanzisha mafunzo ya kijeshi ya hiari kwa Wananchi wote watakaopenda ili wawe askari wazuri pindi itakapohitajika.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itasimamia kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kupokea na kuweka kumbukumbu ya matukio ya uhalifu na kuyashughulikia kisayansi zaidi.

## 2.11. MAMBO YA NCHI ZA NJE

Hakuna Taifa duniani linaloweza kujitenga katika mashirikiano na mataifa mengine. Hili linatokana na utegemezi na muingiliano wa masuala ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, kibiashara, mabadiliko ya tabia nchi, maambukizi ya maradhi, na ulinzi na usalama. Maendeleo ya mwanadamu, ulinzi na usalama, na kusaidiana wakati wa majanga kunalifanya kila taifa lilazimike kuwa na mahusiano na mataifa mengine.

### Hali iliyo sasa

- Tanzania bado haijawa na sera thabiti ya masuala ya mahusiano ya mambo ya nchi za nje yenye kuleta tija na maslahi zaidi ya kiuchumi kwa Watanzania. Katika awamu ya tano mahusiano ya kiuchumi na kijamii na nchi za nje na asasi za kimataifa yamedorora.

- Ushirikiano wa kimataifa limefanywa kuwa ni suala la Muungano chini ya wizara ya mambo ya nchi za nje na ushrikiano wa kimataifa na hivyo

kuinyima Zanzizbar fursa na uhuru wa kujiendeleza kwa kuwa na mahusiano ya kiuchumi na nchi na mashirika mbalimbali ya kimataifa.

- Baada ya miaka 56 ya Muungano kumekuwepo na matumizi makubwa yanayotokana na uendeshaji wa ofisi zetu za kibalozi na kuwa na mabalozi ambao kimsingi wanashindwa kufanya ushawishi mkubwa wa kisiasa na kiuchumi ili kulisaidia taifa letu kusonga mbele katika sekta mbalimbali. Uteuzi wa mabalozi umekuwa wa kisiasa zaidi kuliko kufanikisha jukumu la kulinda na kuboresha maslahi ya Tanzania kiuchumi na kiusalama.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaendeleza mahusiano mazuri na mataifa mbalimbali kwa kushughulikia dosari zilizopo na kujielekeza zaidi katika kuhifadhi na kulinda amani ya dunia na usalama wake, kuhifadhi mazingira, kutumia fursa za kiuchumi kuliendeleza taifa na dunia kwa ujumla, kujilinda na athari za mabadiliko ya tabia nchi, na maambukizi ya maradhi. Diplomasia ya Tanzania itajikita katika kuhakikisha taifa letu linanufaika kiuchumi, kibiashara na kuboresha huduma za jamii. Tutashirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu nchini Tanzania.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaendelea na uungaji mkono na kushiriki kikamilifu katika Jumuiya na mashirika mbalimbali ya kimataifa ikiwa ni pamoja na UN, WHO, AU, EAC, SADC, Commonwealth, na kadhalika; kwa ajili ya kutekeleza maamuzi ya pamoja yanayofikiwa na kufaidika na manufaa yatokanayo na uwepo wa jumuiya hizi.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanya maslahi ya kiuchumi kuwa nguzo muhimu ya Sera ya Mambo ya Nje ya Tanzania na kwa hivyo mahusiano yetu na nchi nyingine kwa kiasi kikubwa yatalenga

katika kuimarisha uchumi na kukuza biashara. Kwa kweli Siasa itatumikia Uchumi na siyo Uchumi kutumikia Siasa.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa kunakuwepo na uhusiano mzuri na nchi jirani bila ya kujali itikadi au mfumo wa siasa na uchumi wa nchi hizo. CUF inaamini kwamba mustakabali wa Tanzania utaendelezwa vizuri zaidi kwa kutilia mkazo ushrikiano na nchi jirani ikiwa ni pamoja na kuunga mkono juhudi za kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itatoa ushirikiano wa kipekee na mafungamano ya karibu na nchi zote zitakazoonyesha nia ya kweli ya kuisaidia Tanzania, pamoja na zile nchi zenye uhusiano wa kihistoria na nchi yetu na kuyapa kipaumbele masuala ya usuluhishi na utatuzi wa migogoro katika nchi zote zinazopakana na Tanzania. Mafanikio ya mpango huu siyo tu kwamba yatasaidia kudumisha amani katika nchi zinazohusika, lakini pia yatajenga mazingira mazuri zaidi ya kiuchumi na kisiasa kwa wananchi wa eneo lote hili, ikiwa ni pamoja na kuipunguzia nchi yetu mzigo mkubwa wa wakimbizi wanaokimbia makwao kutokana na hali mbaya ya usalama.

- Ushirikiano wa Kimataifa katika Nyanja za uchumi na biashara utoandolewa kuwa suala la Muungano, ili kuziwezesha pande zote mbili za Muungano kunufaika kikamilifu na mikataba inayogusa maeneo hayo.

# 3. SEHEMU YA TATU

## 3.1. UCHUMI

### HALI YA MAISHA YA MTANZANIA KWA UJUMLA NA SEKTA MUHIMU ZA UCHUMI

- Mapambano ya kudai uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar yalilenga kutokomeza maadui wakubwa watatu - ujinga, maradhi na umaskini. Baada ya miaka 59 ya uhuru wa

Tanganyika na miaka 56 ya Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, umaskini umekithiri, asilimia 30 ya watoto wa Tanzania wana udumavu, na vifo vya kina mama wajawazito bado ni tatizo kubwa. Watoto wanakwenda shule lakini hawapati elimu.

- Takwimu za serikali zinaeleza kuwa katika awamu ya tano uchumi umekua kwa wastani wa asilimia 6.9 kila mwaka. Wananchi wengi hawaamini kama uchumi unakua kwa kasi hiyo. Wanaona hali ya maisha inazidi kuwa ngumu. Vyuma vimekaza. Biashara haitoki. Hata nyumba za Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) ambazo zilikuwa ngumu kuzipata bila kutoa rushwa sasa nyingine hazina wateja mpaka zinatangazwa kwenye magazeti na mitandao ya kijamii. Wafanya biashara wakubwa na wadogo wanalalamika kuwa biashara haitoki. Mzunguuko wa fedha umepungua.

- Benki ya Dunia inakadiria kuwa Pato la Taifa la Tanzania limeongezeka kwa asilimia 5.4 mwaka 2018 na asilimi 5.6 mwaka 2019 na siyo asilimia 7 inayoelezwa na serikali. Kwa sababu ya athari za virusi vya Corona katika uchumi wa dunia, Pato la Taifa la Tanzania litaongezeka kwa asilimia 2.5 tu mwaka 2020. Hii ni chini ya ongezeko la idadi ya watu la asilimia 3. Kwa sababu ya ongezeko kubwa la idadi ya watu ikilinganishwa na ongezeko la Pato la Taifa, ina maana kuwa idadi ya watu maskini itaongezeka.

- Ukuaji wa uchumi katika nchi zinazoendelea huambatana na kuongezeka kwa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi. Uuzaji wa bidhaa nchi za nje ambao tangia hapo siyo wa juu sana, sasa umepungua. Mwaka 2018 Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya dola bilioni 4.4 ukilinganisha na mauzo ya dola bilioni 5.9 mwaka 2012. Sera za serikali zinachangia katika kudumaza uuzaji wa bidhaa nchi za nje. Kwa mfano kwa sababu ya serikali kuingilia kati ununuzi na uuzaji wa korosho, mauzo ya korosho nchi za nje yalipungua toka

dola milioni 529.7 mwaka 2017 na kufikia dola milioni 109.6 mwaka 2018.

- Ukuaji wa uchumi wa Tanzania haujaambatana na kasi kubwa ya kupungua kwa watu masikini. Idadi ya watu masikini kwa kutumia kipimo cha taifa cha umasikini (mtu mzima kutumia shilingi 50,000/ au zaidi kwa mwezi) imeongezeka toka watu milioni 12.3 mwaka 2011 na kufikia watu milioni 14 mwaka 2020.. Kwa kutumia kipimo cha kimataifa cha umaskini, Watanzania zaidi ya milioni 27 ni masikini. Kuporomoka kwa uchumi kwa sababu ya Corona kutaongeza idadi ya watu masikini nchini.

- Utafiti uliofanywa na serikali mwaka 2016 kuhusu umaskini wa watoto (Child Poverty in Tanzania) ulibaini kuwa asilimia 74 ya watoto wa Tanzania wanaishi katika mazingira ya umaskini kwa tafsiri pana inayojumuisha lishe, afya, hifadhi iliyo salama, elimu, mazingira, maji na makazi.

- Jitihada za kuiendeleza nguvu kazi ya wanawake kiuchumi ambao ndio wanachukua asilimia zaidi ya 51 ya watanzania wote hazijazaa matunda yanayotakiwa. Sehemu kubwa ya njia zote za uchumi zinashilikiwa na wanaume. Kundi kubwa la wanawake wako nyuma kielimu na kitaaluma-matokeo yake wanaendelea kukaa majumbani au kujishughulisha na shughuli ndogo ndogo za uzalishaji zisizo na tija. Aidha, taasisi za fedha nyingi ziko mijini na benki inayoitwa ya wanawake ipo Dar es salaam. Mikopo wanayopewa ina riba kubwa lakini pia hakuna mfumo sawia wa kiuchumi unaopelekea shughuli za kiuchumi kuleta maslahi stahiki. Mwisho wa siku mikopo hiyo huwapelekea wengine kukimbia miji na au kupokonywa mali zao (kufilisiwa).

- Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Miaka mitano 2016/17-20/21 ulizinduliwa mwaka 2016. Mpango huo una dhima ya Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Kiuchumi na Maendeleo ya Watu - Nurturing Industrialisation for Economic Transformation and Human Development."

- Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ulisisitiza umuhimu wa utawala bora. Mpango ulieleza katika miaka 10 ya kati ya 2005 na 2015 (kipindi cha uongozi wa Rais Kikwete) kulikuwepo na ongezeko la uhuru wa kujieleza na kutoa maoni na kuimarika kwa maadili ya demokrasia nchini ikiwa ni pamoja na wananchi kutaka serikali na viongozi kuwajibika.

- Pamoja na Mpango wa pili kusisitiza demokrasia kama nyenzo ya uwajibikaji katika kutekekeza Mpango wa Pili wa Miaka Mitano, ujenzi wa demokrasia haukuwa kipaumbele cha awamu ya tano. Katika hotuba yake ya kuzindua Bunge la 11 tarehe 20 Novemba 2015, Rais Magufuli alijadili kero 22 za wananchi alizozibaini wakati wa kampeni. Hata hivyo Rais hakuzungumzia kabisa suala la kuimarisha demokrasia kama nyenzo ya kukuza uchumi na kuleta maendeleo. Katika hotuba yake yote neno demokrasia hakulitaja kabisa.

- Katika dibaji ya Mpango wa Pili wa Miaka Mitano, imeelezwa kuwa tatizo kubwa ya Mipango ya Nyuma ni utekelezaji hafifu wa mipango yetu. Tatizo la utekelezaji limeendelea kuathiri Mpango wa Pili wa miaka Mitano.

- Mpango wa Pili uliteua baadhi ya miradi na kuipa sifa ya miradi kielelezo (flagship projects). Miradi hii ni ile mikubwa na ambayo matokeo yake yanatarajiwa kusukuma au kuwezesha ufanisi wa utekelezaji na uwekezaji wa miradi mingine. Miradi hii ni: Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma; Mradi wa Chuma Liganga;

Maeneo Maalum ya Uwekezaji (Bagamoyo na bandari yake, Mtwara na bandari yake, Mwanza na Kigoma); Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini; Ujenzi wa Reli ya Kati na matawi yake kwa kiwango cha Standard Gauge, Mji wa Kilimo - Mkulazi; Ufufuaji wa Shirika la Taifa la Ndege; na Kusomesha vijana wengi katika fani na ufundi stadi unaohitajika katika maeneo ya kipaumbele.

- Mpango mkubwa wa kufua umeme Stiglers Gorge hauko kwenye Mpango wa pili lakini imeanzishwa katikati ya Mpango. Miradi iliyokuwemo katika Mpango wa Kwanza lakini haikutekelezwa na kuhamishiwa Mpango wa Pili na bado haijatekelezwa ni pamoja na Bandari ya Bagamoyo na Eneo lake la Uwekezaji na Mradi wa Chuma Liganga.

- Katika utekelezaji wa Mpango, Bajeti ya Maendeleo ilitarajiwaa kuwa ya wastani wa shilingi trilioni 11.8 kila mwaka. Matumizi halisi yamekuwa ya wastani wa shilingi trilioni 8.3 kwa mwaka katika miaka minne ya mpango sawa na asilimia 70 ya lengo.

- Malengo muhimu ya Mpango wa Pili hayatafikiwa. Lengo la ukuaji wa Pato la Taifa la asilimia 10 mwaka 2020 halitafikiwa. Ukuaji wa Uchumi katika miaka minne 2016-2019 umekuwa wastani wa 6.9 kila mwaka. Sekta ya viwanda ilitarajiwa ifikie ukuaji wa asilimia 10.5 mwaka 2020 lakini imekua kwa asilimia 5.7 mwaka 2019. Lengo la Mpango ni Sekta ya Kilimo ikue kwa wastani wa asilimia 7.6 mwaka 2020 lakini kilimo kilikua kwa wastani wa asilimia 5.1 katika kipindi cha 2016-19.

- Hotuba ya Rais alipozindua Bunge ilieleza mwongozo mzuri wa viwanda vitakavyojengwa. Viwanda hivyo ni pamoja na vinavyotumia malighafi inayopatikana nchini, viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumiwa na wananchi wengi, na viwanda vinavyoajiri watu wengi. Miaka karibu mitano ya baada ya

hotuba hiyo uzalishaji wa nguo umeporomoka toka mita za mraba 119.5 milioni mwaka 2014 na kufikia mita za mraba 45.4 milioni mwaka 2019. Ikiwa hatuwezi kujenga mazingira ya kuongeza uzalishaji wa nguo ambayo malighafi yake inapatikana nchi kwa urahisi, Tanzania yenye viwanda itaendelea kuwa ndoto.

- Mpango uliweka lengo la kuzalisha umeme MW 4,915 mwaka 2020 ukilinganisha na uzalishaji wa MW 1501 mwaka 2015. Mwaka 2019, uwezo wa kuzalisha umeme nchi nzima umeongezeka na kufikia MW 1,601 tu. Ni wazi kabisa lengo la Mpango wa pili halitafikiwa hata kwa asilimia 5.

- Kwa ujumla bajeti ya serikali haikuongozwa na lengo la kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo. Hotuba za bajeti za Wizara nyingi hazijikiti katika kueleza utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo umefikia wapi. Hotuba ya Rais ya kufunga Bunge tarehe 19 Juni 2020 ya zaidi ya saa mbili haikutaja hata uwepo wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Miaka Mitano.

- Awamu ya tano imeipa kipaumbele Miradi mitatu. Ununuzi wa Ndege, Ujenzi wa reli kwa kiwango cha Standard Gauge na ufuaji wa umeme Stieglers gorge.

- Usafiri wa ndege kimataifa una ushindani mkubwa. Hata kabla ya COVID-19 makampuni ya ndege yamekuwa yanapata hasara. Kuimarisha usafiri wa ndege ndani ya nchi ni jambo jema. Sekta binafsi inaweza kushiriki kikamilifu katika eneo hili. Kushindana katika usafiri wa ndege kimataifa unahitaji mtaji mkubwa wa kununua ndege nyingi, na pia kuwa kitovu cha usafiri (hub) kinachokusanya wasafiri wengi wanaoenda miji mbalimbali. Siyo rahisi kuifanya Dar es Salaam au KIA kuwa kitovu cha usafiri wa ndege kama ilivyo Addis Ababa.

- COVID-19 na mabadiliko ya teknolojia ya TEHAMA inayowezesha mikutano kufanyika kwa njia ya mtandao inatarajiwa kupunguza sana abiria wanaosafiri kwa ndege hata baada ya maradhi haya kutoweka. Mashirika mengi ya ndege yana wakati mgumu. Bila msaada wa serikali yatafilisika. Huu si wakati mzuri kuwekeza kununua ndege za safari za kimataifa na ukategemea kurudisha gharama ya ununuzi na kupata faida.

- Mradi wa kujenga reli ya Standard gauge ni uwekezaji wa gharama kubwa. Kiuchumi ukarabati wa reli iliyopo na kuifanya ijiendeshe kwa ufanisi ungetangulia ujenzi wa reli mpya. Ujenzi wa reli ya SGR unahitaji uhakika wa fedha za kuigharamia.

- Sababu ya wataalam wa TANESCO kuweka utekelezaji wa mradi mkubwa wa Stigler Gorge miaka ya mbali ni makadirio ya mahitaji ya umeme Tanzania. TANESCO ilikadiria kuwa mahitaji ya juu ya umeme mwaka 2020 ni MW 2260 chini ya nusu ya lengo la mpango wa pili wa kuzalisha MW 4915.

- Utaratibu mzuri ungezingatia kutekeleza miradi midogo na ya kati kama vile kufua umeme MW 600 Mtwara kwa kutumia gesi wakati serikali inajipanga kutekeleza mradi mkubwa wa Stigler's Gorge. Fedha za uhakika za mradi hazipo bali zinategemea kutengewa katika bajeti ya kila mwaka.

- Pamoja na jitihada za kuongeza ukusanyaji wa kodi, mapato ya ndani hayakidhi hata kugharamia matumizi ya kawaida na ulipaji wa madeni, achilia mbali kugharamia miradi ya maendeleo. Hakuna fedha inayobaki kutokana na makusanyo ya ndani kugharamia Mpango wa Maendeleo. Kimsingi utekelezaji wa miradi ya maendeleo unategemea kukopa ndani na nje ya nchi. Kwa sababu hii deni la taifa linazidi kututumka. Hivi sasa kila

Mtanzania anadaiwa kiasi cha wastani wa shilingi laki tisa (900,000.00) kutokana na madeni haya!

Utaratibu mzuri ni kuhakikisha miradi mikubwa inafanyiwa uchambuzi yakinifu wa kina kuhakikisha tija ya miradi hiyo na kupata fedha za uhakika za kuitekeleza. Wizara ya Fedha ilijenga uwezo wa kufanya upembuzi yakinifu wa miradi iliyofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia mfuko wa Millennium Challenge Account. Uchambuzi wa miradi yote uliwekwa wazi kwenye tovuti ya Tanzania MCA.

- Mazingira ya kufanya bishara Tanzania ni magumu sana. Ripoti ya Benki ya Dunia ya mazingira ya kufanya biashara ya mwaka 2020 - Doing Business Report 2020, inaitaja Tanzania kuwa ni nchi ya 141 kati ya nchi 190. Rwanda ni nchi ya 38 na Kenya ni nchi ya 56. Haitoshi kuwa na "mpangokazi wa kuboresha mazingira ya biashara (Blueprint for the Regulatory Reforms to improve the Business Environment) ili mazingira ya biashara nchini yawe rafiki zaidi na yenye gharama nafuu." Inabidi kuwepo na utashi wa kisiasa tokea uongozi wa juu wa nchi kuwa sekta binafsi ni muhimili muhimu wa uchumi wa nchi. Serikali isiwabughudhi wafanyabiashara na wawekezaji, alimuradi sekta binafsi inaheshimu na kufuata sheria za nchi. Kauli za vitisho na kuingilia kati shughuli za kibiashara kama ilivyofanyika kwenye ununuzi wa korosho na kwa wamiliki wa maduka ya kubadilishia fedha, kunapunguza imani ya sekta binafsi kuwa unaweza kufanya biashara bila kubughudhiwa.

- Kukusanya kodi ni muhimu katika kutekeleza mipango ya serikali. Ni muhimu ukusanyaji wa kodi usiue uwekezaji na biashara na kuikatisha tamaa sekta binafsi. Hivi sasa mfumo mbovu wa kodi unaowanyanyasa karibu walipa kodi wote na unazuia maendeleo ya sekta binafsi.

- Serikali ya CCM imeshindwa kutumia jiografia nzuri ya nchi yetu kuinua uchumi wa nchi na kuliongezea taifa mapato. Kilimo ambacho kimsingi ndio sekta tegemeo kwa Watanzania walio wengi hakijasimamiwa ipasavyo na badala yake kumekuwa na kauli mbiu za kisiasa zaidi kuliko utekelezaji wa sera za kuwainua wakulima. Yaliyotokea kwa wakulima wa korosho na mbaazi ni kielelezo cha Serikali ya CCM kutokuwa tayari kumkomboa mkulima na sekta ya kilimo kwa ujumla. Kilimo kimeendelea kutengewa Bajeti ndogo sana, chini ya asilimia 2 miaka yote mitano iliyopita.

**Dira ya mabadiliko ya CUF**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa na hasa UNDP, UNICEF, WHO, UNESCO, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na wadau wengine wa maendeleo itaanda mpango wa kufanikisha Malengo yote ya Maendeleo Endelevu ifikapo 2030. Serikali Kuu itashirikiana na halmashauri zote kuandaa mpango wa kila hamashauri kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya Maendeleo Endelevu.

- Serikali ya Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na CUF itaandaa bajeti zinazotekelezeka. Mfumo wa kodi na utekelezaji wake utazingatia uwazi na kutoathiri uwekezaji na biashara yenye tija. Mamlaka ya kodi itaelekezwa kujenga mazingira ya walipa kodi kufurahia kuwajibika kutimiza wajibu wao.

- Kwa kuweka mazingira mazuri ya kukuza uchumi na kukusanya kodi, tutaongeza ukusanyaji wa kodi toka wastani wa asilimia 12.1 kwa mwaka katika kipindi cha awamu ya tano na kufikia asilimia 17 mwaka 2024/25. Serikali itakusanya alau asilimia 2 ya Pato la Taifa kama mapato yasiyotokana na kodi. Lengo la mapato ya

serikali ukijumlisha na mapato ya halmashauri yafikie asilimia 20 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25.

- Miradi mikubwa iliyoanzishwa na serikali ya awamu ya tano ikiwemo ujenzi wa reli kwa kiwango cha standard gauge na ufuaji wa umeme Stigler's Gorge itatafutiwa fedha za uhakika za kuigharamia toka Benki ya Maendeleo ya BRICS na taasisi nyingine za kimataifa.

- Serikali itaipa fursa sekta binafsi kuwekeza katika maeneo yanayoendeshwa kibiashara na kwa ushindani. Serikali itajikita zaidi katika ujenzi wa miundombinu ya usafiri, nishati na maji; uimarishaji wa sekta ya elimu, sayansi na teknolojia, huduma za msingi za afya na ulinzi wa mazingira.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaboresha mazingira ya kuwekeza na kufanya biashara. Itajiwekea lengo la kutoka nchi ya 141 na siyo zaidi ya nchi ya 50 kati ya nchi 190, katika wepesi wa kufanya biashara kama inavyoanishwa na Taarifa ya Benki ya Dunia ya *Doing Business*

- Chama cha CUF kinatambua kuwa robo tatu ya Watanzania wote ni wakazi wa maeneo ya vijijini. Hii ina maana kwamba kimsingi tunapozungumzia umasikini wa Mtanzania kwa kiasi kikubwa mlengwa ni Mtanzania wa kijijini. Watanzania wengi walioko vijijini ama ni wakulima, wafugaji, wavuvi, au ni wenye kufanya shughuli mchanganyiko. Sehemu kubwa ya shughuli zote hizi inahusu uzalishaji na kwa hivyo basi kusudio la kukabilaina na kupunguza umasikini ni lazima lilenge kwanza kwenye kuboresha uzalishaji; na pili kutafuta masoko ya uhakika. Kuboresha uzalishaji kuna maana ya kuboresha mipango, miundombinu, na ushauri wa kitaalamu, na kusimamia upatikanaji wa masoko na bei nzuri ya bidhaa za wakulima. Ili kuendeleza sekta ya kilimo, itatengewa

alau asilimia 10 ya bajeti ya serikali. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itayasimamia ipasavyo maeneo haya na Halmashauri za Wilaya zitakua ni vituo muhimu katika kufanikisha mkakati huu.

- Kutafanyika mabadiliko ya msingi ambapo Halmashauri zitabadili mwelekeo kutoka kuwa ni asasi zinazoshughulikia zaidi masuala ya huduma za kiutawala na kuwa ni asasi zinazoshughulikia zaidi mkakati wa kuinua hali za maisha za wananchi.

- Chini ya mwelekeo huu mpya kila halmashauri itawajibika kuweka mazingira yatakayovutia uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo vitakavyotumika kuongeza thamani ya mazao mbalimbali yanayozalishwa vijijini. Mathalani, badala ya muhogo kuuzwa kama muhogo unaweza kusindikwa na kuuzwa kama wanga, badala ya asali kuuzwa kama asali inaweza kutiwa kwenye mchanganyiko wa mazao mengine ya asili yanayopatikana katika maeneo husika na kutengeneza vipodozi vyenye ubora wa juu, korosho zinaweza kubanguliwa na kufungwa vizuri badala ya kuuzwa nje zikiwa katika hali ghafi, nakadhalika. Aidha ajira itakayopatikana kwenye viwanda hivi itaongeza mzunguko wa fedha wa kudumu kwenye maeneo ya vijijini na hivyo kuchochea ukuaji wa ajira katika sekta zingine zisizo rasmi.

- Mfumo usioridhisha wa kodi utafanyiwa marekebisho ili mabilioni ya shilingi yanayopotea hivi sasa kutokana na misamaha holela ya kodi yaokolewe na kuelekezwa kwenye kuinua hali za maisha ya watanzania wanaoogelea kwenye dimbwi la umasikini usio na dalili ya kumalizika hata kwa miaka mia moja ijayo.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaanza utaratibu wa kuwalipa pensheni kila mwisho wa mwezi na kuwatunza wazee wanaofikia miaka 70 na kuendelea kupitia idara ya usawi wa

jamii. Chini ya Serikali inayoongozwa na CUF hakutakuwa na makundi ya wazee au watoto wanaopita mitaani kuombaomba.

### 3.1.1.SEKTA MUHIMU ZA UCHUMI - KILIMO

- Historia ya maendeleo ya uchumi duniani inaonesha kuwa maendeleo ya viwanda hutanguliwa au kuambatana na mapinduzi ya kilimo. Ongezeko la uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo huongeza upatikanaji wa chakula na kupunguza gharama yake na kuruhusu wananchi kuhama toka vijijini na kwenda mijini kufanya kazi za viwandani. Kilimo kinazalisha malighafi inayotumiwa na viwanda vinavyosindika nafaka, mbegu za mafuta, matunda, nyama na maziwa. Viwanda vya nguo na bidhaa za ngozi hutumia malighafi inayozalishwa na sekta ya kilimo na ufugaji kama vile pamba na ngozi. Pato la wakulima linapoongezeka linakuza soko la bidhaa za viwandani - nguo na mavazi, viatu, sukari, samani na vifaa vya matumizi ya nyumbani. Soko kubwa la ndani la bidhaa hizi huwezesha kuanzishwa kwa viwanda vyenye uwezo mkubwa na gharama za wastani za chini na kuvifanya viwanda hivyo kuweza kushindana na bidhaa za kutoka nje, na hata kuweza kuuza nje ya nchi. Kuongezeka kwa mapato ya wakulima huongeza uwekaji wa akiba ambayo inaweza kutumiwa kuwekeza katika viwanda. Mauzo ya bidhaa za kilimo nje ya nchi hulipatia taifa fedha za kigeni za kuagizia mashine, vipuri na malighafi kutoka nje ya nchi.

- Utafiti katika nchi nyingi zinazoendelea unaonesha kuwa kasi ya kukua kwa tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo kunapunguza umaskini kwa kasi kubwa kuliko ukuaji wa sekta nyingine yeyote.

**Hali ilivyo sasa**

- Zaidi ya robo tatu ya Watanzania wanategemea sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi katika maisha yao. Wengi wa Watanzania wanaotegemea kilimo ni maskini. Sera ya Furaha na Haki Sawa kwa Wote ina lengo la kuleta mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi ili kuutokomeza umaskini na kuchochea maendeleo ya viwanda.

- Kilimo chetu kimeendelea kuwa duni kwa sababu ya sera mbovu za serikali ya CCM. Tuna ardhi ya kutosha, mito na maziwa makubwa. Jiografia ya Tanzania inafanya nchi yetu iwe na majimbo yenye hali ya hewa tofauti. Mazao mbali mbali ya chakula na biashara yanastawi katika ardhi ya Tanzania. Mahindi, Mtama, Mpunga, Ngano, Jamii ya kunde, Ndizi, Mihogo, Viazi, Karanga, Matunda na Mbogamboga, na hata uyoga vinastawi vizuri katika maeneo mbalimbali. Mazao ya biashara kama kahawa, pamba, chai, katani, korosho, karafuu, tumbaku, alizeti, ufuta, pareto, minazi, chikichi, na hata maua yanastawi. vizuri nchini mwetu. Nchi yetu ina uwezo mkubwa wa kuzalisha mazao ya chakula na biashara kukidhi mahitaji ya ndani na kuuza nchi za nje. Lakini miaka 56 baada ya Muungano, Tanzania haijatumia ardhi yake kutokomeza umaskini kwa sababu ya sera mbaya na uongozi usiokuwa na dira sahihi ya maendeleo. Asilimia 30 ya watoto wana udumavu kwa kukosa lishe bora.

- Hakuna ubunifu wa kuangalia ni mazao gani mapya ya kibiashara yanaweza yakakuzwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Kwa mfano, michikichi inaweza kukuzwa kwa ufanisi katika ukanda wote wa pwani ya Tanzania. Tungeondoka kwenye kasumba kuwa michikichi ni zao la mkoa wa Kigoma sasa nchi ingekuwa inajitosheleza kwa mafuta ya kula na malighafi ya viwandani. Nchi yetu imekuwa tegemezi wa kuagiza mafuta ya kula na yale ya kuendesha magari na mitambo nchi za nje. Mazao ya dizeli na petroli mbadala kama vile miwa, michikichi, nazi na mbono

(jatropha) yanaweza kukuzwa kwa ufanisi katika maeneo mengi ya nchi. Petroli na Diseli mbadala ni bidhaa zenye soko kubwa duniani na hasa Ulaya. Kuna fursa ya kuitumia vyema jiografia nzuri ya nchi yetu kukuza kilimo. Muhogo unaweza kuwa zao la biashara ndani na nje ya nchi na kuchangia katika kupunguza umasikini vijijini.

- Tanzania imekosa sera sahihi ya kukuza kilimo na kuinua hali za maisha ya Watanzania. Zana za kilimo na pembejeo haziwafikii wakulima na hata zinapowafikia huwa zimechelewa na kufika nje ya wakati. Matumizi ya mbolea hayakidhi mahitaji ya kilimo cha kisasa. Masoko ya mazao ya wakulima hayatabiriki. Hata mikopo ya kununulia mazao imekauka na kusababisha kuanguka kwa bei wanayolipwa wakulima.

- Sera za serikali ya CCM kuhusiana na mazao ya chakula hazitabiriki. Wakuu wa Wilaya wanaweza kuzuia uuzaji wa nafaka nje ya wilaya zao wakati wowote wakitaka. Matokeo yake hakuna wafanyabiashara wa nafaka inayozalishwa nchini wenye mtazamo wa muda mrefu, badala yake kuna walanguzi wenye mtazamo wa muda mfupi.
- Pamoja na kudaiwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu, wastani wa bajeti halisi ya kilimo ya kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano haijazidi asilimia mbili ya matumizi yote ya Serikali. Nchi yetu haina huduma bora kwa ajili ya kukuza kilimo cha kisasa na kwa ujumla kumekuwa na udhaifu mkubwa hasa katika maeneo ya uwekezaji kwenye tafiti, motisha kwa wakulima ili wajaribu mazao mapya, ushauri na utaalamu kwa wakulima, mikopo ya zana za kilimo na pembejeo, miundombinu duni na hasa barabara mbovu za kwenda vijijini.

**Dira ya mabadiliko ya CUF**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaasisi mapinduzi ya kilimo ya kweli na kukifanya kiilimo kiwe injini ya maendeleo yetu. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itayafanyia kazi mapendekezo ya muda mrefu ya Tume ya Prof. Shivji ya Ardhi kwa nia ya kuhakikisha kuwa sera bora ya Taifa ya ardhi inapatikana. Sera inayolengwa ni ile ambayo pamoja na mambo mengine inazuia watu kuhodhi maeneo ya ardhi ambayo hawayatumii kwa uzalishaji, inaelekeza utenganisho na mipaka kati ya ardhi inayomilikiwa kitaifa na ile inayomilikiwa na vijiji, na inayoelekeza kwamba Serikali iwe na Mamlaka na ardhi ya Taifa tu. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa umiliki wa ardhi kimila unapewa hadhi sawa na umiliki wa ardhi kwa hati. Mashamba ya wananchi bila kujali kuwa yana mazao ya kudumu ama la yatalipwa fidia inayostahili na inayoendana na thamani ya pesa ya wakati husika, pale Serikali itakapoihitaji ardhi hiyo kwa matumizi mengine.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya itatekeleza azimio la serikali za nchi za SADC ya kutumia alau asilimia 10 ya bajeti ya serikali katika sekta ya kilimo. Maeneo muhimu ya kuwekeza yatakuwa ni pamoja na utafiti wa kilimo, barabara za vijijini na mawasiliano, mfumo wa kilimo cha umwagiliaji maji, usambazaji wa pembejeo, na huduma za fedha za kuweka akiba na kukopa kununulia pembejeo.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kwamba taaluma ya ubwana/ubibi shamba inarejeshewa hadhi yake. Hii ina maana kuwa idadi ya wanafunzi wetu wanaosomea taaluma hii itaongezwa kwa kiasi kikubwa na wahitimu wote wa taaluma hii (wa zamani na wapya) watapewa umuhimu mkubwa. Maafisa ugani watawezeshwa ili waweze kufanya kazi zao katika viwango vinavyotakiwa na vyenye tija kwa wakulima.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaanzisha mfuko rasmi wa kulea na kukuza uzalishaji kwa wakulima (Agricultural Incubator Fund), kwa ajili ya kilimo cha kibiashara. Mfuko huu ambao utakuwa wa kudumu utalenga katika kuwasaidia wakulima nchini kote kuanzisha kilimo cha kibiashara kwa kuwapa uwezo wa kununulia matrekta, vifaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, ujenzi wa maghala, pembejeo na kadhalika.

- Ili kuendeleza kilimo Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaruhusu na kurahisisha biashara ya ndani ya mazao ya kilimo. Serikali itarekebisha mfumo wa kodi na ushuru wa mazao ya kilimo; ikiwa ni pamoja na kufuta ushuru na ada zote za mazao katika ngazi ya mkulima, ili kuongeza motisha kwa wananchi kuwekeza juhudi zaidi katika uzalishaji wa mazao ya kilimo. Vizuizi vyote visivyo na msingi katika biashara ya mazao yote ndani ya nchi vitaondolewa na kuboresha ushindani wa soko la mazao.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itawapa motisha wafanyabiashara wa ndani kuwekeza katika ununuzi wa nafaka toka maeneo yenye ziada na kuuza kwenye maeneo yenye upungufu na kubuni sera zinazotabirika katika biashara ya mazao ya chakula.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itasimamia na kuweka utaratibu mzuri wa usambazaji wa mbegu bora, mbolea na pembejeo. Aidha itatumia fursa iliyoletwa na Teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kuhakikisha kwamba wakulima wanapata mafunzo ya kilimo kwa gharama nafuu, pamoja na kupokea taarifa ya masoko na bei za mazao. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaweka mkakati maalum wa kusambaza na kutumia huduma za TEHAMA kuchochea ukuaji wa kilimo.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itasimamia kuhakikisha kuwa wakulima wote waliokopwa mazao yao na serikali zilizotangulia wanalipwa fedha zao. Wahusika wote waliokopa mazao hayo watasimamiwa na Serikali kulipa madeni yote haraka iwezekanavyo. Atakayeshindwa kufanya hivyo kwa muda uliowekwa atafikishwa mahakamani na kutaifishwa mali zake ziwafidie wakulima.

- Uboreshaji wa miundombinu na njia za mawasiliano utasimamiwa kwa makini na Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF. Pamoja na mambo mengine Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa kila halmashauri inajenga mazingira ya kuanzishwa kwa viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kusindika na kuyaongezea thamani mazao mbalimbali yanayozalishwa na wananchi katika maeneo ya halimashauri husika. Utaratibu huu siyo tu kwamba utawasaidia wazalishaji vijijini kuwa na soko ambalo liko tayari, bali pia utasaidia sana katika suala zima la kuongeza ajira nchini.

- Kwa kushirikiana na taasisi za kimataifa kama FAO, Benki ya Dunia, IFAD na taasisi za utafiti wa kilimo, Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanya utafiti wa kina juu ya mazao mengine ya biashara yanayoweza kustawishwa nchini, na baada ya kuyajua na kutambua maeneo ya nchi yanakoweza kukuzwa, itatoa msaada kwa wakulima wa maeneo husika ili weweze kuyakuza ikiwa ni pamoja na kuwatafutia wabia. Aidha kwa kushirikiana na taasisi hizi, Serikali itaimarisha shughuli za utafiti katika vyuo na taasisi za kilimo nchini ili ziweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika upanuzi na uimarishaji wa shughuli za kulimo.

- Maeneo ya mashamba na ardhi ya vijiji yaliyochukuliwa na viongozi au watu wengine isivyo halali, yatarejeshwa kwa wananchi na Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itasimamia

miradi mikubwa na midogo ya kilimo cha umwagiliaji maji sanjari na ulinzi wa mazingira.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha wakulima na wafugaji wanaishi kwa kwa amani bila mgongano kwa kuwaandalia mfumo mzuri wa mgawanyo wa maeneo ya wafugaji na maeneo ya wakulima sanjari na kuwachukulia hatua za haraka watendaji wote wa serikali wanaoshiriki kufanya hujuma dhidi ya kundi moja kati ya haya kwa maslahi binafsi.

- Tanzania ina fursa ya kukuza sekta ya kilimo kwa wastani wa asilimia 8 kwa mwaka kwa muda wa miaka 10 ijayo, ukilinganisha na ukuaji wa wastani wa asilimia 4 katika miaka 10 iliyopita . Tuna ardhi ya kutosha kukidhi mahitaji yetu ya chakula na kuuza nchi za nje. Sekta ya kilimo inapokua kwa kasi inachochea ukuaji wa sekta nyingine. Upatikanaji wa chakula kwa bei nafuu unapunguza gharama za maisha na gharama za kuajiri wafanyakazi wenye afya njema. Kilimo cha kisasa kinahitaji mbolea, mbegu bora na utaalamu. Gesi iliyonguduliwa inaweza kutumiwa kutengeneza mbolea. Kilimo kinahitaji huduma za usafiri - kusafirisha pembejeo na mazao - hatua ambayo inaongeza ajira. Mazao ya kilimo ni malighafi katika viwanda vya kusindika nafaka, matunda, maziwa na nyama. Viwanda vya nguo na bidhaa za ngozi vinatumia malighafi inayozalishwa na kilimo. Kipato cha wakulima kinapoongezeka wananunua bidhaa za viwandani kama vile nguo, vyombo vya nyumbani, samani, mabati, saruji na vifaa vinginevyo. Mapinduzi ya kilimo yatachochea ukuaji wa sekta ya viwanda na kuongeza ajira katika sekta rasmi.

### 3.1.2.UFUGAJI

Tanzania ni nchi iliyojaaliwa mifugo mingi kama vile ngo'mbe, kondoo mbuzi na kuku. Pamoja na wingi wa mifugo yetu, ukosefu wa huduma

bora na miundo mbinu umeifanya sekta ya ufugaji nchini kushindwa kutoa mchango mkubwa katika kuinua hali ya maisha ya wafugaji walio wengi, pamoja na uchumi wa nchi kwa ujumla.

**Hali ilivyo sasa**

Wafugaji kwa kipindi kirefu wamekosa kupatiwa huduma sahihi na kuandaliwa mazingira bora yatakayowahakikishia wafugaji ubora wa mifugo yao. Viwanda vichache vya kusindika nyama na ngozi vilivyokuwepo miaka michache iliyopita vimeachwa vikafa na kuwakosesha wafugaji soko lenye uhakika zaidi la bidhaa zao. Upatikanaji wa masoko ya nje kwa ajili ya mifugo, au bidhaa zinazotokana na mifugo ni jambo ambalo halijapewa umuhimu unaostahili. Kwa sababu ya ukosefu wa miundo mbinu imara baadhi ya mifugo husafirishwa kwa njia ya kutembezwa maporini kwa muda mrefu na kupelekea kuathiri ubora wa mazao ya mifugo.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

**Kuinua ubora wa mifugo inayozalishwa**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanya sensa ya mifugo kwa nia ya kujua uwiano uliopo kati ya idadi ya mifugo na huduma zilizopo. Hii ni muhimu ili kuweza kupata takwimu sahihi za mahitaji ya madaktari wa mifugo, idadi ya majosho, ukubwa wa maeneo ya malisho, idadi ya manywesheo, mahitaji ya masoko na umbali wa soko na eneo la ufugaji nakadhalika. kufuatia kujulikana kwa takwimu sahihi za mahitaji halisi ya huduma kwa wafugaji, Serikali itaweka utaratibu madhubuti wa kuimarisha na kuboresha usambazaji wa huduma hizo.

**Kupanua shughuli za ufugaji na kuongeza ajira**

Pamoja na wingi wa mifugo iliyopo nchini bado kuna nafasi ya kuipanua sekta hiyo na kuongeza ajira za wananchi wetu. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaanzisha mfuko rasmi wa kulea na kukuza

uzalishaji kwa wafugaji (Livestock Incubator Fund) na wananchi wengine nchini kote wenye nia ya kujiajiri kwenye sekta hiyo kwa ajili ya ufugaji wa kibiashara. Mfuko huu ambao utakuwa wa kudumu utalenga katika kuwasaidia wafugaji kuanzisha ufugaji wa kibiashara kwa kuwapa uwezo wa kununua mitamba bora, uanzishaji wa mashamba ya malisho, uchimbaji wa mabwawa, ujenzi wa mabanda nakadhalika.

**Kuboresha huduma ya masoko**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa kila halmashauri inajenga na kumiliki viwanda vidogo vidogo kwa ajili ya kusindika na kuyaongezea thamani mazao mbalimbali yanayotokana na mifugo katika maeneo ya halmashauri husika. Aidha kwa kushirikiana na wafanyabiashara wa ndani na wawekezaji wa nje Serikali itahimiza ujenzi wa viwanda vya usindikaji wa bidhaa za mifugo kama vile nyama, maziwa, jibini, ngozi, vifungo vya mavazi kutokana na pembe, gundi ya kwato, na mapambo mbalimbali kutokana na mifupa na kadhalika.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itawasaida wafugaji kuanzisha makampuni yao kwa ajili ya uuzaji wa mifugo yao nchi za nje kwa kutoa ushauri wa kitaalamu na misaada mingine itakayohitajika ikiwa ni pamoja na kuwatafutia masoko.

### 3.1.3.UVUVI

Tanzania ina ukanda mrefu wa bahari na vilevile imejaaliwa kuwa ni mshirika katika maziwa makuu matatu yaliyomo kwenye Bara la Afrika. Zaidi ya hayo ina maziwa mengine madogo madogo mengi na mito kadhaa mikubwa. Maji yote haya yana utajiri mkubwa wa samaki na bidhaa nyingine za majini. Bila shaka sekta ya uvuvi pekee ingeliweza kuchangia kiasi kikubwa kabisa katika pato la Taifa na kupunguza kwa kiasi kikubwa kabisa umasikini unaoikabili jamii ya wavuvi nchini.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya uvuvi nchini**

Wavuvi nchini ni mashahidi kwamba sekta ya uvuvi haijapata msukumo wa kutosha ili iondokane na ukale na kujiingiza katika uvuvi wa kisasa wenye tija na uhifadhi wa mazingira. Uharibifu mkubwa wa mazingira kwa kutumia mabomu na sumu na nyavu za uvuvi zisizokidhi viwango ni miongoni mwa matukio yanayoendelea hivi sasa nchini. Siyo tu kwamba mabomu na sumu yanafanya uharibifu mkubwa wa mazingira na kuhatarisha maisha ya walaji wa samaki, lakini ni wazi pia kuwa uvuvi wa namna hii ukiendelea baadha ya miaka michache ijayo hakutakuwa tena na sekta ya uvuvi nchini, na wavuvi waliokuwa wanadhani wanaupiga vita umasikini watajikuta ni masikini maradufu zaidi.

Hapajafanyika juhudi za kutosha za makusudi kuwasaidia wavuvi wetu kuingia katika uvuvi wa kisasa. Hali hii imesababisha Taifa lishindwe kufaidika na utajiri mkubwa wa samaki tulionao katika eneo letu la bahari. Wavuvi wa kizalendo kutokana na kuwa na vyombo duni wamekuwa hawawezi kwenda katika maeneo ya mbali na mwambao yenye kina kikubwa cha bahari wanakopatikana samaki wengi zaidi. Hali hii imesababisha uvuvi katika maeneo haya kuingiliwa na wavuvi wa kigeni ambao wemekuwa wakiendesha shughuli za uvuvi kinyume cha sheria na kuliibia Taifa letu utajiri wa rasilimali hii ya asili.

Pamoja na kuwa na utajiri mkubwa wa samaki, kutokana na uchache wa samaki wanaovuliwa, bei ya samaki katika soko ni ya juu kuliko inavyopaswa kuwa na vilevile wakazi wa kandokando ya rasilimali hizi hawapati samaki wa kutosha kama chakula. Serikali imeacha wafanyabiashara wakubwa kununua kila samaki anayevuliwa na hivyo wenyeji hawawezi bei ghali ya samaki walioko katika ushindani wa bei na badala yake kuambulia kula ‘MAPANKI'.

**Dira yamabadiliko ya CUF katika sekta ya uvuvi**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua zifuatazo ili kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya uvuvi nchini:

• Itaanzisha mfuko rasmi wa kudumu wa mikopo ya masharti nafuu kwa wavuvi na wananchi wengine wenye nia ya kujiajiri kwenye sekta hiyo kwa ajili ya kununulia vifaa vya kisasa vya uvuvi na hifadhi, na kuanzisha ufugaji wa samaki (fish farming).

• Itatoa huduma ya mafunzo kwa wavuvi kwa kiasi kikubwa yatakayolenga katika matumizi ya njia bora za hifadhi ili kuhakikisha kuwa mavuno ya wavuvi hayapotezi ubora wake kabla ya kufikia kwenye soko.

• Itaimarisha shughuli za doria katika maeneo ya uvuvi ili kuhakikisha kuwa wavuvi hawaendelei na utaratibu wa uvuvi unaoharibu mazingira na kuleta maangamizi makubwa kwa samaki na viumbe wengine wa majini, ambao una muelekeo wa kuhatarisha ajira kwenye sekta ya uvuvi.

• Itaweka utaratibu wa kisheria unaohitaji wasindikaji wa mazao ya samaki kununua samaki kiasi maalum cha samaki kila wanaponunua, kutoka kwa wavuvi wadogo wadogo. Utaratibu huu utasaidia uwepo wa mzunguko wa fedha kwa kutoa ajira kwa wananchi wetu.

**Uboreshaji wa soko na upanuzi wa ajira**

- Juhudi zitafanywa kuhakikisha kuwa wawekezaji zaidi wa ndani na nje ya nchi wanafungua viwanda vya kusindikia minofu ya samaki katika maeneno yote yenye mavuno makubwa ya samaki, hususani katika mwambao wa bahari ya Hindi.

- Huduma za ukaguzi na uchunguzi zitaimarishwa ili kuhakikisha kuwa siku zote mavuno yetu ya samaki yanakuwa katika kiwango

cha juu cha ubora ili kujihakikishia mauzo mazuri katika masoko, hususani ya nje.

- Halmashauri za miji na wilaya zilizoko kwenye maeneo ya wavuvi zitahamasishwa kuingia ubia na makampuni binafsi kujenga maghala ya hifadhi baridi (cold Storage Facilities) kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi kuhifadhi mavuno ya ziada kwa kulipa ushuru kidogo.

### 3.1.4.MAENDELEO YA VIWANDA NA AJIRA RASMI

- Maendeleo ya uchumi na jamii ni mchakato wa ukuaji wa kasi wa pato la taifa na mabadiliko ya mfumo wa uchumi kutoka kutegemea kilimo, ufugaji na uvunaji wa mali ya asili, na kuelekea kutegemea viwanda na ugavi wa huduma za kisasa. Nchi masikini zinategemea sana sekta za msingi hususan kilimo, ufugaji na uvuvi. Nchi zilizoendelea zimefanikiwa kubadili mfumo wa uchumi kutoka kutegemea kilimo na kukuza sekta ya viwanda kwa kasi kubwa na kuongeza mchango wake katika pato la taifa. Baada ya ongezeko kubwa la wastani wa pato la taifa mchango wa sekta ya viwanda hupungua na sekta ya huduma za kisasa kuongezeka.

- Maendeleo ya viwanda hutanguliwa au kuambatana na mapinduzi ya kilimo. Ongezeko la uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo huongeza upatikanaji wa chakula na kupunguza gharama yake na kuruhusu wananchi kuhama toka vijijini na kwenda mijini kufanya kazi za viwandani.

Kilimo kinazalisha malighafi inayotumiwa na viwanda vinavyosindika nafaka, mbegu za mafuta, matunda, nyama na maziwa. Viwanda vya nguo na bidhaa za ngozi hutumia malighafi inayozalishwa na sekta ya kilimo na ufugaji kama vile pamba na ngozi. Pato la wakulima linapoongezeka linakuza soko la bidhaa za viwandani - nguo na mavazi, viatu, sukari, samani na vifaa vya matumizi ya nyumbani.

Soko kubwa la ndani la bidhaa hizi huwezesha kuanzishwa kwa viwanda vyenye uwezo mkubwa na gharama za chini na kuvifanya viwanda hivyo kuweza kushindana na bidhaa za kutoka nje na hata kuweza kuuza nje ya nchi. Kuongezeka kwa mapato ya wakulima huongeza uwekaji wa akiba ambayo inaweza kutumiwa kuwekeza katika viwanda. Mauzo ya bidhaa za kilimo nje ya nchi hulipatia taifa fedha za kigeni za kuagizia mashine, vipuri na malighafi kutoka nje ya nchi.

- Ukuaji wa uchumi unaambatana na Mabadiliko ya mfumo wa uchumi kutoka kutegemea sana kilimo na kuelekea kwenye ongezeko la ajira viwandani, kutoka nguvu kazi inayoishi vijijini kuelekea nguvu kazi inayoishi mijini. Mabadiliko ya mfumo wa uchumi husababishwa na ushindani wa soko.

Serikali zenye malengo ya kukuza uchumi endelevu zinawajibika kujenga ushindani katika masoko yote kuruhusu makampuni mapya yenye tija kuanza na makampuni yanayopata hasara kufilisika. Soko la Ajira linahitaji kuwa jepesi kuruhusu makampuni mapya kuajiri wafanyakazi na makampuni yanayopata hasara kupunguza wafanyakazi. Sheria za kazi zinatakiwa zijikite katika kurahisisha uanzishwaji wa ajira. Ni muhimu sana kuwa na utaratibu wa hifadhi za jamii kwa wafanyakazi wanaopoteza ajira ili kuwapunguzia makali wakati wakitafuta ajira mpya na kuruhusu kuwepo kwa soko la ajira linalonyumbulika.

- Ili kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi, ni muhimu kutumia mfumo wa soko katika ugawaji na matumizi ya raslimali, nguvukazi, malighafi na bidhaa nyingine. Maendeleo ya uchumi kwa ujumla na hususan maendeleo ya viwanda ni mchakato unaobadilika na unahitaji kila wakati kuboresha teknolojia na menejimenti.

Utaratibu wa kutumia mfumo wa soko ni muhimu lakini peke yake hauwezi kukuza uchumi na uzalishaji viwandani na kuleta mabadiliko

ya mfumo wa uchumi yanayohitajika ili kuongeza pato la wastani la mwananchi wa kawaida. Serikali ina wajibu muhimu wa kuweka mazingira mazuri ya kujenga miundombinu kama vile barabara, reli, bandari, mawasiliano, ugavi wa maji na ufuaji na usambazaji wa umeme.

- Vile vile serikali inawajibika kuendeleza elimu bora kwa wote na kusisitiza elimu ya sayansi, ufundi na teknolojia ipewe nafasi maalum katika mfumo mzima wa elimu. Ili kuwa na nguvu kazi yenye tija, huduma za msingi za afya kwa wananchi wote ni jambo la msingi. Pia serikali ina wajibu wa kuratibu na kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji hasa katika sekta zinazohitaji kuwepo kwa miundombinu na huduma nyingine za kiuchumi.

- Kwa kawaida kampuni yoyote ili iweze kusonga mbele na kupata mafanikio, ni sharti safu yake ya uongozi ijazwe na watu wenye ujuzi wa hali ya juu, uzoefu wa kutosha na shauku ya kuleta mafaniko. Kwa kuwa watu hawa ni wataalamu wanapaswa kuwa na uhuru wa kutosha kufanya maamuzi bila kungoja ridhaa ya wanasiasa. Aidha mafanikio ya kukuza uchumi na biashara yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na ubora wa miundombinu inayohitajika, kama vile barabara, reli, bandari, mawasilinao, nishati, maji na huduma za fedha.

Miaka 56 ya Tanzania tumeshuhudia kudidimia kwa kasi kwa sekta ya viwanda na mashirika/makampuni ya huduma. Viwanda na mashirika/makampuni mengine yamekufa sio kwa sababu nyingine yoyote zaidi ya kuwa na uongozi mbaya wa mfululizo ulioteuliwa toka Ikulu na udhaifu wa miundo mbinu iliyohitajika.

- Kuongezeka kwa ajira rasmi ni kigezo muhimu cha uchumi unaokua na kupungua umasikini. Hii ni kutokana na ukweli kwamba shughuli nyingine zote za kujiajiri zinategemea matumizi

ya vipato vya wale wenye ajira rasmi. Mkulima, Seremala, Fundi cherehani, Kinyozi, Muuza duka na kadhalika, wote wanategemea mzunguko wa fedha ambao chanzo chake ni yule mwenye ajira rasmi. Mathalani, kikijengwa kiwanda mahali kinachoajiri wafanyakazi 1000 ambao kwa wastani kila mmoja wao analipwa shilingi 500,000/= kwa mwezi, kila mwisho wa mwezi kutakuwa na jumla ya shilingi milioni 500 kwenye mikono ya wafanyakazi hao ambazo ziko tayari kutumiwa. Fedha hizi zikiingia kwenye matumizi zitakuwa ni kichocheo kikubwa kwa sguhuli mbalimbali za kiuchumi zinazopakana na kiwanda hicho.

- Wakati analizindua Bunge la 11, Rais Magufuli alieleza lengo lake ni kukuza sekta ya viwanda iweze kuajiri asilimia 40 ya nguvukazi mwaka 2020. Ni wazi lengo hili halitekelezeki ukizingatia kuwa ajira ya kudumu na ya muda viwandani mwaka 2015 ilikuwa watu 183,994, ambayo ni chini ya asilimia 1 ya nguvu kazi yote.

**Hali ilivyo hivi sasa**

- Maendeleo ya viwanda ni madogo sana nchini. Ukuaji wa sekta ya viwanda umepungua toka asilimia 10.8 mwaka 2015 na kufikia asilimia 5.8 mwaka 2019. Ajira viwandani ni ndogo sana. Katika nchi yenye nguvu kazi ya watu milioni 30, ni Watanzania 243,220 tu ndiyo wameajiriwa katika sekta ya viwanda.

- Katika miaka 30 iliyopita China imefanikiwa kuwa karakana ya dunia na kuzalisha bidhaa za viwandani zinazouzwa katika soko la dunia. Gharama za uzalishaji wa bidhaa za viwandani zimeongezeka sana China. Mishahara imepanda, bei ya ardhi imeongezeka sana, thamani ya fedha ya China inapanda, uchafuzi wa mazingira unao sababishwa na kuwepo viwanda vingi umeongezeka. Sera ya ya China hivi sasa ni kuongeza utumiaji wa bidhaa ndani ya nchi na kupunguza kutegemea kuuza bidhaa nje ya nchi. Inakadiriwa kuna ajira za watu milioni 85 zitahama toka

China kwenda nchi nyingine katika kipindi cha miaka 10 ijayo. Tanzania ina fursa ya kupata baadhi ya ajira zitakazohama toka China ikiwa tutajipanga vizuri.

- Pamoja na kauli mbiu ya kujenga Tanzania ya Viwanda, mazingira ya uwekezaji na biashara hayavutii. Hivi sasa siyo rahisi kupata leseni na ardhi ya kujengea viwanda.

**Dira ya mabadikoko ya CUF**

- Nchi yetu ina bahati ya mali ya asili nyingi. Ina pwani na bandari na imezungukwa na nchi ambazo hazina bandari. Kwa kuwa tuna bandari gharama za kushiriki katika biashara zaweza kuwa ndogo. Tuna vianzio vya kufua umeme wa maji takriban MW 5000 ambapo hivi sasa tunatumia MW 560 tu. Tuna gesi inayoweza kutumiwa kufua umeme na ni malighafi ya viwanda vya mbolea na kemikali. Tuna makaa ya mawe yanayoweza kutumiwa kufua umeme. Tuna madini ya chuma, nickel, shaba, uranium na mengine mengi. Tuna misitu na ardhi inayoweza kuoteshwa miti ya mbao inayoweza kukua kwa haraka.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itazindua sera mpya za kitaifa kusimamia viwanda na mashirika ya huduma kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya kuvutia kwa wawekezaji wa ndani na nje. Sera hizi zitalenga kuimarisha na kuboresha miundo mbinu katika nyanja za usafiri, mawasiliano, maji na nishati; kuweka mfumo wa kodi unaoeleweka na kutabirika ambao haubagui kati ya wawekezaji wakubwa na wadogo; kuandaa nguvu kazi inayohitajika; na kuandaa mazingira ya kuwawezesha watanzania wengi zaidi kujiingiza katika umiliki wa shughuli za uzalishaji, biashara na utoaji wa huduma.

Aidha sera za kusimamia viwanda na mashirika ya huduma zitalenga kuweka mazingira ya kujenga ushawishi kwa wawekezaji wa nje kuingia ubia na Watanzania kwa motisha maalum. Sera hizi zitaandaa pia mazingira ya kuwachochea wazalishaji wa ndani ya nchi kuimarisha viwango vya ubora wa bidhaa zao ili ziwe na ushindani kwenye masoko. Aidha Serikali itaandaa mazingira yatakayoleta unafuu wa kuridhisha katika gharama za uzalishaji.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaweka mkakati madhubuti na kujenga mazingira ya kuanzisha na kuendeleza viwanda vyepesi vya kusindika mazao ya kilimo, nguo na mavazi, viatu na bidhaa za ngozi, samani, vifaa vya matumizi ya nyumbani na vifaa vya umeme na elektroniki vyenye uwezo wa kuajiri vijana wengi. Vile vile viwanda vinavyotumia malighafi inayopatikana nchini kama vile viwanda vya mbolea na kemikali vitaanzishwa.

- Maendeleo ya viwanda yenye tija na ufanisi ni kitu kinachohitaji mtaji mkubwa. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaimarisha Benki ya Maendeleo ya Tanzania - Tanzania Investment Bank - kwa kuiongezea mtaji na kuboresha utendaji wake ili kuongeza uwezo wake wa kuwasaidia wawekezaji makini katika sekta ya viwanda.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaanzisha maeneo maalum ya uchumi karibu na bandari za Bagamoyo, Mtwara na Tanga ambayo yatashehenezwa huduma za uhakika za umeme, maji, mawasiliano na usafiri wa rahisi kwenda bandarini. Aidha, wafanyabiashara wazalendo wenye viwanda ambao wameonyesha uwezo wa kuendesha viwanda na kuhimili ushindani watahamasishwa kutoa mawazo yao kuhusu mikakati ya kukuza viwanda nchini.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF pia itaanzisha kanda maalum za uchumi katika mikoa ya Mwanza, Kigoma, Katavi, Rukwa na Mbeya ambazo zitalenga masoko ya ndani ya nchi ya nchi, hususan katika mikoa ya kanda ya maziwa makuu ya nyanza, Tanganyika na Nyasa na masoko ya nchi za maziwa makuu za Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya watu wa Congo, Zambia na Malawi.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaboresha elimu ya sayansi, ufundi na teknolojia ili kuandaa nguvukazi yemye uwezo wa kuajiriwa viwandani.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa shirika la umeme na mamlaka za maji zinapewa kipaumble maalumu na na kuimarishwa ili zitoe huduma bora na za uhakika.

- Chimbuko kubwa la umeme kukatika hovyo ni kwamba mfumo wa kupokea na kusambaza umeme nchini yaani GRID YA TAIFA, umeoza. Serikali ya CCM inafumbia macho suala hili japo ni jambo linalosababisha hasara kubwa kwa watumiaji wa umeme. Katika sekta ya umeme moja ya vipaumbele vya Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itakuwa ni kufufua GRID YA TAIFA. Tunahitaji umeme ukatike kwa dharura kubwa na siyo kwa sababu mfumo umeoza.

**Upanuzi wa ajira na kutofautisha maeneo ya kuwekeza**

- Ili kuwasaidia wananchi wetu mbalimbali na hususani vijana wetu wanaohitimu katika vyuo vya elimu ya juu na wananchi waliopunguzwa makazini - walio wabunifu na wenye mawazo mapya - kujiingiza katika shughuli za kujiajiri kupitia biashara na uzalishaji, Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaanzisha

mifuko rasmi ya kulea na kukuza biashara na uzalishaji viwandani (Trade and Manufacturing Incubator and Accelerator Funds). Kupitia uwezeshaji utakaofanywa na mifuko hii, hofu ya wahitimu wa vyuo kukosa ajira itabaki kuwa ni historia na wale wenye biashara tayari ambazo zinashindwa kukua kutokana na mtaji mdogo wataweza kupata mitaji ya kukuza biashara zao.

- Katika kila mkoa Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itatenga maeneo ya ardhi ambayo yatapimwa mahususi kwa ajili ya uwekezaji wa kistrategia. Wawekezaji wakubwa wa ndani na nje wanaotaka kujenga viwanda vya kisasa na kuwekeza kwenye huduma za kisasa, mathalani hospitali za kisasa, hasa kwa ajili ya masoko ya nje .

### 3.1.5.SEKTA ISIYO RASMI

**Hali ilivyo sasa**

- Hakuna mazingira muafaka ya kiutendaji kwa sekta isiyo rasmi.
- Hakuna usalama wa mali ya wafanyabiashara katika sekta hii.
- Sekta isiyo rasmi inaumizwa na mzigo mzito wa kodi isiyolipika.
- Serikali ya CCM bado haijaonesha kutambua na kuthamini sekta hii ipasavyo.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanya uwekezaji endelevu ili kurasmisha shughuli za wale ambao hivi sasa zinafanyika chini ya mwavuli wa sekta isiyo rasmi. Hii itawajengea mazingira rafiki ya ukuaji wa shughuli zao na pia itaisaidia serikali kuweka takwimu sahihi ya shughuli za kiuchumi zilizopo na

katika kukusanya kodi. Aidha kwa kuwa shughuli nyingi za sekta isiyo rasmi hufanywa katika mazingira ambayo siyo sahihi - mathalani kwenye njia za waenda kwa miguu pembezoni mwa barabara , urasmishaji utaondoa shughuli hizo katika mazingira ya aina hiyo na hivyo kuleta nafuu kwa wadau wanaokwazika.

### 3.1.6.MISITU

**Misitu na mapori ya asili**

- Misitu ni chanzo muhimu cha ajira na pato la wananchi wengi. Sekta ya mbao na samani inategemea misitu moja kwa moja. Watanzania wengi wanategemea misitu kupata nishati ya kupikia. Ujenzi wa nyumba vijini unategemea misitu. Misitu ni muhimu kwa kilimo. Mimea inategemea mchavusho wa wadudu wanoishi misituni ili kuzalisha vyakula. Nyuki wa asali wanategemea uwepo wa misitu. Mvua inategemea uwepo wa misitu. Uwepo wa misitu unazuia mmonyoko wa udongo na kuhifadhi rutuba ya ardhi. Mito haikauki kwa kuwepo misitu. Kuwepo kwa misitu katika vyanzo vya maji kunazuiwa mchanga kuongezeka kwenye mabwawa ya kufua umeme. Mikoko inazuia mafuriko ya bahari. Misitu inazamisha hewa ukaa na kusaidia katika kupunguza kasi ya ongezeko la joto duniani. Dawa za asili za mitishamba zinatoka misituni.

- Tanzania imejaaliwa misitu na mapori mengi ya asili yenye mchanganyiko mkubwa wa mimea. Pamoja na kwamba mimea hii imekuwa ikichangia uchumi wetu kwa kiasi fulani, bado mkazo wa kutosha haujawekwa kuhakikisha kwamba faida yote iliyomo kwenye mimea hii inapatikana. Uvunaji wa Gum Arabica ambao ni utomvu mgumu utumikao kuimarisha vinywaji vya aina mbalimbali bado hautiliwi mkazo, pamoja na kwamba kuna soko kubwa la bidhaa hii duniani, na bidhaa yenyewe inapatikana kwa

wingi nchini hasa katika mkoa ya Dodoma, Singida, Tabora na Shinyanga.

- Uharibifu na ukataji wa misitu holela unahatarisha kilimo na usalama wa chakula, unakausha mito, unaongeza mmonyoko wa udongo, unaongeza joto na unahatarisha usalama wa viumbe wengine.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya Misitu**

- Juhudi za dhati hazijachukuliwa kuhakikisha kuwa uvunaji endelevu wa mali asili iliyoko katika misitu na mapori ya asili yaliyoko nchini unatumika kunyanyua Pato la Taifa.

- Serikali kwa kiasi kikubwa imezitelekeza taasisi zetu zinazoshughulika na tafiti zinazohusu mimea asilia hususan katika tafiti za madawa. Matokeo yake ni kwamba taasisi zinafanya kazi kikamilifu tu pale zinapopata wafadhili wa nje ambao huja kuhodhi matokeo na manufaa yanayotokana na tafiti hizo.

- Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika maeneo yote yanayozunguka hifadhi za Taifa. Wanavijiji wamekuwa hawana haki ya kulinda mazao yao dhidi ya wanyama waharibifu, na pale wanapochukua hatua dhidi ya uharibifu wowote wamekuwa wakinyanyaswa, kupigwa, kuuliwa na hata kufunguliwa kesi za kubambikiziwa na askari wa wanyama pori.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

Ili kuhakikisha kuwa Taifa linanufaika kikamilifu kutokana na misitu na mapori yake, serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua zifuatazo:-

- Itaanzisha programu mahsusi ya kufanya tathmini ya mimea asilia inayopatikana nchini. Tathimini hii itafanyika kwa lengo la kujua aina, wingi, mahali inapopatikana na matumizi yake ya kijadi. Tathmini hii itafanywa kwa ushirikiano wa jopo la vyuo vikuu vya serikali nchini chini ya idara husika katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Aidha kupitia programu hii vitengo vya matumizi ya miti asilia katika taasisi ya madawa asilia ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba, na Idara ya Kemia ya Chuo Kikuu cha Dr es salaam vitaimarishwa.

- Itaanzisha benki maalumu ya kuhifadhi viasili (Gene Bank) pamoja na kila aina ya mmea unaopatikana nchini kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa na idara zinazohusika katika vyuo vya serikali. Benki hii itakuwa ni kinga maridhawa endapo janga lolote litatokea na kusababisha aina yoyote ile ya mmea kutoweka.

- Itaandaa na kutekeleza sera kitaifa kuhusu uvunaji endelevu wa mimea asilia. Sera hii itasaidia sana katika kuweka taratibu za wazi na zinazotabirika za kusimamia uvunaji na biashara ya mimea asilia, husasani kwa ajili ya masoko ya nje.

- Itahakikisha kuwa wananchi wanalipwa fidia kwa mali na mazao yao yanayoharibiwa na wanyamapori wanaotoroka kutoka katika hifadhi za Taifa. Aidha elimu ya uraia itatolewa kwa watendaji wote wa Hifadhi za Taifa ili weweze kuzingatia haki za binadamu.

- Itawashirikisha wananchi wanaoishi karibu na hifadhi ya misitu kuilinda misitu hiyo kwa kupata ajira na manufaa mengine ya ulinzi wa misitu. Serikali itajiunga na mpango wa jumuiya ya kimataifa kulinda misitu na kulipwa fedha kwa kuwa misitu inapunguza hewa ukaa.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahamasisha upandaji wa miti kwenye maeneo yasiyokuwa na miti asilia

### 3.1.7.MADINI

Nchi yetu ina utajiri mkubwa wa madini ya aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na dhahabu, Almasi, Tanzanite, Bati, Chuma, Uranium, Phosphorus, Makaa ya mawe, Vito, Nickel, Chokaa, Jaribosi, Chumvi Mfinyanzi, Gesi, Mafuta na kadhalika.

Nchi kama Ghana, Afrika kusini, Botswana na nyingiezo zimetumia mapato toka sekta ya madini kujenga miundombinu na kukuza uchumi wa nchi zao kikamilifu. CUF inathamini na kutambua umuhimu mkubwa wa kuendeleza mahusiano mema kati ya serikali na wachimbaji wa ndani na nje ya nchi kwa kukaribisha uwekezaji mkubwa na wa kiteknolojia za kisasa katika sekta ya madini.

Kwa muda mrefu Chama cha CUF kimeeleza kuwa Tanzania inatapeliwa katika sekta ya madini. Serikali inalipwa asilimia tatu tu ya thamani ya madini yanayochimbwa Tanzania. Tunafarijika kuwa serikali ya awamu ya tano imechukua baadhi ya sera za CUF na kujaribu kuzitekeleza katika suala hili.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya Madini**

- Wachimbaji wadogo wadogo wa madini wamekuwa na wakati mgumu kutokana na maeneo yao ama kuchukuliwa na wachimbaji wakubwa, au kutokana na ukosefu wa mitaji ya kutosha, zana za kisasa, na masoko bora ya bidhaa zao.

- kumekuwepo na malalamiko ya muda mrefu juu ya wananchi wanazozunguka maeneo ya uchimbaji kwamba wamekuwa hawanufaiki na rasilimali ya madini yaliyopo katika maeneo yao na badala yake kumekuwa na athari kubwa za kimazingira na kwa afya za wananchi kutokana na kemikali zinazotumika katika migodi kumwagwa bila kutibiwa na kuingia kwenye ardhi na vyanzo vya maji. Mfano mzuri ni athari zilizopatikana katika mgodi wa dhahabu wa North Mara miaka kadhaa iliyopita.

- Serikali ya awamu ya tano imejitahidi kurekebisha Sheria ya madini na mikataba isiyo na manufaa ya kuridhisha kwa Taifa. Hata hivyo zinahitaji kuambatana na sera zinazotabirika kwa wawekezaji wa ndani na nje. Aidha, tofauti na sasa, kuna umuhimu wa kuwa na mfumo wa kitaalam wa udhibiti na ukaguzi wa madini yanayovunwa usioendeshwa kisiasa.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF katika sekta ya Madini**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa utajiri mkubwa wa madini unatumika kikamilifu kuinua uchumi wa nchi yetu na hivyo kuboresha hali ya maisha ya wananchi. Serikali itazindua Sera Mpya ya Uwekezaji katika sekta ya madini, kwa lengo mahususi la kulinda maslahi ya wananchi, wachimbaji wadogo wadogo na wawekezaji kwa ujumla. Pamoja na mambo mengine sera hii italenga kuchukuliwa kwa hatua zifuatazo:

- Kupitiwa kwa taarifa za Tume zote zilizowahi kuundwa ikiwemo Tume ya Jaji Mstaafu Paul Bomani na nyingine, na kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na tume hizo na kuyafanyia kazi maeneo ambayo bado hayajashughulikiwa kikamilifu na serikali zilizotangulia.

- Kuanzishwa kwa mjadala wa kina kati ya Serikali na wawekezaji wote wa ndani na nje ya nchi ili kufikia maridhiano muafaka juu ya namna bora ya kulinda maslahi ya pande zote mbili.

- Kufanyika kwa marekebisho ya utozaji wa mrahaba na kodi kwenye madini. Marekebisho husika ni lazima yalenge kwamba mapato ya serikali yawe ni asilimia thelathini (30) ya thamani ya mauzo ya madini. Tukifikia hapa tutakuwa na uwiano wa mapato ya migodi yetu na ile ya Kusini na Magharibi mwa Afrika.

- Kuimarisha udhibiti na ukaguzi wa mavuno ya madini ili kuondoa udanganyifu wa kiasi cha madini kinachovunwa.

- Kurekebisha mfumo wa misamaha ya kodi na uagizaji wa bidhaa mbalimbali kutoka nje ya nchi ili kuweka urari sawia wa kukuza sekta ya biashara nchini.

- Kushirikiana na wawekezaji wa ndani na nje katika kuhakikisha kuwa makampuni yote yanaweka na kutoa taarifa sahihi za mitaji yao na kuepuka kufanya udanganyifu wa kuongoeza thamani ya mitaji yao (over invoicing of capital expenditure) kwa madhumuni ya kukwepa kodi.

- Kuhakikisha kuwa migodi yote mipya inasamehewa ushuru wa forodha kwa asilimia 100 kuhusiana na mitambo itakayoingizwa kabla ya kuanza uzalishaji, na baada ya kuanza uzalishaji itapata msamaha wa kodi ya mapato wa asilimia 100 katika miaka miwili ya kwanza. Baada ya kipindi hicho kila mgodi utalazimika kulipa kodi kamili kwa mujibu wa viwango vitakavyowekwa.

- Kuhakikisha kuwa huduma muhimu ikiwa ni pamoja na masoko mazuri zinawafikia wachimbaji wadogo. Kufanikisha hili serikali itawasaidia wachimbaji wadogo wadogo wajisajili kama kampni na

kwamba kampuni inayohusika ndio itakayomilikishwa mgodi unaohusika.

- Kuhakikisha kuwa vitalu ambavyo vimetelekezwa kwa muda mrefu bila kuendelezwa vinashughulikiwa kwa mujibu wa sheria husika.
- Kusimamia uanzishwaji wa viwanda vya koboresha madini husika kabla ya kuuzwa nje (polishing industries) ili kuyaongezea thamani na kuanzisha ajira rasmi mpya kwa watanzania.
- Kuhakikisha kuwa maeneo yaliyo na utajiri wa madini yanapewa kipaumbele cha kipekee ili maendeleo yake yaendane na hadhi na ulinganifu wa utoaji wa mchango mkubwa wa utajiri huo kwa Taifa.
- Kuhakikisha kuwa wananchi wengi zaidi wanajishughulisha na shughuli za uzalishaji wa madini ya chumvi na mfinyanzi ambayo yanapatikana nchini kwa wingi na hayana tatizo la soko. Madini ya chumvi yana soko kubwa katika nchi za jirani. Mfinyanzi ni madini yenye soko kubwa katika viwanda vya petrol sehemu mbalimbali duniani.
- Kufanikisha uwekezaji wa kuchimba gesi katika bahari kuu unaotarajiwa kufanywa na kampuni ya Statoil ya Norway.
- Kfanikisha kuanzishwa kwa viwanda vya mbolea vinavyotumia gesi kama malighafi.
- Kuhakikisha kuwa mradi wa kusambaza gesi kwa mabomba kwa matumizi ya majumbani na viwandani utakamilishwa haraka iwezekanavyo.

### 3.1.8.UTALII

Ziko nchi nyingi duniani ambazo zinategemea kwa kiasi kikubwa biashara ya utalii kuweza kufidia gharama za mahitaji ya wananchi wake. Nchi hizi zimefanikiwa kwa sababu zimewekeza kwa dhati kwenye sekta hii, pamoja na kwamba baadhi yake hazina vivutio vingi vya watalii. Bahari ya Hindi, Visiwa vya Zanzibar na Mafia, Delta ya mto Rufiji, Mbuga za wanyama za Serengeti, Ngorongoro, Lake Manyara, Mikumi na Selous, milima Kilimanjaro na Meru na ukarimu wa wananchi wetu na tamaduni zao, unaifanya Tanzania kuwa nchi ya pekee kwa mapumziko murua kwa wageni watokao nchi za Ulaya, Marekeni na Asia. Ni dhahiri kwamba Tanzania ni moja ya nchi za dunia zinazofaa kutembelewa na anayehitaji mapumziko murua ya uhakika. Hata hivyo hatujautumia urithi huu kikamilifu kuinua hali ya maisha ya Watanzania tuliopo sasa na wale wa vizazi vijavyo.

Maradhi ya maambukizi ya virusi vya Corona (COVID-19) yameathri sana biashara ya utalii duniani kote. Nchi nyingi zinazoleta Watalii Tanzania zilizuia wananchi wao wasisafiri ili kujikinga na Corona. Safari za ndege zilizuiwa. Kuna wasiwasi kuwa COVID-19 inaweza kuathiri usafiri wa ndege wa kimataifa na biashara ya utalii kwa muda mrefu.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya utalii**

Hakuna uwekezaji wa kutosha wa miundo mbinu inayohitajika kwa huduma ya utalii. Serikali kwa muda mrefu imejikita katika kuangalia utalii wa asili, yaani ule wa kuja kuangalia mbuga za wanyama au kupanda mlima Kilimanjaro, na kusahau kuendeleza maeneo ya utalii ya aina nyingine. Juhudi za kuhamasisha utalii wa ndani zimekuwa zikifanyika kwa msimu na hazijitoshelezi inavyotakiwa.

Katika harakati za kuzuia maambukizi ya Corona, Tanzania haitangazwi vizuri katika Jumuiya ya Kimataifa. Wananchi na wakaazi wengine wa nchi yetu hawapimwi kubaini jamii imeathiriwa kwa kiasi gani. Kibaya

zaidi serikali imesitisha kutangaza maambukizi ya Corona tangu tarehe 29 Aprili 2020. Tovuti ya Kituo cha Kudhibiti Magonjwa barani Afrika (Africa CDC) inaonyesha kuwa mpaka tarehe 21 Mei, Tanzania imepima vipimo vya Corona 652 tu na kubaini wagonjwa 509 wakati Kenya imepima vipimo 52,507 na kubaini maambukizi 1,109. Uganda imepima vipimo 77,072 na kubaini maambukizi 274 na Rwanda wamepima watu 53,317 na kubaini maambukizi 314. Pamoja na kutokuwepo taarifa za vipimo, Tanzania imetangaza kuwa maambukizi ya Corona yamepungua sana. Hali hii inaweza kuwapa wasiwasi watalii wa nje kuwa Tanzania siyo salama kwa maambukizi ya Corona.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

**Kuimarisha Upimaji wa Corona Nchini na hasa kwenye vituo vya Utalii**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itajiunga na Jumuiya ya Kimataifa kupima maambukizi Corona na kutoa taarifa ya kiasi cha maambukizi kilichoko kwenye jamii. Wataalam wa taasisi za Wizara ya Afya watafanya vipimo kwa kutumia sampuli zilizochukuliwa bila utaratibu maalum (random sample) ya watu 5,000 mpaka 10,000 kujua hali halisi ya corona jijini Dar es Salaam, Arusha na Zanzibar. Utafiti huu utafanywa kitaalamu na kwa uwazi na matokeo yake yatatangazwa.
- Vituo vya Kitalii ikiwa pamoja na hoteli na mbuga za wanyama vitaweka taratibu maalum za kuzuia maambukizi ya Corona na kuzitangaza kwenye mitandao ya kijamii.

- Utafiti wa Africa CDC unaoonyesha kuwa Tanzania haiwezi kuwa na maambukizi makubwa ya Corona utatangazwa katika mitandao ya kijamii.

**Kuimarisha huduma za utalii**

- Serikali itaimarisha mawasiliano ya aina zote katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ambayo kwa hivi sasa yako kwenye ukanda wa utalii.

- Serikali itatafuta wawekezaji zaidi kuwekeza katika huduma za watalii kama vile hoteli, usafirishaji, uandaaji wa ziara na kadhalika

- Serilaki itatumia mbinu za kisasa kuhifadhi mazingira na kuzuia ujangili katika hifadhi za Taifa. Mbinu hizo ni pamoja na matumizi ya picha za satellite na matumizi ya ndege za drone kupata picha halisi ya kile kinachotokea kila siku katika mbuga za wanyama na maeneo mengine ya utalii.

**Kupanua wigo shughuli za utalii**

Hivi sasa shuguhuli za kitalii nchini zimeelemea sana kwenye utalii wa kiasili. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF pamoja na kuchukua hatua za kuimarisha utalii wa kiasili, pia itasimamia kwa karibu uanzishwaji na utunzwaji wa utalii wa kimazingira na kiutamaduni (eco - tourism & cultural tourism). Utalii wa aina hii utawavutia wageni wengi wenye nia ya kujua Watanzania wanavyoishi na mazingira yao, hususani wanafunzi na watafiti. Aidha Serikali itafanya juhudi kubwa kuhamasisha na kutoa vichocheo kwa watalii wa ndani. Matarajio ni kuongeza pato linalotokana na utalii kwa mwaka na kufikia mara mbili au zaidi ya ilivyo sasa, katika miaka 5 ijayo.

**Kukuza na kupanua soko la utalii**

Pamoja na kuimarisha miundo mbinu ya kitalii na kupanua vivutio vya utalii, Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanya juhudi kubwa kuitangaza biashara yetu ya utalii nchi za nje, ikiwa ni pamoja na

kuanzisha kituo kikubwa cha utalii kwenye mtandao wa internet ambacho kitakuwa na habari zote za utalii nchini na ambazo zitaboreshwa mara kwa mara ili wageni wenye nia ya kuizuru nchi yetu wawe na taarifa kamili ya nchi yetu na sekta ya utalii nchini.

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF italinda mazingira ya hifadhi za Taifa kwa kuwashirikisha wananchi wanaoishi kando kando ya hifadhi, ili pia wanufaike na mapato ya hifadhi hizo. Serikali itatengeneza utaratibu ambao utahakikisha kwamba kila kijiji au kata ambayo eneo lake lina kivutio chochote cha utalii inapewa sehemu ya mapato yanayotokana na utalii kwa nia ya kujengea miundo mbinu ya maendeleo ya eneo husika. Hii itawafanya wenyeji wa maeneo husika wanufaike moja kwa moja na maeneo waliyoyatunza kwa karne kadhaa.

**Huduma kwa wafanyakazi wa idara ya wanyamapori**

Huduna hizi zitaimarishwa kwa kiasi kikubwa kwa kuboresha maslahi zaidi na kuwapatia vitendea kazi. Kuimarishwa kwa huduma kutakuwa ni motisha kwa wafanyakazi hawa kutoa huduma bora na ya uhakika zaidi siyo kwa wanyama pori tu, bali pia na kwa watalii wanaouzuru maeneo yao.

**Kusimamia maeneo ya uwindaji**

Serikali itachunguza tuhuma mbalimbali zinazoelekezwa katika maeneo haya na kuchukua hatua muafaka kurekebisha matatizo yaliyopo.

### 3.1.9. SEKTA YA FEDHA NA HUDUMA ZA KIBIASHARA

Sekta ya Fedha inayojumlisha Benki Kuu, Benki za biashara, Benki za maendeleo ya kisekta, Masoko ya mitaji, Makampuni ya bima, nakadhalika ni muhimu katika kukuza uchumi wa kisasa. Kazi kuu ya sekta ya fedha ni kukusanya akiba toka kwa wananchi, kampuni na taasisi mbalimbali na kuwakopesha wawekezaji, wafanyabiashara na wananchi wengine wenye miradi na mahitaji mbalmbali.

Asasi za fedha ndizo ubongo wa uchumi. Zinaamua kampuni, miradi na watu gani wanaokopesheka. Benki zinahudumia sekta ya biashara na kurahisisha mfumo wa malipo na utunzaji wa akiba. Kigezo kimojawapo muhimu cha uchumi imara katika nchi yoyote ni umadhubuti wa mtandao wa kibenki uliopo.

Benki Kuu ndiyo msimamizi wa ujumla wa sekta ya fedha. Kwa nchi masikini kama Tanzania, Benki Kuu ina majukumu asilia ambayo ni:

1)Kutoa sarafu,

2) Ni Benki ya benki za biashara,

3) Ni Benki ya Serikali,

4) Kusimamia ugavi wa fedha na mkopeshaji wa mwisho wa benki za biashara na asasi nyingine za fedha (Lender of last resort).

5) Kwa nchi zinazoendelea jukumu la tano ni kuweka akiba ya fedha za kigeni na kusimamia thamani ya sarafu.

6) Jukumu la sita ni kujenga mfumo na taasisi za benki na kufanya maamuzi juu fedha zitakazochochea maendeleo ya uchumi.

Utekelezaji wa Azimio la Arusha ulitaifisha benki za biashara zote na kuanzisha Benki ya Taifa ya Biashara - NBC. Kampuni zote za bima zilitaifishwa na kuwekwa chini ya shirika la bima la Taifa - NIC. Pia serikali ilianzisha Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini - CRDB na Benki ya Uwekezaji - TIB.

Kuporomoka kwa uchumi miaka ya 1980 kulilazimisha marekebisho ya sera za uchumi. Mabadiliko ya sheria yaliruhusu wawekezaji binafsi kuwekeza katika sekta ya benki. Hatimaye NBC ilibinafsishwa kwa kuuza sehemu kubwa ya hisa zake kwa Benki ya Biashara ya Afrika ya Kusini na CRDB iliingia ubia na wawekezaji binafsi na shirika la maendeleo la misaada la Denmark (DANIDA).

Hivi sasa kuna benki za biashara 51 na taasisisi nyingine za fedha 9 zinazosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania, lakini huduma za sekya ya fedha nchini siyo za kuridhisha.

**Hali ilivyo hivi sasa katika sekta ya Benki**

- Pamoja na jitihada za kueneza huduma za kibenki kwa kuanzisha matawi mengi zaidi na matumizi ya mtandano wa mawasiliano ya simu kupata taarifa za kibenki na kulipia huduma mbalimbali, bado sekta ya benki imekuwa na mfumo usio sawa wa utoaji wa mikopo na utozaji wa riba, ukilinganisha na hali ya mzunguko wa fedha kiuchumi.

- Maendeleo ya sekta ya fedha yamedorora. Uwiano wa ugavi wa fedha na pato la taifa umepungua toka asilimia 23 mwaka 2015 na kufikia asilimi 20 mwaka 2018

- Pamoja na kupungua kwa mfumko wa bei wastani wa riba ya mikopo ya mwaka mmoja imeongezeka toka asilimia 13.7 mwaka 2016 na kufikia asilimia 18.3 mwaka 2017, na asilimia 16.7 mwaka 2019. Wafanyabiashara wadogo na wa kati hawapati mikopo na wakipata wanatozwa riba ya zaidi ya asilimia 20

- Wastani wa riba ya amana ya muda maalum wa mwaka mmoja imepungua toka asilimia 11.5 mwaka 2016 na kufikia asilimia 8.8 mwaka 2019. Tofauti kati ya riba ya mikopo na riba ya amana imeongezeka toka asilimia 2.2 mpaka kufikia asilimia 9.4 mwaka 2018 na asilimia 7.9 mwaka 2019

- Ukuaji wa mikopo katika sekta binafsi umepungua toka asilimia 25 mwaka 2015 na kufikia asilimia 1.7 mwaka 2017 kabla ya kuongezeka kiasi na kufikia asilimia 4.9 mwaka 2018 na asilimia 11 mwaka 2019.

- Mikopo chechefu isiyolipika imeongezeka toka asilimia 6.6 mwaka 2015 na kufikia asilimia 11.5 mwaka 2017; na kupungua kidogo na kuwa asilimia 9.8 mwaka 2019. Ili sekta ya benki iwe imara, thamani ya mikopo chechefu inatakiwa iwe chini ya asilimia 5 ya mikopo yote

- Kumekuwa na tatizo la kutokuwa na udhibiti wa idadi ya wateja katika matawi kiasi cha kusababisha msongamano mkubwa kama ule wa magari barabarani katika kuwahudumia wateja kwa haraka. Wakati mwingine humchukua mtu mpaka masaa matano akiwa katika foleni ya kusbiri kuweka au kuchukua fedha.

- Mashine za ATM zilizowekwa katika baadhi ya maeneo hazina ubora na hivyo kuzorotesha ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wakati wote.

- Mtandao wa kibenki umejikita zaidi katika maeneo ya mijini na kuwatelekeza wananchi wengi wa maeneo ya vijijini ikiwa ni pamoja na wakulima kupata huduma za kibenki kwa ukaribu. Mathalani Benki ya Rasilimali Tanzania (Tanzania Investment Bank- TIB) ambayo ina dirisha la kilimo (Agriculture window) ipo Dar es salaam.

- Serikali na Watanzania katika sekta binafsi hawamiliki benki kubwa za kibiashara. Utendaji wa mabenki haya unaongozwa na makao makuu yao nje ya nchi. Athari hizi zimeonekana mara kwa mara wakati wa mtikisiko wa uchumi duniani. Mabenki hupunguza kasi ya kutoa mikopo sekta binafsi hata kama Tanzania inakuwa haina matatizo kama yale yanayotokea nchi za Marekani na Ulaya. Serikali hushindwa kutumia benki hizi kupunguza athari za mtikisiko wa uchumi duniani.

- Mashine za ATM zilizowekwa katika baadhi ya maeneo hazina ubora na hivyo kuzorotesha ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wakati wote.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

Sekta ya benki inahitaji kufanyiwa marekebisho ya msingi kuiimarisha ili kurejesha imani ya wananchi kwa benki zilizopo na kujenga mazingira yatakayowahakikishia wawekezaji juu ya uwezo wa mfumo wetu wa benki kukidhi mahitaji yao. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua zifuatazo ili kuhakikisha kuwa mfumo wa kibenki unaimarishwa na kuweza kutoa mchango mkubwa katika kuinua hali za maisha ya watanzania:

**Kuboresha huduma za kibenki nchini**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanyia marekebisho sheria ya Benki Kuu ili iweze kutumia mamlaka iliyopewa katika mazingira ya uwazi na ithibati zaidi katika kutekeleza majukumu yake ya ukaguzi na usimamizi. Aidha mabadiko hayo yatalenga kuziwezesha benki kuwa huru zaidi katika kuamsha huduma mpya katika utoaji wa mikopo kwa nia ya mikopo hiyo kuwafikia watu wengi zaidi. Mfano mzuri wa huduma hizi ni utaratibu unaoruhusu benki kuwekeza katika miradi mbalimbali itakayoona inafaa na kushiriki katika kugawa faida badala ya kutoza riba.

- Pamoja na kuboresha huduma kwa wateja, utaandaliwa utaratibu wa kudhibiti ukomo wa idadi ya wateja katika matawi ili kuondokana na msongamano mkubwa katika kuwahudumia wateja na hii itawezesha uanzishwaji wa matawi mengi zaidi yatakayotoa ajira na kuharakisha maendeleo ya Taifa

- Mtandao wa kibenki utaenezwa mpaka maeneo ya vijijini ili wananchi wengi wa maeneo ya vijijini ikiwa ni pamoja na wakulima waweze kupata huduma za kibenki kwa ukaribu.

- Juhudi za makusudi zitafanyika kuhakikisha kuwa Benki ya uwekezaji Tanzania (TIB) inakuwa na divisheni ya kibiashara ili iweze kusaidia ukuaji wa uchumi kwa kutoa huduma za mikopo kwa wajasiriliamali wetu walio wengi ambao mitaji yao ya biashara ni midogo na haihimili soko la ushindani wa kibiashara

- Sera ya benki itaangaliwa upya ili kupunguza riba ya mikopo na kuweka uwiano wa haki kati ya riba inayotolewa kwa amana za wateja na riba inayotozwa katika mikopo ya wateja. Hii itasaidia wananchi wengi kukopa na kuwa na uwezo wa kulipa bila kuhofia kupoteza amana na dhamana zao.

**Serikali kuendelea kumiliki Benki ya Wananchi**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaendelea kuimiliki benki ya Posta Tanzania na kuiwezesha kimtaji ili iweze kupanua mtandao wa huduma zake katika maeneno yote ya nchi yetu na kufanikisha kuwahudumia wananchi wengi zaidi waliowekwa mbali na huduma za benki za kibiashara.

**Kuboresha huduma za kibenki nchini**

**Benki ya Raslimali Tanzania (Tanzania Investment Bank)**

- Tanzania Investament Bank (TIB) itaongezewa mtaji na kuundiwa Menejimenti na Bodi mpya ya watu wenye ujuzi na uzoefu, na wasio na shutuma za ufisadi na ubadhirifu ili kuijengea uwezo wa kutoa mikopo ya muda mrefu inayolenga uzalishaji, na kuanzisha matawi katika kila mkoa na baadae kila wilaya.

**Benki ya Kilimo ya Tanzania (Tanzania Agricultural Development Bank)**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaiongezea mtaji Benki ya Kilimo ya Tanzania kuiwezesha kuwa na matawi nchi nzima na kuwahudumia wakulima wenye miradi ya kilimo inayoweza kujengewa uwezo na kuongeza tija.

### 3.1.10. MASOKO YA MITAJI NA HISA

Dhana ya masoko ya mitaji na hisa bado ni ngeni kwa Watanzania walio wengi. Ugeni huu unatokana na historia ya nchi yetu kutoka katika sera za "Ujamaa' zilizoshinikizwa kwa watanzania kwa karibu miaka 35 ambazo hazikuwa zinaruhusu kabisa kuwepo kwa aina hii ya masoko. Hata baada ya Serikali ya awamu ya pili kuzitupilia mbali sera hizo na kuruhusu uchumi wa soko huria, bado taasisi hii haikupata kipaumbele kutokana na ukweli kwamba mazingira halisi ya kiuchumi ya wakati huo hayakuwa yanaruhusu. Soko la hisa wakati huo halikuwa na maana yoyote kwa sababu hakukuwa na wanunuzi wala wauzaji. Wananchi ambao mara nyingi ndio wanunuzi (wa hisa) katika soko la aina hii walikuwa taabani kwa umasikini na makampuni (ukiondoa machache sana ) ambayo ndio wauzaji yalikuwa katika hali mbaya mno.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya masoko na mitaji ya hisa**

- Soko la Mitaji na Hisa la Dar es salaam, The Dar es salaam Stock Exchange (DSE), halina uchangamfu wa kutosha na uendeshaji wa shughuli zake ni mdogo sana. Ni kweli kuwa moja ya sababu zinazofanya shuguhuli za soko hili kudorora ni ugeni wa dhana hii kwa Watanzania. Lakini sababu kubwa zaidi ni umasikini wa wananchi. Ni vipi utarajie wananchi kujiingiza katika biashara ya kununua na kuuza hisa hali ya kuwa walio wengi hawana hata kipato kinachoweza kukidhi mahitaji yao ya kawaida ya mwezi?

Umasikini wa watanzania umewafanya walio wengi wasiwe na shauku ya kuwekeza katika miradi ambayo matunda yake yatachukua muda mrefu kuonekena, na si kwa sababu hawaelewi umuhimu wa kuwekeza katika miradi hiyo. Tatizo lao ni kutomudu kusubiri kwa muda mrefu. Hii ndiyo sababu michezo ya upatu, pamoja na matatizo yake, ni maarufu na wananchi huichangamkia sana. Katika upatu faida haitarajiwi baada ya kipindi kirefu cha mwaka, bali ni katika kipindi cha miezi au hata majuma machache tu. Mtu anajua kuwa akiwekeza huko huo ni muda mfupi mno kiasi cha kutoweza kuathiri ulipaji wa karo za wanawe au kodi ya pango kwa mwenye nyumba.

- Hivi sasa Dar es Salaam Stock Exchange ina kampuni 27 tu zilizosajiliwa na kuorodheshwa kwenye soko hilo. Hatifungani za kampuni (Corporate Bonds) sita tu ndizo ziko sokoni hivi sasa

- Hapajakuwepo na nia thabiti au mikakati sahihi mbadala ya kuwasaidia wananchi kuondoa umasikini wao. Kipaumbele kilikuwa kiwekwe kwenye aina zingine za masoko ya mitaji ambazo zingeendana na hali halisi iliyopo. Masoko ya aina hii ni yale yenye mitaji inayotafuta wa kuitumia kwa kuingia ubia, kulelea mawazo mapya ya kibiashara na kuwezesha biashara ambazo tayari ziko sokoni kuongeza kasi ya ukuaji. Masoko haya kwa kiingereza yanajulikana kama **Venture Capital Markets, Start - up Incubators na Growth accelerators.**

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

- Kuimarisha soko la hisa la Dar es salaam (DSE). Pamoja na mambo mengine serikali itahamasisha makampuni zaidi yenye sifa kujiorodhesha kwenye soko la hisa.
- Serikali itaruhusu masoko mengine ya mitaji na hisa kufanya kazi sambamba na DSE ili kuongeza ushindani na kutoa uwanja mpana zaidi wa wanunuzi na wauzaji wa hisa kuchagua.
- Serikali itaruhusu kampuni mpya zinazosajiliwa kujiorodhesha DSE kwa utaratibu maalum ili ziweze kuuza hisa zake kukuza mitaji yao
- Serikali itaimarisha kanuni zinazoyataka makampuni kuweka mahesabu sahihi na pia itaimarisha huduma za ukaguzi.
- Makampuni na mashirika yote ya Serikali yaliyobinafsishwa yatahamasishwa kujiorodhesha kwenye soko hili.

**Kupanua huduma za masoko ya mitaji**

Mbali ya kwamba Serikali itaanzisha mifuko mahususi ya mikopo ya masharti nafuu (Incubator and accelerator Funds) kwa ajili ya kulea na kuharakisha ukuaji wa shughuli za kiuchumi zinazomilikiwa na wajariamali wazalendo kama ambavyo imekwishaelezwa kwenye sehemu nyingine za Ilani hii, serikali pia itatoa leseni kwa makampuni binafsi yatakayokuwa na nia ya kufungua mifuko ya aina hii kwa nia ya kuwawezesha wananchi wenye mawazo mapya ya kibiashara lakini wasio na sifa za kukopa katika mabenki, kufanikisha malengo yao.

### 3.1.11. HUDUMA ZA BIMA

Dhana ya Bima ni kutoa kinga ili kufidia madhara yanayoweza kutokea. Mbali ya kwamba nchini Tanzania ziko bima za aina nyingi, ni aina

chache tu (zile ambazo zinalazimishwa kwa mujibu wa sheria) ndizo ambazo zimeshamiri. Bima nyingi muhimu, kama vile bima ya kinga dhidi ya uharibifu kwenye biashara-mathalani kutokana na moto, bima ya kinga dhidi ya unyang'anyi, n.k, bado haziwavutii wananchi wengi.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya Bima nchini**

Kwa muda mrefu mno kumekuwa na usumbufu mkubwa kwa wananchi wengi ambao walikuwa wakifuatilia malipo yao ya bima NIC - ambalo lilikuwa ndiyo shirika pekee la bima nchini. Wakati mwingine kwa visingizio mbalimbali ilichukua hata zaidi ya mwaka mmoja kabla ya muathirika kufidiwa. Hali hii imewafanya wananchi wengi wajenge utamaduni wa kutokuwa na imani na taasisi za bima. Hivi sasa soko la bima ni huru na ufanisi umeongezeka kwa kiasi kukubwa. Kuna kampuni 32 zilizosajiliwa kufanya biashara ya bima nchini.

**Dira ya mabadiliko ya CUF**

**Umarishwaji wa shirika la bima la Taifa (NIC)**

Shirika la Bima la Taifa litaendelea kuimarishwa kwa kuongezewa mtaji ili pamoja na mambo mengine lifanye shughuli zake kwa ufanisi na liweze kuhimili ushindani na makampuni binafsi ya bima na hatimaye liweze kuuza hisa zake katika soko la hisa.

**Uimarishaji wa ushindani katika sekta ya bima**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahimiza Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania (TIRA) kusimamia vizuri sekta ya bima ili kuimarisha ushindani na kupanua orodha ya huduma zinazotolewa. Aidha serikali itaihimiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bima na makampuni ya bima kutoa elimu ya kina kwa wananchi kuhusu huduma zao ili zieleweke; na wananchi wengi zaidi waweze kushiriki.

### 3.1.12. HIFADHI YA JAMII

Nchini Tanzania kwa sasa kuna mifuko miwili ya hifadhi ya jamii. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ambao wanachama wake wengi ni watumishi wa sekta ya umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ambao kila mfanyakazi kwenye sekta binafsi rasmi ni lazima kisheria awe mwananchama. Mbali ya nia nzuri ya kuwepo kwa mifuko hii, uendeshaji wake umekuwa na manufaa kidogo kwa wanachama wake na badala yake serikali imekuwa ikitumia fedha za wanachama kujinufaisha. Sheria inayowazuia wanachama walioacha au kuachishwa kazi kabla ya kufikia umri wa kustaafu kuchukua fedha zao mpaka wafikie umri wa kisheria kuweza kustaafu, ina nia ya kuiwezesha serikali kupitia mifuko hiyo kujikopesha fedha za wanachama hao.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya hifadhi ya jamii**

- Kwa muda mrefu sasa mifuko hii imekuwa ikiwekeza fedha za wanachama wake kwenye vitega uchumi mbalimbali lakini faida itokanayo na vitega uchumi hivi haigawiwi kwa wanachama. Mifuko hii imekuwa ikikopesha fedha za wanachama kwa watu ambao siyo wanachama.

- Serikali inadaiwa mabilioni na mifuko hii kwa kuchelewa kulipa michango ya watumishi wa umma.

- Mifuko hii imekuwa ikihodhi fedha za wanachama zinazotokana na michango ya mwajiri, pale inapotokea mfanyakazi kufukuzwa kazi. Aidha kumekuwa na usumbufu mkubwa kwa wanachama wanaotaka kuchukua michango yao baada ya kuacha ajira zao.

- Sera ya kukata kodi mafao ya wafanyakazi wanaostaafu au kuacha na kuachishwa kazi haina mantiki hata kidogo ikizingatiwa kuwa muathirika anahitaji sana mafao haya kama

mtaji wa kujianzishia shughuli nyingine za kujiendeshea maisha yake, na mafao haya ni sehemu ya mapato ambayo tayari yalishakatwa kodi.

- Sera hizi mbovu za huduma ya hifadhi ya jamii huwalenga zaidi watumishi walio katika sekta rasmi na kuwatelekeza kabisa wananchi wengi walio katika sekta isiyo rasmi; hususani wakulima, wafugaji, na wavuvi.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

**Kuifanya mifuko hii iwajibike zaidi kwa wanachama**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua zifuatazo ili kuboresha hifadhi ya jamii na kuofanya iwe na maana kwa walengwa:

- **Kulipa madeni yanayodaiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii**. Serikali italipa madeni inayodaiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii bila kuchelewa ili kuiimarisha na kuifanya iwe na program zinazolenga kuwanufaisha zaidi wanachama wake.

- **Mgawanyo wa faida inayotokana na vitega uchumi.** Mifuko hii itawajibika kugawa robo tatu ya faida yote inayotokana na vitega uchumi vilivyotokana na kuwekeza fedha za wanchama, kwa wanachama wa mifuko hiyo.

- **Malipo kwa wanachama wanaoacha ajira zao.** Malipo yao yatakamilishwa katika kipindi cha miezi mitatu (3) na mwanachama atakuwa na haki ya kuchagua utaratibu wa malipo anaoutaka. Sheria itarekebishwa ili mwanachama awe na haki ya kuchukua fedha zake zote kwa mkupuo mmoja iwapo huo ndio utakuwa uamuzi wake.

- **Kusitisha utaratibu wa kujimilikisha michango ya waajiri.** Utaratibu huu utasisitishwa mara moja na michango ya mwajiri

atakabidhiwa mfanyakazi aliyefukuzwa kazi sambamba na michango yake.

- **Kusitisha utaratibu wa kukata kodi kwenye mafao ya wanayakazi.** Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafuta mara moja utaratibu wa kukata kodi kwenye mafao ya wafanyakazi wanaostaafu au kuacha kazi, ili kutoa fursa kwa wahusika kujianzishia shughuli za kuendeshea maisha yao wakiwa na uwezo mzuri zaidi.

- **Kuasisi sera ya Taifa ya hifadhi ya jamii.** Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaasisi sera ya taifa ya hifadhi ya jamii ili huduma hii iweze kuwanufaisha wananchi walio wengi, ikiwa ni pamoja na wale wanaofanya shughuli zao katika sekta isiyo rasmi.

### 3.1.13. MATUMIZI YA BANDARI

- Ni nchi chache duniani zenye jiografia nzuri kama Tanzania lakini hazitumii jiografia husika kama nyenzo ya kujinufaisha kiuchumi. Tanzania ina ufukwe wa bahari upatao kilometa 1424 na ndani yake kuna Bandari za Tanga, Dar es salaam, Mtwara na Zanzibar kwa upande wa mashariki. Upande wa Kaskazini, Kaskazini Magharibi, na Kusini Magharibi inapakana na mataifa ya Uganda, Rwanda, Burundi, Congo, Zambia na Malawi. Haya yote ni mataifa ambayo hayakujaaliwa milango ya bahari, hivyo ni tegemezi kwa mataifa ya jirani ya Tanzania, Kenya, na Msumbiji kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa zao.

- Miongoni mwa nchi hizi tatu - yaani Tanzania, Kenya na Msumbiji, Tanzania ina nafasi ya kipekee kabisa. Tofauti na Kenya ambayo nchi pekee inazopakana nazo zisizokuwa na bandari ni Uganda na Sudan ya kusini, au tofauti na Msumbuji ambayo nchi pekee inazopakana nazo zisizokuwa na bandari ni Swaziland, Zimbabwe, na Malawi; Tanzania kama ambavyo tumekwishaona inapakana na

mataifa sita yasiyo na bandari. Hii ina maana kwamba bandari zetu za Tanga, Dar es salaam, na Mtwara ni maeneo yaliyotakiwa kuwa na harakati nyingi za usafirishaji wa bidhaa zinazoingia na kutoka katika nchi hizi za jirani. Kwa kifupi bandari hizi zilitakiwa kuwa ni chanzo kikubwa sana cha ajira na mapato ya nchi.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya Bandari nchini**

- Huduma mbovu bandarini na mtandao mbovu wa njia za reli na barabara ni mambo ambayo yemesababisha nchi jirani zisizo na bandari kutopendelea kuendelea kutumia bandari zetu kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, Malawi na Zambia ziko karibu zaidi na bandari ya Mtwara kuliko zilivyo karibu na bandari ya Dar es salaam. Hata hivyo zinapoamua kusafirisha bidhaa zake kupitia Tanzania zinalazimika kutumia bandari ya Dar es salaam kwa sababu mawasilino ya barabara na reli ni rahisi zaidi. Hali kadhalika Uganda iko karibu zaidi na bandari ya Tanga kuliko ilivyo karibu na bandari ya Dar es salaam, lakini ni rahisi zaidi kwa njia hiyo.

- Wizi na uzembe ni mambo ambayo yanawafanya wafanyabishara wengi wa nchi jirani kupendelea bandari za nchi nyingine kuliko zile za kwetu. Mathalani, Zambia ilishawahi kutamka wazi kuwa pamoja na umbali kati ya Zambia na Afrika Kusini, na uhusiano wa karibu kati yake na Tanzania, iko radhi ianze kutumia bandari za Afrika Kusini kusafirishia bidhaa zake kwa sababu:- mosi, itakuwa na uhakikia wa usalama wa bidhaa hizo, na pili upotevu wa muda utakuwa mdogo. Hali kadhalika kwa sababu hizo hizo sehemu kubwa ya bidhaa za Uganda na Rwanda hupitia katika bandari ya Mombasa nchini Kenya.

- Kuna urasimu mkubwa katika kutoa makontena bandarini. Inaweza kumchukua mfanyabiashara wiki au miezi kadhaa

kufanikiwa kupata mizigo yake kutoka bandari za Tanzania. Huu ni uzembe mkubwa na unawafanya wafanyabiashara wengi wazikimbie bandari zetu.

**Dira ya mabadiliko ya CUF**

Ni wazi kabisa kuwa kungekuwapo na njia za reli zinazounganisha bandani ya Mtwara na Mbamba Bay kwenye Ziwa Nyasa, na miji ya Arusha na Mwanza kwenye ziwa Victoria, na hali ya ufanisi ikaongezwa katika utendaji wa bandari zetu, bila shaka bandari za Mtwara na Tanga zingekuwa ni bandari chaguo la kwanza kwa nchi za Malawi na Uganda. Hali hii ingepunguza msongamano kwenye bandari ya Dar es salaam na kutoa nafasi kwa bandari hii kutoa huduma bora zaidi kwa nchi za Zambia, Congo, Burundi na Rwanda.

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua za makusudi kabisa kuhakikisha kuwa bandari zetu zinakuwa ni chanzo kikubwa cha mapato ya nchi na ajira. Hatua hizi ni pamoja na:-

**Kuongeza ufanisi na tija kwenye utendaji wa bandari zetu**

- Ubinafsishaji wa baadhi ya shughuli za bandari utaendelezwa ili kuvutia teknolojia mpya, mitaji, utaalamu na ufanisi, hususan katika usalama wa bidhaa za wateja.

- Kutakuwa na utaratibu wa makusudi wa kujifunza kutoka kwa wenzetu waliopata mafanikio makubwa kwenye matumizi ya bandari zao.

- Mradi wa Bandari ya Bagamoyo na Eneo lake la Uwekezaji utapitiwa upya na kurekebisha kasoro zilizopo ili utekelezwe.

**Kuzifanya bandari zetu ziwe ni chaguo la kwanza;**

Ili kuzifanya bandari zetu kuwa ni chaguo la kwanza kwa wasafirishaji wa mizigo wa nchi jirani, pamoja na kuongeza ufanisi katika utendaji tunahitaji pia kuangalia suala la gharama kwa wasafirishaji hao. Kama ambavyo tayari imeshaelezwa, kuna wasafirishaji ambao wangevutiwa zaidi na matumizi ya bandari za Tanga na Mtwara iwapo kungekuwa na usafirishaji mzuri wa reli kuanzia kwenye bandari hizo. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua za dharura kabisa kutafuta wawekezaji watakaowekeza katika ujenzi wa njia hizo za reli.

Serikali itahakikisha kuwa panakuwa na kampuni za uhakika za kupakua na kupakia mizigo na itazisimamia ipasavyo ili kuondoa msongamano bandarini na kufanya mhusika kupokea mzigo wake kwa siku chache baada ya mzigo kuwasili bandarini. Kampuni ambayo itashindwa kufanya kazi hii kwa haraka na kwa ufanisi itaondolewa mara moja na kazi kupewa kampuni nyingine.

### 3.1.14. MAPATO YA KODI

Kulipa kodi ni wajibu wa kila mwananchi mwenye uwezo wa kiuchumi kufanya hivyo. Hata hivyo mazingira ya ulipaji kodi yanatakiwa yaandaliwe vizuri kiasi kwamba wajibu huu ugeuke kuwa ni utamaduni uliokumbatiwa na wananchi na siyo jambo la kuchukiza.

Iwapo utamaduni wa namna hii utajengwa ni dhahiri kabisa kuwa mapato ya serikali yatokanayo na kodi yatakuwa ni makubwa na ya kuridhisha. Kwa bahati mbaya sana mazingira yaliyoko nchini kwetu katika masuala ya kodi yamekuwa ni kizingiti dhidi ya kukua kwa utamaduni huu. Hali hii imesababisha kuwe na udhaifu mkubwa katika uksanyaji wa kodi.

**Hali ilivyo sasa katika eneo la mapato ya kodi**

- Viwango vya kodi vimepelekea kujengeka kwa hisia kuwa ni vikubwa mno kiasi cha kutishia uhai wa biashara au maendeleo ya mlipa kodi.

- Hisia za matumizi mabaya na ufisadi wa fedha za walipa kodi unaofanywa na Serikali umewafanya walipa kodi wengi kuwa na imani kuwa kodi inayokusanywa haitumiki kwa maslahi ya Taifa.

- Hivi sasa kuna utaratibu wa kutoza kodi ambao unawapendelea walipa kodi wakubwa (kwa kuwapa misamaha holela) na kuwakandamiza walipa kodi wadogo.

- Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) imekuwa ikitumiwa na serikali ya CCM kuwatisha walipa kodi, na hususani wafanyabiashara wakubwa ili kuiunga mkono CCM na Yule ambaye hafanyi hivyo hutozwa kodi kubwa kuliko uhalisia au kufilisiwa kwa mlango wa nyuma.

- Kumekuwa na tozo za kodi zinazojirudia (Duplication of Taxes) kwa bidhaa au huduma ileile, jambo ambalo linawaumiza walaji na kuwakatisha tama wafanyabiashara.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2000 CUF - Chama cha Wananchi kilifanya kampeni kubwa dhidi ya mwenendo mzima wa ukusanyaji kodi nchini. Kutokana na juhudi hizi kumekuwa na mafanikio kiasi Fulani. Mafanikio haya ni pamoja na kuondolewa kwa utaratibu uliokuwepo uliokuwa unamshinikiza mlipa kodi kulipa sehemu ya kodi inayotarajiwa (Provisional Taxes) kabla ya kuanza kwa shughuli yenyewe inayotakiwa itozwe kodi, na kufutwa kwa kilichokuwa kinaitwa kodi ya maendeleo. Hata hivyo bado kunahitajika marekebisho makubwa katika mfumo wa kodi na jinsi inavyotumiwa ili kuwajengea watanzania utamaduni wa kuridhia kulipa kodi. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF

inakusudia kuchukua hatua zifuatazo ili kufanya Mabadiliko ya kweli kwenye mfumo wa kodi kwa ajili ya kuleta manufaa yanayotarajiwa na wananchi:

**Kodi za Serikali kuu**

**Kuangalia upya viwango vya kodi**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itavipitia upya viwango vyote vya kodi zinazotozwa na Serikali Kuu kwa nia ya kuvirekebisha visiwe ni kero kwa walipa kodi. Viwango vya kodi vinavyohusu vifaa vya elimu, vifaa vya afya, pembejeo za kilimo, maji, nishati, ujenzi wa makazi binafsi na mawasiliano ikiwa ni pamoja na reli na barabara vitapewa upendeleo maalum kwa kipindi cha miaka kumi ili kukuza uwekezaji katika maeneo hayo.

**Utaratibu wa kodi ya mapato kwa kampuni mpya**

Wafanyabiashara wapya hufanya kazi kwa miezi mitatu tu kabla ya kuanza kulipa kodi. Huu ni muda mfupi mno kwa biashara kuanza kuonyesha mwelekeo. Pamoja na mambo mengine, Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaondoa utaratibu huu na badala yake wafanyabiashara wapya waliosajiliwa kama kampuni watawajibika kulipa kodi ya mapato katika faida halisi watakayopata baada ya kipindi kimoja cha biashara (mwaka mmoja) kumalizika.

**Misamaha ya kodi**

Hakutakuwa na misamaha ya kodi. Iwapo itatokea kuwa kwa sababu Maalum za Kimkakati kuna umuhimu wa kutoa msamaha wa kodi fulani, basi Serikali italiomba Bunge kuidhinisha msamaha huo baada ya kuhakikisha kuwa msamaha huo wa kodi utaongeza tija katika uchumi wa nchi.

Marekebisho kwenye kodi za mauzo na VAT. Kodi ya ongezeko la thamani (VAT) itashushwa kutoka asilimia kumi na nane (18%) ya sasa hadi asilimia kumi na tano (15%). Hata hivyo wigo wa wafanyabiashara wanaostahili kujiorodhesha kwa ajili ya kodi hii utapanuliwa na kuwaingiza wafanyabiashara wote ambao mauzo yao kwa mwaka hayapungui shilingi milioni 20. Hata hivyo, utaratibu wa ushuru wa stampu kwa wale wafanyabiashara wasio na sifa ya kujiorodhesha kwa ajili ya VAT utatumika.

**Ushuru wa barabara**

Mianya ya kukwepa ushuru wa barabara unaotozwa katika mafuta ya petrol na dizeli itachunguzwa na kuondolewa.

**Matumizi ya kodi maalum**

Hivi sasa kuna kodi kadhaa ambazo hutozwa maalum kwa ajili ya kuimarisha eneo fulani la huduma, mathalani ushuru wa barabara. Hata hivyo matumizi ya kodi hizi yamekuwa hayaeleweki vema na mara nyingi kisingizio kinachotolewa ni kwamba zimechotwa kugharamia masuala fulani nje ya yale yaliyokusudiwa. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itapitisha sheria inayozuia matumizi ya kodi hizi nje ya makusudio ya awali, na iwapo kutakuwa na dharura yoyote inayohitaji sehemu ya kodi hizi kutumika nje ya makusudio yake, itabidi kwanza serikali iombe idhini ya Bunge.

**Kodi katika mafao ya wastaafu**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafuta kodi yoyote inayotozwa kwenye mafao ya wafanyakazi wanaostaafu au kupunguzwa makazini, kwasababu yoyote ile. Ufutaji wa misamaha holela ya kodi, kurahisisha ukusanyaji wa kodi na kukusanya kodi stahiki toka sekta ya madini kutaongeza ukusanyaji wa pato la Taifa kama mapato ya Serikali.

**Kodi za Serikali za Mitaa**

**Kutenganisha vyanzo vya kodi**

- Ni muhimu sana vyanzo vya kodi za Serikali kuu na zile za Serikali za mitaa vikatenganishwa ili kuondoa uwezekano wa kuwatoza wananchi kodi ya aina moja mara mbili. Serikali za mitaa zitatakiwa kuangalia upya kodi zinazotoza na pale ambapo itabainika kodi fulani inayotozwa tayari inatozwa na Serikali Kuu japo kwa jina tofauti, kodi hiyo itafutwa.

- Kodi na ada za mazao. Ilikuongeza motisha kwa wakulima kodi na ada za mazao zitafutwa katika ngazi ya mkulima.

- Marekebisho ya sheria yatafanyika ili kuziwezesha ngazi za kata kusimamia maendeleo ya maeneo yao kwa kurejeshewa nusu ya mapato yanayotokana na kata husika. Mapato yanayorejeshwa yatatumiwa na kata katika kupanga na kusimamia miradi ya maendeleo ndani ya kata.

### 3.1.15. MTANDAO WA MAWASILINO

Moja ya mambo yanayochangia kuongezeka haraka kwa maendeleo katika nchi ni mtandao mzuri wa mawasiliano. Barabara, reli, usafiri wa majini pale unapowezekana, usafiri wa anga, simu, fax, na hivi sasa intaneti vimethibiti kuwa ni nyenzo muhimu za maendeleo. Kuwepo kwa njia za uhakika za usafiri ndani ya nchi kunarahisisha sana usafirishaji wa idadi kubwa ya watu na kiasi kikubwa cha bidhaa toka pande moja ya nchi hadi nyingine. Hali hii mbali ya kuokoa muda, pia ina mchango mkubwa katika kushusha gharama za kibiashara na hatimaye bei ya bidhaa. Hali kadhalika inasaidia sana kukuza maingiliano ya watu kwenye jamii na hivyo kufanya watu wa upande mmoja kujifunza kutoka kwa watu wa upande mwingine. Kwa kifupi mtandao mzuri wa mawasiliano unaongeza tija kwa kwango cha juu iwe ni kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Aidha kuwepo kwa mawasiliano mepesi ya

mbali (simu, e mail, internet, na fax) kumeongeza uhakika wa miamala na kupunguza muda wa kuikamilisha. Hali hii inapunguza gharama za kufanya biashara na kuwezeshwa faida kubwa zaidi kuzalishwa.

### 3.1.16. RELI NA BARABARA

**MTAZAMO WA CUF JUU YA USAFIRI WA RELI NA BARABARA NCHINI**

Tanzania ina tatizo kubwa la mawasiliano ya ardhini kwa maana ya usafiri na usafirishaji. Sehemu kubwa ya mtandao wa barabara uko katika hali mbaya kabisa. Kielelezo cha ubovu wa barabara zetu si kigeni kabisa kwa wakazi wa miji yetu. Barabara takribani zote alizoziacha mkoloni zikiwa na lami hivi sasa ni vumbi na makorongo matupu. Pamoja na tuhuma za uongozi mbaya unaosimamia mamlaka za Reli zilizoko nchini, mtandao wa reli uliopo mbali ya kwamba ni chakavu, pia hauko kimkakati. Tanzania ina njia kuu za reli tatu. Kuna reli ya kati inayoanzia Dar es salaam hadi Kigoma na ambayo ina tawi linaloanzia Tabora hadi Mwanza. Kuna reli ya Tanga inayoanzia Tanga hadi Moshi na Arusha na pia kuwa na matawi, moja linaloanzia Korogwe hadi Dar es salaam, na jingine linaloanzia Kahe (mkoani Kilimanjaro) hadi Taveta mpakani mwa Kenya na Tanzania. Reli ya tatu ni ile ya TAZARA inayoanzia Dar es salaam hadi Tunduma mpakani mwa Tanzania na Zambia.

Reli za Tanga na ile ya kati zilijengwa na wakoloni wa Kijerumani kati ya mwaka 1896 na 1905. Baadaye wakoloni wa Kiingereza waliongeza matawi katika reli hizo yanayounganisha miji tuliyoitaja. Wajerumani walipozijenga reli hizi kusudio lao kubwa lilikuwa kurahisisha usafirishaji wa mazao (hasa katani, kahawa na pamba) kufika kwenye bandari za Tanga na Dar es salaam. Wakoloni wa Kiingereza hali kadhalika nao walizitumia reli hizi kikamilifu kwa malengo hayohayo. Kudidimia kwa kilimo cha mazao ya biashara baada ya uhuru na kuwepo kwa barabara nzuri inayoiunganisha mikao ya Arusha,

Kilimanjaro, Tanga na Dar es salaam kumepunguza kwa kiasi kikubwa umashuhuri wa reli ya Tanga.

Ili kuurejesha umaarufu wake inabidi juhidi zifanyike kuongeza wingi wa mizigo inayohitaji kufikishwa bandarini Tanga. Ni dhahiri kabisa kuwa kuhuishwa kwa shughuli za kilimo cha kibiashara katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, na Tanga yenyewe kutatoa mchango mkubwa katika kufanikisha hili. Lakini kuenda mchango mkubwa zaidi ukatokana na kufanikisha juhudi za kuhakikisha kuwa bidhaa za Uganda, na pengine Rwanda, zinasafirishwa kupitia reli hii kwenda na kutokea bandarini Tanga. Hata hivyo ili suala hili lifanikiwe itabidi kwanza lijengwe tawi la reli litakaloiunganisha miji ya Arusha na Mwanza.

Hadi hivi karibuni umuhimu wa reli ya kati ulikuwa ni wa kipekee kabisa ikizingatiwa kuwa hakukuwa na mtandao wa barabara nzuri uliokuwa unaunganisha mikoa ya Dar es Salaam na ile ya kanda ya ziwa. Reli ya kati ndiyo iliyokuwa inatoa usafiri pekee wa uhakika uliokuwa unategemewa na sehemu kubwa ya wananchi wa kanda ya ziwa. Katika miaka ya hivi karibuni umuhimu wa reli hii umepungua kufuatia kukamilika kwa barabara ya lami inayotokea Dodoma hadi Mwanza na ujenzi wa daraja katika mto Malagarasi ambao umewezesha usafiri wa barabara kwenda mkoa wa Kigoma.

Reli ya TAZARA ilijengwa kwa msaada kutoka China kwa ushirikiano kati ya Tanzania na Zambia kati ya mwaka 1970 na 1975. Reli hii ilijenggwa kwa kuzingatia zaidi hali ya kisiasa iliyokuwepo kusini mwa Afrika katika miaka ya sabini, kuliko mahitaji ya kiuchumi ya Watanzania. Ujenzi wa reli hii ulizingatia zaidi kuisaidia Zambia kufikisha bidhaa zake (na hasa hasa madini ya shaba) katika bandari ya Dar es salaam baada ya njia za kusini, kupitia Zimbabwe hadi Beira nchini Msumbiji, au Zimbabwe hadi Afrika Kusini kuwa hazipitiki kutokana na vita vya ukombozi. Reli hii haikuzingatia ukweli kuwa kuna

siku vita vya ukombozi vingemalizika, na Zambia ianze kuvutika tena kutumia njia za Kusini kwa usafirishaji wa bidhaa zake. Bila shaka wangelizingatia hili wangehakikisha kuwa reli inajengwa kufuata maeneo yote yenye wingi wa watu (tofauti na ilivyo sasa) ili ikitokea kuwa usafirishaji wa bidhaa za Zambia unadorora, reli hii inaendelea kuwa huduma muhimu kibiashara na kimawasiliano kati ya maeneo hayo. Hivi sasa reli hii inakabiliwa na tishio la Zambia kukimbilia nchi za kusini mwa Afrika kwa usafirishaji wa bidhaa zake. Migogoro ya mara kwa maraya kiuendeshaji inayolikumba shirika la TAZARA ni kioo cha hali hii. Ni wazi kabisa kuwa zanahitajika juhudi kabiashara kuiokoa reli hii kabla haijafikwa na kile kilichovifika viwanda vyetu. Ujenzi wa matawi kati ya Tunduma na Rukwa, Mbeya na mpaka wa Malawi kuunganisha na Songea, Tunduru hadi bandarini Mtwara kutatoa uhai mkubwa sana siyo kwa TAZARA tu, bali pia kwa bandari ya Mtwara na shughuli za kiuchumi kwa ujumla kwa eneo lote la kusini.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya mawasiliano ya Reli na Barabara**

- Rushwa, Ubadhirifu na kutojali ndani ya Serikali vimetoa mchango mkubwa katika kusababisha hali mbaya katika sekta ya mawasiliano ya ardhini kama tunavyoshudia hivi sasa.

- Bado Serikali imeshindwa kuona kuwa matumizi ya vivuko katika maeneo ambayo hayana madaraja katika barabara kuu na barabara zinazounganisha mikoa, kwa malengo ya muda mrefu yana gharama kubwa zaidi kuliko kujenga madaraja katika maeneo hayo.

- Pamoja na hatua za serikali ya awamu ya tano kuikarabati reli ya Tanga, kufa kwa kilimo cha kibiashara katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, na Arusha, na kutokuwa na nia thabiti ya kupanua fursa za kibiashara na nchi ya Uganda kunabaki kuwa ni tishio kubwa kwa reli hiyo. Serikali haiwezi kuendelea kubeba hasara ya

kuendesha reli hiyo bila kuwepo kwa mizigo ya kutosha kwa ajili ya kuifanya ijiendeshe kibiashara.

- Ubinafsishaji usio makini wa uendeshaji wa shirika la Reli umeliongezea matatizo na kudidimiza ufanisi wa shirika hilo na kuathri kwa kiasi kikubwa juhudi za wananchi za kujikwamua kiuchumi. Kuna malalamiko yanayohusu huduma mbovu katika mabehewa, ikiwa ni pamoja na kujaa wadudu kama kunguni, mende, panya na uchafu wa kila aina.

- Katika kipindi cha miaka ishirini iliyopita Serikali ya CCM imeingia katika mashindano na CUF kuhusu kuweka mtandao wa barabara nchini, baada ya dhamira ya CUF juu ya suala hili kuwa wazi kupitia Ilani zilizopita. Hata hivyo kama ilivyo kawaida ya jambo lolote ambalo halifanyiki kwa dhati kuna ushahidi kuwa barabara takribani zote zinazojengwa chini ya miradi hii zina ubora ambao uko chini ya viwango vinavyotakiwa.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha mawasiliano ya barabara na Reli kuwa ni miongoni mwa mambo yanayoendelea kupewa umuhimu wa kipekee. Ili kufanikisha hili serikali itatenga fedha za kutosha kukarabati na kujenga barabara na reli mpya.

**MKAKATI WA CUF KUBORESHA USAFIRI WA RELI**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itakaribisha wawekezaji wa kibiashara kwenye ujenzi wa matawi ya reli ambayo umuhimu wake tayari tumekwisha ueleza hapo juu.

- Kwa sababu reli ni raslimali ya kistrategia Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF haitalibinafsisha shirika la Reli isipokuwa litapatiwa menejimenti makini na bodi imara yenye uhuru wa

maamuzi na kufanya kazi zake kitaalamu zaidi, na kwa kuzingatia maslahi ya Taifa. Menejimenti itapewa mikataba yenye viwango vinavyopimika (Performance Management Contracts).

- Pamoja na mambo mengine menejimenti itakuwa na wajibu wa kuhakikisha inaboresha huduma za usafiri wa reli. Uboreshaji utapimwa kwa:

i. Kuwa na vifaa vya kisasa vya utendaji kazi, ikiwa ni pamoja na mabehewa ya abiria na mizigo yenye viwango na hadhi ya kimataifa, ili kuweza kulinda usalama na afya za abiria na mizigo; na

ii. Kuwa na ratiba ya uhakika ya usafiri na usafirishaji na kuwajibika kikamilifu, ikiwa ni pamoja na kulipa fidia, pale itakapozembea kutekeleza wajibu wake kwa wateja.

**MKAKATI WA CUF KUBORESHA BARABARA NCHINI**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa ushuru wote wa barabara unaelekezwa kwenye ujenzi wa barabara mpya na kurekebisha zile zilizoharibika, huku asilimia 50% ya fedha za ushuru wa barabara zikielekezwa kwenye ujenzi wa barabara za vijijini. Aidha wawekezaji kwenye sekta ya barabara (Kwa ajili ya ujenzi wa barabara zitakazolipiwa ushuru, yaani Toll Roads) watatafutwa ili pamoja na matumizi ya kodi ya serikali na misaada tunayoweza kupata kutoka nchi mbalimbali marafiki, kasi ya kuboresha usafiri wa barabara nchini kote iwe ya kuridhisha.

- Katika kipindi cha miaka mitano Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa maeneo yote ambayo hivi sasa yanatumia vivuko katika barabara kuu na mabarabara

zinazounganisha mikoa, yatakuwa na madaraja ya uhakika na utumiaji wa vivuko kusitishwa. Kabla ya kufikia malengo haya uvushaji katika vivuko vyote utakuwa bila malipo.

- Pamoja na kukarabati barabara zilizopo Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itajenga kilomita 500 za barabara kuu mpya za lami kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano.

- Sekta ya miundo mbinu na hasa ujenzi wa barabara imekuwa ikilalamikiwa juu ya uwepo wa ubadhirifu na ufisadi kutokana na makandarasi kujiingiza au kulazimishwa kushiriki utoaji wa rushwa na kuathiri ubora wa viwango vya barabara zinazojengwa. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua maalumu za kudhibiti suala hili kwa kuzingatia na kuiboresha sheria ya manunuzi ya umma, na kuhakikisha kuwepo kwa utaratibu makini wa kuingia katika mikataba ya ujenzi.

- Sanjari na kuthamini makandarasi wazalendo, suala la kuharakisha ujenzi wa miundo mbinu ili kukuza uchumi wa Taifa ni jambo linalohitaji kupewa msukumo wa kipekee. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha miradi mikubwa ya ujenzi inapewa makampuni yenye uwezo mkubwa kifedha, kiutendaji (vifaa vya kutosha na vya kisasa), uzoefu, na utaalamu wa hali ya juu.

Makampuni haya yatepewa kazi hizo na kuwekewa utaratibu wa kuwashirikisha wazalendo (sub-contracts) katika kutekeleza kazi za mradi husika. Lengo hapa ni kuondokana na ucheleweshwaji wa miradi ya barabara kutokana na mapungufu ya kiutendaji na kiufundi, jambo ambalo aghalabu hupelekea wakandarasi kufanya kazi kwa kulipua na wakati mwingine kusababisha gharama za mradi kuongezeka.

### 3.1.17. USAFIRI WA MAJINI

Ukiondoa hali ilivyo sasa kati ya Dar es salaam na Zanzibar ambako wawekezaji kadhaa wanaendesha safari za maboti yaendayo kasi, hali katika meneo mengine yanayohitaji usafiri wa majini siyo ya kuridhisha. Usafiri wa baharini kati ya Dar es salaam na mikoa ya kusini, na kati ya Dar es salaam na kisiwa maarufu cha Mafia, umedidimia kabisa. Usafiri katika maziwa makuu kwa sehemu kubwa unategemea meli chakavu za kizamani ambazo mbali ya kuhatarisha usalama wa abiria, kutokana na uchakavu unaozikabili zinashindwa kuwa na ratiba za uhakika.

Kwa nyakati tofauti tumeshuhudia maafa ya watu wengi yakitokea na bado hatujaweza kuitumia vizuri fursa hii ya kuwa na bahari na maziwa makuu. Juhudi za watu mbalimbali kuwekeza katika usafiri wa majini katika maeneo ambayo hivi sasa yana tatizo kubwa la usafiri huo zimekuwa zikikwama kutokana na sababu zisizokubalika zinazonasibishwa na ubinafsi na ufisadi.

**MKAKATI WA CUF KUBORESHA USAFIRI WA MAJINI**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanya juhudi kubwa kupata wawekezaji watakaowekeza katika maeneo yote ambayo hivi sasa yanahitaji usafiri wa majini. Kwa sababu huduma hizi hazipo kabisa katika maeneo mengi serikali itaweka msamaha wa kodi wa miaka mitano mfululizo kwa watakaokubali kutoa huduma ya usafirishaji katika sehemu zote ambazo zimekuwa hazina usafiri wa majini kwa muda mrefu. Serikali itafanya kila liwezekenalo bila kuathiri maslahi ya Taifa kuwasaidia wawekezaji hao kufanikisha utoaji wa huduma hii muhimu.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaasisi mpango wa kuanzisha bandari nyingi ndogo ndogo katika miji na vijiji vikubwa vilivyoko katika mwambao wa bahari na maziwa makuu ili

kusogeza karibu zaidi huduma ya usafiri na usafirishaji wa majini kwa wananchi.

### 3.1.18. USAFIRI WA ANGA

- Usafiri wa anga siyo maarufu sana kwa Watanzania walio wengi, kwani wananchi wengi hawana uwezo wa kumudu gharama kubwa zinazoambatana na usafiri huo. Pili, kuna mikoa michache tu ambayo ina viwanja vya ndege vinavyoweza kuhudumia ndege kwa muda wote. Mikoa minigne haina viwanja vya ndege kabisa au vilivyopo ni vya msimu. Ukosefu wa viwanja vya ndege katika maeneo mengi ya nchi vyenye uwezo wa kuhudumia ndege muda wote kumesababisha wawekezaji wengi wasivutiwe kuwekeza katika aina hii ya usafiri.

**MKAKATI WA CUF KUBORESHA USAFIRI WA ANGA**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itakaribisha wawekezaji kuwekeza zaidi katika sekta ya usafiri wa anga, na hasa yale makampuni ya nje ambayo yana uzoefu mkubwa katika kutoa huduma za haraka kati ya mji na mji (shuttle services). Kwa kawaida makampuni haya yanatoa huduma ya usafiri wa anga kwa gharama nafuu sana kiasi kwamba huduma zao zinavuta watu wa aina zote wakiwemo na wananchi wenye kipato cha chini.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa walau kila mkoa nchini unakuwa na kiwanja kimoja cha ndege kinachoweza kuhudumia ndege muda wote bila kujali majira ya mwaka na pia kila kanda inakuwa na kiwanja cha ndege kikubwa kimoja kinachoweza kuhudumia ndege zenye ukubwa unaohitaji viwanja vikubwa. Viwanja hivi vya kikanda vitasaidia pia kuleta mashirika ya ndege ya kimataifa ambayo yatafanya biashara ya

kubeba mizigo na abiria kutokamaeneo mbalimbali ya nchi yetu kwenda nchi za nje.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafuatilia kwa umakini gharama za usafirishaji wa anga na hasa bei za mafuta ya ndege, kwa nia ya kuangalia jinsi ya kuzifanyia marekebisho yenye lengo la kushusha gharama za uendeshaji na kuleta unafuu kwa abiria.

### 3.1.19. HUDUMA ZA SIMU, NUKUSHI (FAX), POSTA, NA MTANDAO (INTERNET)

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA ni moja ya miundo mbinu muhimu katika mkakati wa kukuza uchumi katika karne ya 21. Teknolojia hii imepunguza sana gharama za mawasiliano na inaongeza tija katika uzalishaji na utoaji huduma katika sekta zote. Matumizi ya mtandao wa kompyuta kupitia Internet yameleta mapinduzi katika sekta ya elimu, huduma za afya na burudani za aina mbalimbali. Teknolojia ya simu za mkononi imeongeza utumiaji wa huduma za simu. Hata hivyo hapa kuna tatizo la bei kubwa mno zinazotozwa na makampuni ya simu kwa wateja. Pamoja na gharama za mawasiliano ya simu kuwa juu, bado Watanzania walio wengi wanatumia muda mwingi kuwasiliana kwa njia hiyo na hivyo kuwapunguzia uwezo wa kutumia fedha zao katika maeneo mengine.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya Mawasiliano ya simu, Fax, Posta na Intaneti**

- Mtazamo wa kuona kuwa huduma za mawasiliano ni anasa tu unasababisha mamlaka ya usimamizi wa mawasiliano (TCRA) usijali sana malalamiko ya wateja kuhusu gharama kubwa na huduma mbovu za mawasiliano kutoka katika makampuni yanayoendesha biashara hiyo.

- Mfumo wa siasa za Ujamaa zilizotufungia katika kijichumba kisicho na madirisha ya kuona mambo ya maana na maendeleo yanayofanyika katika maeneo mengine ya dunia, ni jamabo lililotuchelewesha sana Watanzania katika sekta ya mawasiliano.

- Kampuni ya simu Tanzania (TTCL) hadi leo inaendeshwa zaidi kisiasa kuliko kitaalamu pamoja na kwamba kampuni hii ilikuwa ni moja ya makampuni machache sana ya umma nchini yaliyokuwa yanajiendesha kwa faida. Wakati menejiment ya TTCL inabinafsishwa kwa mara ya kwanza kampuni ilikuwa na akiba ya mabilioni benki. Hata hivyo kwa sababu ambazo hazijawekwa wazi viongozi wa Serikali ya CCM walilazimisha kampuni hiyo ibinafsishwe.

- Gharama za mawasiliano ya simu nchini, bila kujali kuwa ni simu za kawaida au za mkononi, ziko juu kupita kiasi. Kwa wastani bei zinazotozwa na makampuni ya simu yalioyoko nchini ni mara tisa zaidi ya bei zinazotozwa na makampuni yanayotoa huduma hizo katika maeneo mengine duniani, na hasa yale yaliyoko katika nje ya bara la Afrika. Kuna mgongano mkubwa wa kimaslahi kwa sababu baadhi ya viongozi wa umma wanaoshiriki vikao vya kupanga viwango vya malipo ya gharama za simu nchini, wakati huohuo ni wajumbe wa bodi katika baadhi ya makampuni hayo ya simu nchini.

- Serikali ya CCM imeshindwa kuelewa kuwa uchumi wa kisasa unatumia kompyuta na mtandao (internet), na kuwa ili wananchi weweze kushiriki kikamilifu katika uchumi wa aina hii ni lazima kuwe na juhui za makusudi kabisa kuwafikishia huduma hii muhimu, pamoja na kufanya maandalizi ya kimfumo katika sekta ya elimu ili wanafunzi na walimu weweze kuingia moja kwa moja katika matumizi ya teknolojia hii. Aidha kutokana na ujuzi mdogo, Watanzania walio wengi hawajaweza kutumia teknolojia hii ya

mawasionao (hata simu za mkononi) kwa kiwango cha juu kabisa. Watanzania walio wengi matumizi yao ya simu huishia katika kupiga, kutuma ujumbe mfupi, kupokea, na kutumia mitandao ya kijamii basi. Simu za mkononi, hususan simu janja, zimesheni viwezeshi (applications) mbalimbali vinavyoweza kusaidia kuratibu shughuli mbalimbali za kila siku za mtumiaji wa simu.

**Mpango wa CUF katika kuboresha matumizi ya huduma za simu, Fax, Posta, na intaneti**

Serikali ya CUF pamoja na mambo mengine itachukua hatua makhsusi kuhakikisha kuwa huduma za simu, fax, na mtandao wa intaneti zinasambaa kwa haraka na kufika kote nchini.

**Gharama za mawasiliano**

Serikali ya CUF itahakikisha kuwa gharama za mawasiliano zinashuka ili kuwiana na gharama zinazotumika katika mataifa mengine.

**Kuwakaribisha wawekezaji zaidi**

Serikali itakaribisha makampuni zaidi ya ndani na nje kuwekeza kwenye sekta hii na yale yatakayowekeza vijijini yatapewa motisha maalum.

**Matumizi ya kodi**

Kwa muda wa miaka kumi ijayo, kodi yote ya mauzo inayotozwa na serikali kwa watumiaji wa simu, fax, na intaneti itarejeshwa tena kuwekezwa kwenye upanuzi wa huduma za mawasiliano haya vijijini.

**Kujifunza kwa wenzetu**

Pamoja na jitihada nyingine, serikali pia itachukua hatua za kujifunza na kuiga kutokana na uzoefu walioupata wenzetu wa nchi mbalimbali, hususani Bangladesh na kampuni yao ya GrameenPhone, juu ya

usambazaji wa huduma ya simu kwa malengo ya kupiga vita umasikini vijijini.

**Huduma ya mtandao (internet)**

Katika kipindi cha miaka 10 serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itasambaza mkonga wa broadband kufika katika kila makao makuu ya wilaya. Lengo hili litasaidia sana kupunguza gharama za mawasiliano. Aidha njia ya mkonga huu pia itatumiwa na TANESCO katika usambazaji wa umeme kwa haraka.

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF pia itafanya mazungumzo na makampuni yanayosambaza huduma za internet nchini ili makampuni hayo yasambaze huduma hizo hadi kwenye shule za msingi na sekondari, na vyuo kwa gharama nafuu. Gharama hizi zitakuwa zinafidiwa na serikali kama punguzo la kodi yake kwa serikali.

### 3.1.20. HUDUMA ZA UZALISHAJI MALI

**NISHATI**

Hatuwezi kuzungumizia uchumi wa kisasa iwapo hakuna nia ya kushughulikia suasla la nishati na maji. Hii ni kutokana na ukweli kwamba uchumi wowote wa kisasa unaonishwa na matumizi ya hali ya juu ya mashine - iwe ni mitambo ya viwandani, matrekta ya mashambani au vyombo vya usafirishaji na kadhalika. Vyombo vyote hivi hutegemea nishati na maji kujiendesha. Hivyo basi ili uweze kupata ufanisi wa juu kutoka kwenye mashine ni sharti kwanza kuwepo na uwekezaji wa kiasi cha kutosha kwenye sekta ya nishati na maji ili kuhakikisha kuwa siyo tu kuwa vitu hivi ninapatikana, bali vinapatikana kwa bei ya kuridhisha. Hata hivyo Tanzania ni nchi ambayo imeonyesha udhaifu mkubwa sana katika sekta za nishati na maji.

**UMEME**

Umeme ambao ndiyo nishati kuu kwa matumizi ya mitambo viwandani na ambayo pia inapaswa kuwepo majumbani ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa lengo la kulinda mazingira, unazalishwa kwa kiwango kidogo, unasambazwa kwa ufanisi mdogo na bei yake ni kubwa sana.

Uzalishaji umeme nchini Tanzania kwa asilimia 90% unategemea maji ya mvua. Hili lisingekuwa ni tatizo sana kama hifadhi ya maji haya kwenye mabwawa ya kuzalishia umeme ingekuwa ni ya uhakika. Kwa bahati mbaya sana uhakika huo haupo. Ukiondoa maji,**TANESCO** pia huzalisha umeme kwa kutumia mafuta ya dizeli na hivi karibuni gesi ya Songosongo na Mnazi Bay. Kutokana na uzalishaji mdogo TANESCO imejikuta ikilazimika kuingia mikataba ya gharama kubwa na makampuni binafsi ya kufufua umeme. Makampuni haya ni pamoja na IPTL, AGRECO, na SIMBION POWER. Mikataba hii siyo tu kwamba haijasaidia kuondoa tatizo la umeme, lakini pia imekuwa ni mzigo mkubwa kwa watumiaji, huku serikali ikipoteza mabilioni ya shilingi kutokana na ufisadi uliofanywa wakati wa kuandaa mikataba hiyo**.**

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya umeme nchini**

Bila shaka makucha ya UFISADI ambayo yamejikita kila mahala chini ya serikali ya CCM, hadi kuteketeza takribani kila nyanja ya maisha ya Mtanzania yanaiparua na **TANESCO** pia. Hali ilivyo TANESCO ni kama ifuatavyo:

- **GRID YA TAIFA** (Mfumo wa upokeaji na usambazaji umeme) imeoza. Kuoza huku kunapelekea umeme ukatike hovyo bila mpangilio. Hali hii haikupaswa kuwepo kwa sababu kila lita ya mafuta ya petroli na dizeli inayouzwa, ndani yake kuna fungu linaloelekezwa kwenye mfuko wa nishati. Hiki ni kielelezo cha dhahiri kabisa kuwa pamoja na kwamba kunawezekana kukawa na ubadhirifu mkubwa ndani ya shirika hilo, lakini pia fedha za

mfuko wa nishati zimekuwa zikitafunwa kwa miaka mingi bila kufanyia kazi iliyokusudiwa.

- Uchambuzi unaonyesha kuwa pamoja na **TANESCO** kuwa na matatizo mengi tangu wakati ikiwa chini ya menejiment ya umma, matatizo hayo yaliongezeka kwa kiasi kikubwa baada ya menejimenti hiyo kufukuzwa na nafasi yake ikachukuliwa na menejiment ya kigeni. Pamoja na kwamba baadaye shirika hilo liliwekwa tena chini ya menejimenti ya wataalam wa ndani, hadi sasa hakuna jipya zaidi ya gharama za umeme kuongezeka kukiambatana na kuongezeka kwa kukatika hovyo kwa umeme.

- Pamoja na matumizi ya mita za LUKU kuwepo nchini kwa muda mrefu sasa, inashangaza kuwa TANESCO hadi imeshindwa kufikisha huduma hiyo kwa watumiaji wote. Mita za LUKU zingesaidia sana kupunguza malalamiko ya TANESCO ya muda mrefu kuwa baadhi ya wateja wake, hususan idara na taasisi za serikali, wamekuwa wakiliiingizia shirika hili hasara kwa kuwa na malimbikizo ya bili ya muda mrefu. Aidha, mita za LUKU kwa upande mwingine zingepunguza malalamiko ya wateja ambao bado wanatumia mita za kizamani kuwa bili wanazoletewa na **TANESCO** ni kubwa mno na kuwa haziakisi matumizi halisi ya umeme.

- Gharama za kuunganishiwa umeme zimeendelea kuwa ghali. Kwa sababu hii wananchi wengi, hata walioko katika maeneo ambayo nguzo zimebahatika kupita karibu na makazi yao wanaishia kuzitizama tu.

- Tatizo la kukatikakatika kwa umeme limekuwa halina tiba tena. Wananchi wengi wanapata hasara kubwa baada ya umeme unaokatika kurudi kwa nguvu na kuunguza vifaa vyao muhimu, huku utaratibu wa kuwafidia hasara hizo ukiwa haueleweki. Kwa hakika hali hii inarudisha nyuma maendeleo yao.

- Viwanda na sehemu nyingi za uzalishaji hazifanyi kazi kwa ufanisi kutokana na ukatikaji wa umeme wa mara kwa mara. Wamiliki wa maeneo ya uzalishaji wamekuwa wakipata hasara kubwa kwa kulazimika kutumia mashine za kufufua umeme zinazoendeshwa kwa dizeli au petroli. Hali hii inakatisha tamaa na kuleta athari hasi katika uchumi wa nchi.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

- **Menejimenti mpya kwa TANESCO**

Serikali ya umpja wa kitaifa chini ya CUF italiimarisha shirika la TANESCO kwa kuteua menejimenti ya wataalam wenye uzoefu katika shughuli za umeme na kuwapa mkataba wenye malengo yanayopimika (management performance contract). Sanjari na uboreshaji wa Menejimenti, ili kuleta tija na ufanisi, serikali kwa kuzngatia uzoefu na mafanikio yaliyopatikana kwa nchi zingine itaunda utaratibu wa kuwa na mgawanyo wa makampuni yatakayosimamia Nishati ya Umeme kama ifuatavyo:

i. Kuwepo kwa kampuni inayoshughulikia uzalishaji pekee (electricity power generation);
ii. Kuwepo na kampuni ya kushughulikia usambazaji (electricity power transmission); na
iii. Kuwepo kampuni nyingine ya kushughulikia masoko na mauzo ya nishati ya umeme (electricity power distribution).

- **Uanzishaji wa vyanzo vipya vya umeme**

Pamoja na serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF kuendelea na mpango wa kutumia gesi ya Songsongo, Mnazi Bay na maeneo mengine kufua nishati ya umeme, serikali pia itatafuta wawekezaji watakaowekeza kwenye ujenzi wa vinu vya kuzalisha umeme kutokana na vyanzo vingine, hususan kwa kutumia malighafi ya makaa ya mawe

kutoka katika mgodi wa Kiwira na migodi mingine. Tathmini ya kina itafanywa kuzingatia gharama na athari ya ajali mbaya na uchafuzi wa mazingira kabla ya kuamua kutumia madini ya uranium kuzalisha umeme. Hili ni muhimu ili kutuhakikishia kuendelea kupata umeme wa kutosha hata kama kutakuwa na tishio la ukame litakaloathiri uzalishaji wa umeme wa maji.

- **Nishati ya jua na upepo**

Serikali itafuta ushuru wote kwenye vifaa vinavyotumika kuzalisha umeme kutokana na nishati ya jua na upepo, ili kuharakisha usambaji wa umeme katika maeneo ya vijijini. Hali ilivyo kwa sasa ni kwamba vifaa vya kuzalisha umeme kwa kutumia jua na upepo ni ghali na Watanzania wengi, hususan wale wa vijijini, hawana uwezo wa kumudu gharama hizo.

**BIDHAA ZA PETROLI**

Baada ya mchakato wa ubinafsishaji wa biashara ya mafuta ya petrol, makampuni mengi binafsi yamejitokeza kushiriki katika kufanya biashara ya bidhaa za petroli. Katika hali ya kawaida ingetarajiwa kuwa ushindani baina ya makampuni haya ungepelekea kushuka kwa bei za bidhaa za petroli na hivyo kuwa wa manufaa kwa wateja. Hali kadhalika ingetarajiwa kuwa Serikali ingenufaika zaidi kwa kuwa na idadi kubwa zaidi ya walipa kodi katika sekta hiyo. Hata hivyo hali halisi ni tofauti kabisa kwani badala ya manufaa yaliyotarajiwa sekta hiyo imevurugika. Siyo tu kwamba bei ya bidhaa za petroli imeongezeka kwa kiasi kikubwa, lakini pia imekuwa ikibadilika mara kwa mara hata kama huko katika soko la dunia la bidhaa hiyo hali imetulia.

Moja ya sababu zinazochangia sana magendo na ukwepaji kodi katika biashara ya mafuta nchini ni bei kubwa ya bidhaa za pertroli. Sababu nyingine ni usimamizi dhaifu kwa mafuta yanayoorodheshwa kuwa ni ya kusafirishwa kwenda nchi jirani. Kwa kutumia ujanja ujanja na rushwa

sehemu ya mafuta haya imekuwa ikiuzwa nchini bila kulipiwa kodi. Bei kubwa katika biadhaa za petroli ni zao la utitiri wa kodi unaotozwa na serikali kwenye bidhaa hizo.

**Hali ilivyo kwa sasa**

- **Viwango vya kodi**

Viwango vikubwa vya kodi vinavyotozwa kwenye bidhaa za petroli ni mzigo mzito kwa Watanzania na kwani hupelekea bei ya bidhaa hizo kuwa juu na kusababisha ongezeko la gharama za uzalishaji wa bidhaa za viwandani pamoja na gharama za usafirishaji wa bidhaa kutoka sehemu moja hadi nyingine.

- **Tatizo la Uchakachuaji wa Mafuta**

Katika jitihada ya kutengeneza faida ya ziada, kumekuwa na tabia mbaya ya kuchakachua mafuta. Tatizo hili kwa kweli limekuwa kubwa na hadi sasa mamlaka ya kusimamia Nishati na Maji (EWURA) imekosa ufumbuzi wa kudumu.

- **Kushindwa kukuza uchumi na kushuka kwa thamani ya shilingi**

Kushindwa kuendesha uchumi wa nchi vizuri na kuendelea kuporomoka kwa thamani ya shilingi kila kukicha, kumetokana na mchango mkubwa wa kupandisha mara kwa mara bei ya mafuta yanayonunuliwa na Tanzania kwenye masoko ya Dunia. Kati ya mwaka 1995 na mwaka 2019 shilingi ya Tanzania imepoteza thamani yake dhidi ya dola ya kimarekeni kwa asilimia 317.40. (317.4%). Wakati mwaka 1995 dola moja ya Kimarekani ilikuwa inanunua shilingi 575 za Kitanzania, mwaka 2019 dola hiyo hiyo moja ya Kimarekani ilikuwa inanunua shilingi 2,400 za Kitanzania.

Ubinafsihaji holela wa sekta ya bidhaa za petroli umerutubisha rushwa katika sekta hiyo na kuchochea kuongezeka kwa magendo ya bidhaa hizo kwa kiwango cha kutisha. Serkali haikuwa makini wakati wa kusajili kampuni mpya za mafuta na kuzipa leseni za kufanya biashara hiyo. Nyingi ya kampuni hizi hazina sifa zinazostahili kwa kampuni ya mafuta kuwa nazo kwa sababu:

- Nyingi ya kampuni hizi mpya hazina maghala ya hifadhi. Katika biashara ya mafuta kampuni ambayo haina maghala ya kuhifadhia mafuta inayoyapokea kabla ya kuyasambaza inakuwa ni vigumu kwa serikali kufuatalia kodi zake. Sababu ni kwamba kisheria maghala haya yanakuwa chini ya uangalizi wa kudumu wa serikali na muda wote wanakuwepo maafisa wa ushuru wa forodha kukagua mali inayoingia na kutoka. Halijulikani ni vipi serikali ilitarajia kukusanya kodi zake kwa baadhi ya kampuni hizi mpya, ilihali ilijua fika kwamba hazikuwa na maghala ya hifadhi.

- Ukwepaji mkubwa wa kodi unaofanywa na baadhi ya kampuni hizi mpya umesababisha mauzo ya makampuni mkubwa yaliyokuwepo tangu zamani kushuka na hivyo basi kupungua kwa kiasi cha kodi ambacho serikali imekuwa ikikusanya katika sekta hii. Hata hivyo kuna taarifa kuwa kuna baadhi ya vigogo serikalini wanahisa kwenye baadhi ya kampuni hizi mpya na huenda hicho ndicho kilichokuwa kichocheo cha kukiuka taratibu.

- Nyingi ya hizi kampuni mpya zinafanya shughuli zake katika mazingira ya hatari. Biashara ya mafuta inahitaji uangalifu wa hali ya juu. Ni biashara ambayo inaweza kuzua janga kubwa na kuleta madhara makubwa kwa maisha ya watu na mali zao. Kwa kawaida makampuni ya mafuta yanatumia fedha nyingi kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na makandarasi wao juu ya kuchunga usalama. Aidha hutumia fedha nyingi kuweka miundombinu ya kinga dhidi ya majanga ya moto. Kwa kuwa nyingi ya kampuni hizi mpya

huingiza mafuta kwa njia ya barabara kutokea nchi jirani, na hazina sehemu maalumu za hifadhi, ni jambo la kawaida kukuta magari yaliyobeba shehena ya mafuta yakiwa yameegeshwa sehemu mbalimbali katikati ya makazi ya watu. Hali kadhalika, hata makampuni yaliyoweka vituo vya kuuzia mafuta vya rejareja, vituo hivi mara nyingi vinakuwa havikujengwa kukidhi viwango vya usalama vinavyotakiwa.

**MKAKATI WA CUF KUBORESHA SEKTA YA BIDHAA ZA PETROLI**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF pamoja na mambo mengine itachukua hatua zifuatazo ili kuleta marekebisho yanayotakiwa katika sekta hii muhimu:

**Makampuni yatakayofanya biashara ya mafuta nchini**

Serikali itaangalia upya usajili wa makampuni ya mafuta na yatakayoruhusiwa ni yale tu yatakayotimiza masharti ya kuwa na maghala ya hifadhi yaliyojengwa kwa kuzingatia viwango vya usalama vinavyokubalika. Na pili serikali itahakikisha kuwa mafuta yote yanayoingiazwa nchini kwa ajili ya biashara yatakuja kwa njia ya baharini, ila tu katika vyakati za dharura.

**Mafuta yanayosafirishwa nje ya nchi kupitia Tanzania**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanya mazungumzo na majirani zetu wanaopitishia mafuta yao nchini kwetu ili kwa pamoja tukubaliane juu ya suala la kutia rangi mbalimbali kwenye mafuta na mgawanyo wa rangi hizo kwa kila nchi. Mathalani, Tanzania pink na njano, Uganda kijani na bluu, Rwanda zambarau na hudhurungi nakadharika. Kwa utaratibu huu mafuta yoyote yaliyoorodheshwa kuwa yanasafirishwa nje kasha yakauzwa nchini kwa magendo bla kulipiwa kodi yatagululika kwa urahisi na wahusika kudhibitiwa. Utaratibu wa sasa wa kutumia

BIOMARKER unakwepeka kirahisi kwa kuwa unahitaji utafiti wa kimaabara kutambua mafuta ya magendo.

- Pamoja na utaratubu wa kutia rangi serikali pia itaweka sheria inayowalazimisha wasafirishaji wote wa mafuta ya nchi jirani kutia sahihi dhamana inayolingana na kodi yote ambayo serikali ingelipwa iwapo mafuta haya yangeuzwa nchini. Dhamana hiyo itafutika mara moja baada ya serikali kuthibitisha kwamba mafuta hayo tayari yamevuka mpaka na kuingia kwenye nchi yalikokusudiwa.

**Suala la bei ya mafuta**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itazipitia upya kodi zinazotozwa kwenye bidhaa za petroli na kuzirekebisha ili kushusha bei ya nishati hii muhimu. Marekebisho haya yatalenga kuzifanya bei za bidhaa za petrol zinazouzwa nchini ziwe katika uwioano mzuri na bei ya bidhaa hizo katika nchi za jirani, ili pamoja na kuwaletea wananchi unafuu, pia tuwe na silaha nyingine ya kupigia vita ukwepaji kodi na biashara ya magendo ya mafuta katika mipaka yetu.

Aidha serikali itahakikisha kunakuwa na udhibiti wa juu wa mafuta ili kuwabana wafanyabiashara wote wanaoingiza mafuta yaliyo chini ya viwango au yaliyochakachuliwa.

**MAJI NA MAZINGIRA**

Hali ya maji nchini kwa ajili ya matumizi ya viwandani na majumbani ni mbaya sana. Hali hii ni ya kushangaza sana ikizingatiwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo Mwenyezi Mungu amezijaalia sana wingi wa maji, kwani zaidi ya asilimia 6 ya eneo lote la nchi yetu ni maji. Tukumbuke kuwa sehemu kubwa ya maziwa makuu matatu yaliyoko kaitka bara la Afrika yaani Victoria, Tanganyika na Nyasa, iko Tanzania na pia zaidi ya maziwa haya matatu, nchi yetu pia imejaaliwa maziwa

mengine madogo madogo na mito mikubwa na midogo kwa mamia. Aidha Tanzania iko katika ukanda wa dunia ambapo mvua ni nyingi na kwa kiasi kikubwa ni za uhakika.

Tanzania ina bahati ya kuwa na maji ya kutosha kuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo ya uchumi na jamii. Hata hivyo rasilimali ya maji tuliyonayo haijatumiwa ipasavyo kutusaidia kukuza uchumi na kustawisha maisha ya Watanzania kwa ujumla wake. Tanzania ina mabonde tisa ya maji (water basins). Mabonde ya ziwa Victoria, ziwa Tanganyika, ziwa Nyasa, ziwa Rukwa, mto Ruvuma, mto Rufiji, mto Pangani, mito ya Ruvu na Wami, na bonde la ndani (internal drainage basin) la mikoa ya Arusha, Dodoma, Manyara, Singida na Shinyanga.

Mwaka 2006, Tanzania ilipata maji ya mvua ya wastani wa mita za ujazo 2467 kwa kila mtu. Kwa sababu ya ongezeko la watu, wastani wa maji ya mvua yanayoweza kutumiwa na kila mwananchi utapungua na kufikia mita za ujazo 1500 mwaka 2025. Nchi inahesabiwa kuwa na upungufu wa maji ikiwa inapata maji ya muva chini ya mita za ujazo 1000 kwa mtu mmoja. Hivi sasa Tanzania inatumia chini ya asilimia 1 ya maji ya mvua. Hatuna utaratibu mzuri na endelevu wa kuvuna na kuhifadhi maji. Nchi nzima ina mabwawa ya kuhifadhi maji 22. Mengi ni madogo madogo isipokuwa mabwawa yanayohifadhi maji ya kufua umeme kama vile Mtera na nyumba ya Mungu.

Ofisi tisa zinazosimamia mabonde ya maji (Basin Water Offices) hazina uwezo wa kuratibu na kupanga matumizi ya maji katika mabonde yao. ofisi hizi hazina wataalamu wa kutosha kuwezesha kupata taarifa ya haidrolojia ya mabonde yao, matumizi halisi ya maji na kuwa na mipango ya maendeo ya kuvuna na kuhifadhi maji. Kwa muda mrefu nchi imekosa utaratibu endelevu wa kulinda vyanzo vya maji katika mabonde yote, na badala yake serikali hukurupuka wakati maji yakipungua katika mabwawa ya kufa umeme na kuanza kuhamisha wafugaji na wakulima wanaofanya shughuli zao katika vyanzo vya maji.

Hata hivyo pamoja na utajiri huu wa maji, tumekuwa na udhaifu mkubwa katika kayaandaa maji hayo yawe tayari kwa matumizi. Huduma za usambazaji ni mbaya mno kiasi kwamba moja ya kero kubwa sana zinazowakabili wananchi wengi, bila kujali kuwa ni wa mijini au vijijini, ni uhaba wa maji. Haishangazi basi kuwa uchimbaji wa visima hata katikakati ya miji miaka hii imekuwa ni biashara kubwa. Viwanda, makampuni, na watu binafsi wote wanaponea kwenye maji ya chumvichumvi ya visima. Lakini tujiulize, ni mwekezaji gani wa hadhi atawekeza kiwanda muhimu nchini mwetu kwa kutegemea maji ya kisima? Hakuna shaka yoyote kuwa baada ya miaka 59 ya kujitawala suala la maji linatakiwa lianze kupewa umuhimu unaostahili kama kweli tuna nia ya kuboresha maisha ya Watanzania, na kuwavutia wawekezaji wa uhakika.

**Hali ya huduma ya maji ilivyo sasa**

- Serikali haijaona umuhimu wa kuwa na mipango ya kuhifadhi maji ya mvua. Kila mwaka mabilioni ya galoni yanapotelea baharini kupita katika mito yetu inayofurika wakati wa misimu ya mvua.

- Pamoja na kubinafsisha baadhi ya mamlaka za maji ubinafsishaji huo mpaka sasa haujaleta matunda yanayoonekana. Maji bado hayawafikii walengwa wengi kama ilivyotarijiwa na hata hao ambao kwa kiasi fulanI yanawafikia, maji wanayopata sio safi na salama. Wananchi bado wanalazimika kuingia gharama kuchemsha maji hayo au kuyatia dawa ya kuulia vijidudu.

- Maji ya visima yanayotumiwa na wananchi wengi siyo safi na salama kwani visima vingi ni vifupi na vimechimbwa katika maeneo yenye msongamano mkubwa wa makaazi. Kutokana na kuwepo kwa miundo mbinu chakavu ya maji taka au kutokuwepo kabisa kwa miundo mbunu hiyo maji mengi ya visima hivi

yanachanganyika na vinyesi, hasa wakati wa misimu yamvu. Moja ya sababu zilizopelekea kipundupindu kuwa ugonjwa wa kudumu hapa nchini ni matumizi ya maji ya visima hivi kabla ya kutibiwa ipasavyo. Utafiti unaonyesha kuwa asilimia zaidi ya kumi ya magonjwa yote wanayoyapata wanaadamu yanatokana na matumizi ya ya muda mrefu ya maji yasiyo salama.

**MKAKATI WA CUF KUBORESHA HUDUMA YA MAJI KWA MAENDELEO YA TAIFA**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF italichukulia suala la usambazaji wa maji kuwa ni miongoni mwa majukumu ya msingi na ya kpekee ambayo yatashughulikiwa kwa haraka. Pamoja na mambo mengine serikali itachukua hatua zifuatazo:

- Itaimarisha ofisi za mabonde ya maji ili ziweze kupata taarifa ya haidrolojia ya mabonde yao, ziandae mipango endelevu ya matumizi ya maji itakayozingatia matumizi ya maji ya binadamu na mifugo, shuguhuli za viwandani, kufua umeme, kulimo cha umwagiliaji na ulinzi wa mazingira kuzuia ukaukaji wa maji unaosababishwa na binadamu na mfugo yake.

- Itatekeleza mipango endelevu ya ujenzi wa mabwawa ya kuvuna na kuhifadhi maji.

- Itawahamasisha na kusaidiana na wanakijiji kuwa na miradi midogo midogo ya kuvuna maji.

- Itafungua mabonde ya chini (down stream basin) kwa kilimo cha umwagiliaji maji baada ya maji ya bonde kutumiwa katika kufua umeme. Kwa mfano kuna hekta zaidi ya milioni 1 zinazoweza kutumiwa kwa kilimo katika bodne la chini la mto Rufiji.

- Huduma za usambazaji maji zitabinafsishwa na kupewa kampuni zenye uwezo, utaalamu na uzoefu wa kutoa huduma bora kwa wananchi.

- Pamoja na kwamba nia ni kubinafsisha sekta ya maji, bado tuna wajibu mkubwa wa kuwaandaa vijana wetu kufuzu kuchukua nafasi za ajira zitakazojitokeza kwenye makampuni binafsi ya uzalishaji na usambazaji wa maji. Pamoja na mambo mengine serikali itakiimarisha zaidi chuo cha maji cha Rwegarulila na kuanza kuchukua hatua za kukipandisha hadhi kuwa chuo kikuu kishiriki chini ya chuo kikuu cha Dar es salaam ambacho kitatoa wataalam wa viwango vya juu ambao wataisadia sekta ya maji kufikia malengo yake.

### 3.1.21. ELIMU

Kukua kwa uchumi wa kisasa wenye uwezo wa kuboresha maisha ya wananchi kunategemea wafanyakazi wenye ujuzi na maarifa. Kwa hakika utafiti unaonyesha kuwa kukua kwa uchumi wa taifa lolote kunashabihiana kwa karibu na kiwango cha kuwekeza katika sekta ya elimu. Hivi sasa dunia inashuhudia mapinduzi ya teknolojia ya habari na mawasilano (TEHAMA) ambayo yanaleta mageuzi makubwa ya uchumi na biashara ya kimataifa. Ni dhahiri hatutuweza kushindana kiuchumi na kibiashara katika ulimwengu tulionao leo iwapo hatutachukua hata za makusudi kuhakikisha kuwa watu wetu wengi na hasa wanafunzi na vijana wote wanapata fursa kujifunza taaluma hii.

**Elimu ya Awali**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itawahamasisha wananchi - ikiwa ni pamoja na watu binafsi, taasisi za kidini na mashirika yasiyo ya kiserikali kuwekeza kwenye Nyanja hii chini ya utaratibu ufuatao:

- Serikali itashuhulika na kuweka viwango vinavyotakiwa na usajili.

- Serikali itawasaidia wananchi wenye nia ya kuanzisha shule za awali kwa kuwapatia viwanja vinavyotosheleza mahitaji kwa ajili ya kuzingatia viwango wakati wa ujenzi.

- Kwa kuwa hivi sasa hakuna utaratibu wa kuwaandaa walimu wa shule za awali kwenye vyuo vyetu, serikali itauanzisha ili watakaowekeza kwenye shule za awali wasiwe na shina ya kupata walimu wenye sifa.

- Shule za awali hazitatozwa kodi.

**Elimu ya msingi**

Pamoja na kwamba Elimu yetu kwa ujumla imeendelea kukumbwa na matatizo mengi, lakini hali ni afadhali kidogo hivi sasa kuliko ilivyokuwa miaka ya 2000.

Katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2000 CUF ililivalia njuga tatizo hili na kuifanya CCM ije juu na kudai kuwa CUF ilikuwa inasema uongo. Hata hivyo pamoja na kuja juu, baada ya chama hicho kurudi madarakani kilizikubali hoja za CUF, ikiwemo ya kufuta ada na michango yote shuleni, na kuanzisha opereshini kubwa ya kupunguza idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule ambao walikuwa mitaani. Miaka mitano (5) iliyopita CCM imetumia Kauli ya " ***Elimu Bure***" kama Turufu kwa wananchi, ingawa huu ni Msimamo wa CUF wa miaka 20 iliyopita.

Pamoja na mafanikio haya kiasi yaliyokwisha patikana, sehemu kubwa ya watoto ambao wako shuleni wanasoma katika mazingira magumu yenye matatizo makubwa matatu, ambayo ni msongamano kwenye madarasa, njaa, na uhaba mkubwa wa waalimu na vifaa vya kufundishia. Kutokana na matatizo haya na mengine, uwezo wa darasani wa wanafunzi umeendelea kuwa wa chini.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya elimu nchini**

**Ukosefu wa mipango ya kisera tangu mwaka 1961**

Pamekuwepo utamaduni wa kutokuchukua hatua muafaka kwa wakati muafaka katika kukabiliana na changamoto nyingi zinazoikabili sekta hii ya elimu nichini. Ukosefu wa mipango ya kisera tangu awali imesababisha hivi sasa Taifa kujikuta likihitaji kufanya marekebisho makubwa katika elimu ya msingi, ili kurejesha hali ya kawaida katika ngazi hiyo ya elimu.

**Ubora wa kiwango cha Elimu**

Bado kiwango cha ubora wa elimu ya msingi inayotolewa nchini ni cha chini mno. Kwa wastani kila mwaka, zaidi ya nusu ya wanafunzi wote hawapati alama za kufaulu.

**Watoto wenye njaa ni vigumu kufundishika**

Tangu mwaka 2000 na kurejea tena mwaka 2005 na 2010, Chama cha CUF kimekuwa mstari wa mbele kusisitiza kuwa lazima uwepo utaratibu wa kuhakikisha kuwa watoto mashuleni wanapatiwa walau mlo mmoja kwa siku. Uzoefu unaonyesha wazi kuwa mtoto mwenye njaa ni vigumu kufundishika. Lakini suala hili halikupewa umauhimu unaostahiki kutokana na ama kutofahamu au kutokuwa na dhamira ya dhati katika kupambana na adui ujinga, maradhi na umasikini, na kumkomboa mtoto wa Tanzania kielimu. Wilaya zote zilizojaribu zimeshindwa kuendelea na kutoa chakula kwa wananfunzi kutokana na njaa kubwa inayolikabili Taifa kila kukicha na maeneo mengine utaratibu huo umekuwa kero kubwa kwa wazazi/walezi wa watoto wasio na uwezo wa kumudu kuchangia madebe ya nafaka mashuleni.

**Kazi ya ualimu ni kazi ya kitaalamu**

Mbali ya mwalimu kufundisha darasa zima katika ujumla wake, anatakiwa pia kumfuatilia kwa karibu mwanafunzi mmoja mmoja ili aweze kutoa msaada wa ziada kwa wale wenye kasi ndogo ya kujifunza (slow learners). Maslahi duni kwa walimu yamesababisha walimu wengi walazimike kujikita zaidi katika kuhangaikia kujikimu kuliko kzingatia kanuni za ufundishaji. Pia mishahara midogo na malimbikizo ya posho na stahiki nyingine kwa muda mrefu, ni hali inayowakwaza walimu kwa kiasi kikubwa , na kujikuta wakilazimika kuanzisha miradi midogo midogo ili kujikimu na ukata mkubwa. Kujiingiza katika biashara hizi kunawafanya wakose muda wa kutosha wa kufanya kazi yao kwa weledi.

**Elimu ya Awali**

Serikali haijawekeza kabisa kuhakikisha kuwa elimu ya awali inatolewa kwa watoto wate nchini. Kwa mfano, vyuo vya ualimu vya serikali havina utaratibu wa kuandaa walimu wa shule za awali na hivyo kusababisha walimu wengi wa shule zilizopo kutokuwa na taaluma ipasayo. Aidha serikali haitoi msaada wowote, mathalan wa viwanja vya ujenzi wa shule hizo, kwa wenye nia ya kuanzisha shule hizo, pamoja na kwamba inakataa kuzisajili nyingi ya shule zilizopo kwa kisingizio kuwa nyingi ziko katika majengo ya nyumba za kawaida za kuishi, na hivyo kutofikia viwango vinavyotakiwa.

**Lugha ya kufundishia shuleni**

Lugha ya kufundishia imekuwa ni tatizo kubwa sana. Vigogo wa CCM wanawapeleka watoto wao shule za msingi zinazofundisha kwa lugha ya Kiingireza huku Kiswahili kikiwa ni kama somo la kujitegemea. Watoto wa makabwela (mahohehahe) wanapelekwa katika shule zinazotumia Kiswahili kufundisha. Wakati haya yanatokea CCM wanajua kabisa kuwa mtoto yule anayepewa elimu ya msingi kwa kutumia Kiswahili atapaswa kupewa elimu kwa kutumia Kiingereza katika hatua zote za

elimu zinazofuata ikiwa ni sekondari, vyuo na vyuo vikuu. Wanachofanya ni kuwadanganya Watnzania kuwa wanakienzi Kiswahili huku wao wakiwaandaa watoto wao kukabiliana na elimu za ngazi zinazofuata bila matatizo.

Mtoto wa Mtanzania wa kawaida analazimika kuanza kujifunza upya Kiingereza ili aweze kujifunza masomo ya ngazi ya sekondari ambayo takriban yote yanatolewa kwa lugha ya Kiingereza. Katika mazingira haya kujifunza kwa kina (in depth learning) kunakosekana. Hii ndiyo sababu inayosababisha Taifa kuendelea kuzalisha wasomi wenye vyeti vya juu lakini kimsingi wakiwa na uelewa mdogo.

**Stahiki za waalimu**

Pamoja na kwamba kazi ya ualimu ni miongoni mwa kazi ngumu sana, ajira ya ualimu hapa Tanzania ni miongoni mwa ajira zinazodharauliwa na kutopewa umuhimu mkubwa na serikali. Vipato vya waalimu ni vya chini ukilinganisha na vipato vya wataalamu wa fani nyingine. Kwa mfano, mshahara wa mwalimu wa shule ya msingi ni sawa na posho ya siku moja ya kikao anayolipwa mbunge! Shule nyingi hazina makazi ya waalimu na hivyo kuwafanya waalimu kuishi mbali na shule na wakati mwingi katika nyumba ambazo hazina hadhi.

**Elimu kwa watoto wa kike (wasichana)**

Kuna imani kwamba ukimuelimisha mwanamke ndio umeielimisha jamii nzima, Imani hii inatokana na ukweli kuwa wanawake wana jukumu la msingi la kumaumbile la ulezi wa familia. Kuporomoka kwa maadili ya Taifa na ukosefu wa heshima na nidhamu, na kujiingiza katika vitendo hatarishi kama utumiaji wa madawa ya kulevya, uasherati, wizi, nakadhalika, kunatokana na kukosekana kwa kiasi kikubwa msingi wa awali wa malezi ya watoto. Watoto wa kike ndio walezi wa familia watarajiwa wenye nafasi ya kipekee katika familia. Kutokana na ugumu wa maisha wasichana walio wengi wamejikuta hawamalizi elimu ya

msingi na kuendelea na elimu ya juu kutokana na kupewa ujauzito na "MAFATAKI" wakiwa bado shuleni, na hivyo kushindwa kuendelea na masomo. Sera ya kuruhusu wasichana wanaopata mimba kuendelea na masomo bado ni suala lenye utata linalohitaji umakini na uchambuzi wa kina, kuangalia athari zinazoweza kujitokeza kutokana na hilo.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua zifuatazo kuhakikisha kuwa sekta ya elimu katika ngazi za msingi na chekechea inaboreshwa.

- **Asilimia 25 ya bajeti kila mwaka kutumika katika sekta ya Elimu**

Seikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itatumia si chini ya asilimia 25 ya bajeti yake kila mwaka kuboresha sekta ya elimu kwa ujumla. Asilimia 50 ya bajeti yote ya elimu itaelekezwa kwenye kupanua na kuboresha elimu ya msingi. Hili litasaidia kukamilisha marekebisho yanayotakiwa katika ngazi hii ya elimu katika muda wa miaka mitano.

- **Kuhamasisha ujenzi zaidi wa shule binafsi na kufuta kodi katika vifaa vya elimu**

Seikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanya juhudi kubwa kuhamasisha watu binafsi, mashirika ya dini na mengine yasiyokuwa ya serikali, na makampuni ya biashara kujenga shule zaidi za msingi. Ili wananchi walio wengi waweze kumudu gharama za kusomeshea watoto wao kwenye shule hizi serikali haitazitoza kodi yoyote na itatoa ruzuku kusaidia uendeshaji, huku ikidhibiti viwango vya karo. Aidha serikali itavifanyia marekebisho makubwa viwango vya kodi zote zinazotozwa kwenye vifaa vya elimu ili sekta ya elimu kwa ujumla inufaike na punguzo la gharama.

- **Marekebisho ya mitaala**

Serikali ya CUF itafanya marekebisho ya mitaala kwa kuzingatia zaidi umuhimu (relevance) wa maudhui, muda wa kila somo, uwezo wa wanafunzi, na faida ya somo lenyewe. Baadhi ya marekebisho ni haya yafuatayo:

i. Mitaala italenga kukuza lugha ya Kiingereza na hivyo kuwaongezea wanafunzi uwezo wa kumudu vizuri masomo ya sekondari.

ii. Shule zisizomilikiwa na srikali zitakuwa na uhuru wa kufundisha masomo ya ziada kama itakvyokubaliwa na bodi za shule zinazohusika.

iii. Itakuwa ni marufuku kwa wanafunzi wa shule za msingi kutumiwa kwa ajili ya maandamano ya aina yoyote zaidi ya yale yanayohusu siku ya mtoto duniani. Hii ina maana kwamba watoto wa shule za msingi hawatahusishwa na shughuli kama mbio za mwenge, mapokezi ya wanasiasa, au kutumika katika shughuli za kuwachezea ngoma na kuwatumbuiza wanasiasa hao.

iv. Itakuwa ni marufuku kwa wanafunzi kujihusisha na aina yoyote ile ya biashara kwenye maeneo ya shule.

- **Matumizi ya komputa mashuleni**

Seikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itajiunga na mpango wa kimataifa wenye lengo la kumpatia kila mwanafunzi kompyuta (laptop) moja ya bei nafuu. Hatua kwa hatua shule za msingi na sekondari zitaunganishwa na mtandao wa intaneti ili wanafunzi waanze mapema kutumia kompyuta na mtandao wa mawasiliano (internet) kwa ajili ya kujifunza.

- **Lishe kwa wanafunzi**

Utafiti unaonyesha kuwa watoto wenye njaa hawafundishiki, na huu ndio msimamo na mtazamo wa CUF siku zote. Seikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF kwa kushrikiana na halmashauri za wilaya na kmati za shule itahakikisha kwamba watoto wa shule za msingi wanapata walau mlo mmoja kamili wa chakula kikuu kinachopatikana katika eneo husika, wakati wanapokuwa shuleni.

- **Elimu itatolewa bure na kupiga marufuku michango ya aina zote**

Hili ni eneo ambalo limekuwa likilalamikiwa sana na wazazi. Michango ambayo haitabiriki imekuwa ni mingi na inavyoonekana siyo yote ambayo inachangishwa kwa nia njema. Seikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa huduma zote zinazotakiwa katika elimu ya msingi zinakuwa ni jukumu la serilali. Mzazi/Mlezi atapaswa kumnunulia mtoto wake nguo za shule na madaftari tu. Vitabu na vifaa vingine vitagharamiwa na serikali. Kamati za shule na mabaraza ya kata hayataruhusiwa kuirejesha michango ya aina yoyote ile kwa mlango wa nyuma. Chini ya serikali ya CUF mchango wowote ule utakuwa ni suala la hiyari la muhusika.

- **Huduma za ukaguzi**

Huduma za ukaguzi hivi sasa zimedorora kwa kiasi kikubwa. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itazihuisha huduma hizi na kuziimarisha. Kila shule ni lazima ikaguliwe angalau mara moja kwa muhula.

- **Mishahara na makazi ya walimu**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaongeza mishahara na posho za waalimu kama ilivyo kwa watumishi wote wa umma ili kukidhi mahitaji muhimu. Aidha, suala la makazi bora ya mwalimu litakuwa ni

jukumu la lazima kabisa kwa serikali. Serikali itaanzisha mradi mkubwa wa ujenzi wa nyumba za walimu na katika kipindi cha miaka 5 kila mwalimu atakuwa anaishi katika mazingira bora.

**ELIMU YA SEKONDARI**

Tanzania ni nchi iliyoachwa nyuma sana duniani katika maendeleo ya elimu ya sekondari. Chimbuko la Taifa letu kuwa nyuma mno katika elimu ya sekondari linaanzia katikati ya miaka ya sitini pale serikali ilipotangaza kuwa elimu ya darasani (formal education) haina maana sana, ati kwa kuwa ilikuwa inachukuwa miaka 20 hadi 30 mpaka matunda yake kuanza kuonekana, na kuwa ati taifa lisingeweza kusubiri, hivyo mkazo ungeelekezwa kwenye elimu ya watu wazima. Kutokana na msimamo huo athari zifuatazo zilijitokeza:

- Elimu haikuonekana tena kuwa ni haki kwa kila mtoto kujiendeleza hadi mwisho wa upeo wake.
- Dhana ya kufaulu kwa ajili ya kujiunga na masomo ya sekondari iliuawa na sehemu yake ikapandikizwa dhana ya kuchaguliwa.
- Watu na taasisi binafsi, hata waliokuwa na uwezo, walikatazwa kuwekeza kwenye elimu ya sekondari.
- Serikali haikujihangaisha kuwekeza katika mashule mapya ya sekondari ukiondoa mawili matatu ya mchepuo wa kilimo.
- Serikali ya awamu ya nne imejenga sekondari za kata bila maandalizi ya walimu wa kutosha na vifaa muhimu vya kufundishia kama vile maabara na maktaba.
- Hivi leo elimu ya sekondari imekuwa ghali mno kulingana na uwezo mdogo wa wananchi wengi walio masikini. Ijapokuwa CCM inajisifia kuwa imeondoa ada na michango katika shule za sekondari ukweli unabakia palepale kuwa maelfu ya watoto

wanashindwa kujiunga na sekondari kutokana na mzigo wa michango. Mathalani, ili mtoto ajiunge kidato cha kwanza anahitaji aende shule na vifaa au mchango wa dawati, mlinzi, jembe, panga, fyekeo, godoro, tahadhari nakadhalika, hivi vyote vinaleta gharama kubwa. Je, ni wazazi wangapi wanamudu elimu hii ambayo serikali ya CCM wanasema ni bure?

**Dira ya mabadiliko ya CUF**

Kama ilivyo kwa elimu ya msingi, elimu ya sekondari nayo inahitaji kupanuliwa na kuboreshwa. Ongezeko la bajeti ya elimu kwa ujumla litatupa uwezo wa kufanya marekebisho yanayohitajika. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itatumia si chini ya asilimia 25 ya bajeti ya elimu kuimarisha na kuboresha elimu ya sekondari. Pamoja na kusudio hili sserikali itachukua hata zifuatazo ili kuyafikia malengo haya:

- **Elimu ya sekondari bure**

Katika kuongeza nafasi za elimu ya sekondari kwa kila kijana wa Kitanzania, serikali itahakikisha kuwa ada na michango yote katika ngazi hiyo ya elimu vinafuatwa. Aidha, serikali itajenga shule mpya ili kuhakikisha kuwa nafasi za kutosha katika elimu ya sekondari zinapatikana. Hatua hizi zitatuhakikishia kuwa kila kijana aliyepata alama za kufaulu katika mtihani wa darasa la saba aanapata fursa ya kuendelea na masomo ya elimu ya sekondari, bila kikwazo chochote.

- **Kuhamasisha ujenzi wa shule binafsi**

Serikali itafanya juhudi kubwa kuwahamasisha watu binafsi, mashirika ya dini na mengine yasiyokuwa ya kiserikali, na makampuni ya biashara kujenga mashule zaidi ya sekondari. Aidha serikali itatoa kila aina ya msaada unaohitajika ili kufaniksiha lengo hili ikiwa ni pamoja na kuondoa vikwazo visivyo na sababu katika usajili wa shule binafsi. Ili

wananchi walio wengi waweze kumudu gharama za kuwasomesha watoto wao kwenye mashule haya serikali itatoa ruzuku maalum na pia hakutakuwa na kodi kwa shule.

- **Marekebisho ya mitaala**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanya marekebisho kwenye mitaala inayotumiwa na shule za sekondari ili pamoja na mambo mengine:

i. Kupunguza idadi kubwa ya masomo ya lazima ambayo kwa kiasi fulani yanachangia mwelekeo uliopo hivi sasa wa wanafunzi kusoma kwa ajili ya kufaulu mitahini badala ya kuwajengea uwezo wa kukuza uelewa.
ii. Kuingiza elimu zaidi ya vitendo kuliko nadharia.
iii. Kuingiza somo la kompyuta na matumizi ya mtandao wa internet.
iv. Kuhamasisha wanafunzi kujifunza masomo ya hisabati na sayansi.
v. Kuboresha somo la uraia ili kuwafanya vijana waijue katiba ya nchi,wajenge utamaduni wa kuthamini haki za binadamu na kuzitetea, pamoja na kuishi na kusimamia maadili mema.

- **Huduma za ukaguzi**

Kama ilivyo kwa shule za msingi, itakuwa ni lazima kwa shule za sekondari kukaguliwa angalau mara moja kwa muhula.

- **Maslahi ya walimu na makazi bora**

Mazingira ya kazi kwa waalimu wa shule za sekondari yataboreshwa sana ikiwa ni pamoja na kuwapa mishahara na posho zinazolingana na majukumu yao, na kuwapatia makazi bora. Katika kipindi cha miaka 5

kila mwalimu wa sekondari nchini atakuwa anaishi katika makazi bora ambayo yako karibu na mazingira ya shule.

**ELIMU YA JUU**

Elimu ya juu kwa taifa lolote ni muhimu kwa sababu inalenga katika kuwaandaa wataalamu mbalimbali kuja kukabidhiwa majukumu mbalimbali kwenye jamii. Kutokana na ukosefu wa mipango makini tangu awali katika kuboresha elimu kwa ujumla, hapa Tanzania idadi ya wataalamu wanaoandaliwa ni wachache ikilinganishwa na mahitaji halisi, lakini pia ubora wa maandalizi yao hauridhishi.

Waajiri wengi nchini, na hasa wale wa sekta binafsi wamekuwa na upendeleo wa wazi wa wahitimu walioandaliwa kwenye vyuo vya nje ya nchi kuliko wale walioandaliwa nchini. Ni dhahiri kabisa kuwa kwa hali tuliyonayo nchi yetu itakwama katika juhudi za kuboresha uchumi na kujiletea maendeleo iwapo hatua za dharura hazitachukuliwa mapema kuongeza idadi ya wataalamu tunaowaandaa, na pia kuboresha utoaji wa taaluma katika taasisi zetu za elimu ya juu.

**Hali halisi ilivyo sasa katika sekta ya elimu ya juu nchini**

- Tanzania pamoja na kwamba ndiyo nchi yenye idadi kubwa ya watu kuliko nchi zote za Afrika Mashariki, ndiyo ya mwisho kwa idadi ya wananchi wake wenye walau shahada ya kwanza.

- Kumekuwa na wimbi kubwa la wahadhiri katika taasisi zetu za elimu ya juu kuondoka na kwenda vyuo vya nchi zingine za kiafrika kutokana na maslahi duni wanayopata hapa nchini

- Katika taasisi zetu nyingi za elimu ya juu huduma za kitafiti zinalegalega kwa kiasi kikubwa kutokana na serikali kushindwa kutenga fedha kwa shughuli hiyo. Huduma hizi pale ambapo zipo kwa kiasi kikubwa zinafadhiliwa na wahisani wa nje ambao mara

nyingi wao wanaoamua ni aina gani ya utafiti wanataka ufanwe. Hali hii imesababisha Taifa kutonufaika kikamilifu na matokeo ya tafiti mbalimbali zinazofanyika kwenye taasisi hizi.

- Tanzaniaa haijafikia wakati wa kuhitaji wanafunzi wetu wanaosoma katika taasisi za juu za elimu kuchangia gharama. Serikali ya CCM imeulazimisha utaratibu huo kutumika bila kuzingatia mizani ya faida na hasara zake kwa jamii yetu.

- Kumekuwa na kulazimisha kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosoma katika taasisi za juu kusiko endana na uboreshaji wa huduma za msingi zinazohitajika. Matokeo yake ni kwamba mazingira ya wanafunzi wanaosoma miaka hii ni magumu kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma.

- Elimu ya juu imefanywa kama ni anasa na mzigo mkubwa kwa serikali. Wanafunzi wa elimu ya juu wananyanyasika sana kutokana na utaratibu wa utoaji mikopo. Mikopo iliyopo inatolewa kwa upendeleo na hamna uhakika wa waombaji kupata. Aidha gharama za mikopo hii ni kubwa mno na wanaobahatika kukopa hujikuta katika mazingira magumu sana ya kulipa baada kuhitimu na kupata ajira.

- Utoaji wa mikopo kwa kuzingatia maraja ya ufaulu, hauzingatii hali halisi ya mazingira ya elimu Tanzania. Kuna vijana wengi wenye uwezo mkubwa ambao kutokana na hali za wazazi wao wamejikuta wakisoma katika shule zenye mapungufu mengi kama uhaba wa waalimu nakadhalika. Hawa pamoja na uwezo wao mkubwa huishia kupata madaraja ya ufaulu ya chini (daraja la pili na tatu) na kujikuta wakiwa nje ya utaratibu wa kupewa mikopo. Wale watoto wa vigogo wanaosoma shule nzuri na zenye walimu wa kutosha ambako ni rahisi kufaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza ndio ambao CCM imewatengea mikopo.

- Sehemu kubwa ya gharama za posho wakati wa mafunzo kwa vitendo yanayoenda kufanywa na wananfunzi wa vyuo kikuu yanagharamiwa na mzazi na mwanafunzi peke yake. Serikali haioni umuhimu wa mafunzo haya na ina mchango kidogo sana katika kuwezesha mafunzo bora ya vitendo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

- Wanafunzi wa vyuo vikuu leo wanakabaliwa na uhaba mkubwa wa makazi ya kuishi. Serikali ya CCM imeliachia suala hili kuwa mikononi mwa wanafunzi na wazazi. Kinachotokea ni kuwa wanafunzi wengi wanishi kwenye baadhi ya nyumba duni za kupanga zilizoko katika maeneo ya mbali na vyuo vyao. Hali hii huwapawakati mgumu sana wanafunzi hawa na kuwafanya wawe na hisia mbaya kwa jamii.

- Kiwango cha mkopo wanachopewa wanafunzi kwa ajili ya kujikimu ni kidogo sana na hakitoshelezi kulipia gharama za msingi za kuishi. Hii inawaweka wanafunzi katika wakati mgumu sana na imesababisha baadhi ya wanafunzi hawa kujikuta wakijiingiza katika vitendo vya uhalifu na ukiukaji wa maadili.

- Kushindwa kuviunganisha vyuo vikuu ndani ya nchi na huduma ya intaneti ya uhakika pamoja na kuvipatia kompyuta za kutosha ni tatizo linaloathiri uharaka wa kujifunza unaoendana na karne ya sayansi na teknolojia.

**Dira ya mabadiliko ya CUF**

Pamoja na kwamba agenda ya CUF ni kutumia si chini ya asilimia 25% ya bajeti yoe ya elimu kuboresha elimu nchini, serikali pia itachukua hatua zifuatazo kuhakikisha kuwa malengo haya yanatimizwa:-

- **Ugharimiaji (uchangiaji) wa elimu ya juu**

CUF inaamini kuwa Tanznaia haijafikia wakati wa kuhitaji wanafunzi wa elimu ya juu kuchangia gharama. Serikali itaweka utaratibu utakaowawezesha vijana wote wenye sifa na waliochaguliwa kujiunga katika chuo kikuu chochote ndani ya nchi kupata elimu ya juu bila vikwazo. Seriklali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itagharamia mahitaji yote ya msingi ya mwanafunzi wa elimu ya juu bila MKOPO, ikiwa ni pamoja na kugharamia bima ya afya ya kila mwananafunzi. Uboreshaji wa eneo hili la elimu ya juu utafanyika hatua kwa hatua, kwa kuzingatia hali halisi ya ukuaji wa uchumi na mahitajio mengine ya Taifa.

- **Posho za kujikimu vyuoni na wakati wa mafunzo kwa vitendo**

Seriklali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa wanafunzi wa elimu ya juu wanapatiwa posho zinazokidhi mahitaji wanapokuwa vyuoni na wanapokuwa katika mafunzo kwa vitendo.

- **Matumizi ya TEHAMA katika kujifunza**

Seriklali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaandaa mfumo mzuri wa matumizi ya intaneti katika vyuo vikuu vyote vya serikali na kuhakikisha kuwa panakuwa kila mwanafunzi ana kompyuta mpakato yake ambayo muda wote akiwa ndani ya chuo imeunganishwa katika mfumo wa internet. Hali hii itawafanya wanafunzi wetu kujielimisha vizuri zaidi ili waendane na ushindani wa soko la taaluma na ajira kutoka nchi nyingine zilizoendelea duniani.

- **Makazi ya wanafunzi wa elimu ya juu**

Serikali ya CUF itahakikisha kuwa kila chuo kikuu cha umma kinakuwa na makazi thabiti yatakayotosheleza wanafunzi wote. Makampuni makubwa ya ujenzi yatapewa tenda za kujenga mabweni ya kisasa ya wanafunzi yaliyounganishwa na mtandao wa intaneti katika kila chuo.

Lengo la serikali litakuwa kuwezesha kila mwanafunzi apate makazi rafiki kwa usomaji.

- **Mzingira ya wahadhiri**

Seriklali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itazindua mpango maalumu wa makazi kwa wahadhiri na watumishi wengine waandamizi wa vyuo. Sanjari na hilo mishahara na marupurupu ya wahadhiri na watumishi wengine wa vyuo itaboreshwa ili ilingane walao na viwango vya mishahara na marupurupu kwa vyuo vingine hapa Afrika Mashariki.

- **Uboreshaji wa mitaala**

Serikali kwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali toka kwenye vyuo vinavyohusika itaanzisha program ya kuifanyia mitaala inayotumika marekebisho ili ilenge zaidi kwenye kuandaa wahitimu walio tayari kwa kazi.

- **Kuongeza nafasi zaidi za masomo ya Sayasi na Teknolojia**

Pamoja na kwamba serikali ya CUF inakusudia kuipanua elimu ya juu nchini kwa ujumla, ongezeko la nafasi kwa fani za sayansi na teknolojia litapewa kipaumbele. Chini ya mkakati huu madaktari, mainjinia, wanasayansi na wataalamu wa kompyuta wengi zaidi wataandaliwa kila mwaka. Serikali pia itaendelea kuziunga mkono juhudi za watu binafsi, mashirika ya dini, na taasisi nyingine zenye malengo ya kuanzisha vyuo vikuu kwa ajili ya taaluma mbalimbali.

- **Kuimarisha huduma za kitafiti**

Ukiondoa maslahi madogo, udhaifu mkubwa katika huduma za kitafiti ni sababu nyingine kubwa inayowafanya wataalamu mbalimbali kuzikimbia taasisi zetu za elimu ya juu. Seriklali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itajitahidi kuziimarisha huduma hizi kwa kutoa fedha zaidi

kwa ajili ya vifaa na masurufu. Aidha, itaanzisha kitengo maalumu cha uratibu wa kuzifanyia kazi tafiti/vumbuzi mbalimbali zinazopatikana kutokana na jitihada zilizofanywa katika vyuo vyetu.

- **Ujenzi wa miundombinu katika vyuo vikuu vyote**

Seriklali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itatengeneza miundombinu ambayo itawezesha mazingira ya vyuo kuvutia wanafunzi wa ndani na nje ya nchi. Seikali itahakisha kuna vifaa vya kitaalam na kiteknolojia vya kutosha, vitabu vya kutosha, na kuboresha vyumba vya masomo, barabara, korido zenye mapaa juu yake kwenye kila njia zinzounganisha darasa na darasa, ofisi za wahadhiri, sehemu za chakula, mabweni na maeneo mengine. Mtandao huu utasaidia kurahisisha mawasiliano na kupelekea vipindi madarasani kutosimamia hasa nyakati za mvua, ambapo wanafunzi na wahadhiri wengi hushindwa kufika madarasani.

- **Maktaba zenye uwezo mkubwa**

Miaka 56 sasa tangu Muungano hali ya maktaba zetu bado ni duni. Seriklali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa maktaba zetu zinakuwa na uwezo mkubwa sawa na maktaba za nje; na kwa kutumia mawasiliano ya intaneti wanafunzi wa vyuo vyetu wataweza muda wote kusoma vitabu mbalimbali vilivyoko katika maktaba za vyuo vikubwa duniani

**ELIMU MAALUM KWA WATU WENYE ULEMAVU**

Kwa bahati mbaya baadhi ya ndugu zetu wengi nchini wana ulemavu na wana mahitaji ya elimu maalum ili kuweza kujiendeleza. Kwa kawaida watoto au watu wenye ulemavu kwa ujumla wake huwa wana mahitaji maalumu ikiwemo ya uangalizi wa muda wote kulingana na aina na kiwango cha ulemavu wa mtu husika. Hili hupelekea kuwepo kwa gharama za kuwahudumia waangalizi. CUF tunaamini kuwa kuziwezesha familia zenye watoto wenye ulemavu kutasaidia kwa kiasi

kikubwa kukabiliana na vikwazo vya kielimu wanavyopata watoto wenye ulemavu.

**Hali ilivyo sasa**

- Kukosekana kwa sera ya elimu inayojumuisha mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu kwa uwazi kumesababisha idadi kubwa ya vijana wenye ulemavu kukosa fursa ya kupata elimu.
- Huduma zilizoko katika taasisi mbalimbali za elimu kuanzia ngazi ya msingi, sekondari, na vyuo hazijazingatia kikamilifu mahitaji maalum ya wenye ulemavu.
- Hali duni ya maisha ya wazazi ni kikwazo kwa watoto wenye ulemavu kupata elimu bora.
- Ukosefu mkubwa wa vifaa vya kujifunzia ni kikwazo kwa watoto wenye ulemavu kupata elimu bora.
- Kukosekana kipaumbele na kutozingatia kutenga bajeti ya kutosha ya kuwawezesha watoto wenye elemavu ni kikwazo.
- Ulaghai wa kisiasa unaofanyika kwa baadhi ya watu wenye ulemavu na kusahau kusimamia haki za msingi za watu wenye ulemavu ni kikwazo.
- Mazingira hatarishi ya maisha ya watu wenye ulemavu ni kikwazo.

**Dira ya mabadiliko ya CUF**

Kwa kutambua umuhimu mkubwa wa kuwaendeleza watoto wenye ulemavu na kuwapunguzia wazazi mzigo wa ziada katika kuwahudumia, serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua zifuatazo:

- Itazindua sera mpya ya elimu ambayo itakuwa imeyajumuisha kwa ukamilifu mahitaji maalum ya wanafunzi wenye ulemavu.

- Itafanya marekebisho mbalimbali ya kiufundi kwenye taasisi mbalimbali za elimu ili kuondoa vikwazo mbalimbali vinavyowakwaza wanafunzi wenye ulemavu wanaosoma katika taasisi hizo.

- Mahitaji maalum ya kielimu kwa watu wenye ulemavu yatajumuishwa katika mitaala ya vshule na yuo vya waalimu ili kuongeza idadi ya wallimu wenye uwezo wa kutoa elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu.

- Serikali itagharamia kwa asilimia mia moja gharama zote zinazohusiana na masomo ya wanafunzi wenye ulemavu katika ngazi zote za elimu.

**ELIMU YA WATU WAZIMA**

Miaka 56 baada ya kuzaliwa Tanzania bado kuna tatizo la kutojua kusoma na kuandika.

**Hali ilivyo sasa**

- Kuupuuzia kwa muda mrefu umuhimu wa kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule wameandikishwa shule, kumechangia sana katika kuongeza idadi ya vijana wanaoingia katika utu uzima ilhali hawaji kusoma na kuandika.

- Kuanguka kwa ubora wa taaluma inayotolewa katika shule za msingi kume sababisha kundi kubwa la watoto kumaliza darasa la saba wakiwa na uwezo kidogo sana wa kusoma na kuandika. Wengi wa hawa hupoteza ujuzi huu baada ya miaka michache huko mitaani kwa sababu ya kutoweka kwa kiasi kikubwa kwa utamaduni wa kujisomea miongozi mwa wananchi.

- Hivi sasa maktaba mbalimbali za serikali zinatoza ada kwa wanaotaka huduma ya kujisomea. Hali hii inazidi kufifisha hamu ya wananchi kujifunza na kujiendeleza kielimu.

- Mkazo uliokuwepo katika miaka ya 70 kuhusu elimu ya watu wazima uliachiwa taratibu kufifia hadi hatimaye ukatoweka kabisa. Kwa hivi sasa fedha za bajeti ya elimu ya watu wazima zinatolewa lakini haziwanufaishi walengwa.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahusisha upya madarasa ya elimu ya watu wazima. Serikali itaandaa utaratibu utakawezesha kila shule ya msingi iliyoko nchini kuendesha madarasa ya elimu ya watu wazima kila jioni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Kwa hali hii fedha za bajeti ya elimu ya watu wazima zitatumika ipasavyo na hivyo kuwanufaisha walengwa.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafuta ada zote zinazotozwa na maktaba za serikali hivi sasa, na kuhakikisha kuwa huduma katika maktaba hizi zinaboreshwa kwa kiwango cha juu, ili kukidhi haja ya wananchi kujiendeleza kielimu.

- Maktaba zote za serikali nchini zitaunganishwa na mtandao wa intaneti na zitafanya kazi kwa masaa 24.

**Elimu ya ufundi**

Kati ya mambo ambayo Serikali ya CCM haijafanikiwa ni kuimarisha vyuo vya elimu ya ufundi. Nchi yoyote iliyowekeza katika elimu hii inajiweka katika mazingira mazuri ya kuleta maendeleo haraka kwani vijana wengi wanapata ujuzi na kujiajiri katika sekta binafsi au zisizo rasmi.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

Elimu ya ufundi kuwa nyenzo muhimu ya maisha ya vijana.

- Shule na vyuo vya ufundi vitaongezwa katika kila wilaya, kila mwaka, hatua kwa hatua hadi kukidhi mahitaji yaliyopo.
- Kila kijana atakayemaliza elimu ya msingi na hakupata fursa ya kujiunga na shule ya sekondari lazima apate nafasi ya kusoma masomo ya ufundi ili ajijengee mazingira ya kupata ajira au kuwa na uwezo wa kujiajiri katika sekta binafsi.
- Serikali itawapeleka walimu wengi zaidi katika mafunzo ya juu ya ufundi ili vyuo vya ufundi viwe na wataalam wa kutosha.

### 3.1.22. AFYA

Katika Tanzania tatizo la afya za wananchi ni kubwa mno. Huduma za afya ziko katika hali mbaya sana. Hospitali, vituo vya afya, na zahanati ni chache na zinakabiliwa na matatizo mengi. Msongamano mkubwa wa wagonjwa, uhaba wa madaktari na wauguzi, uhaba wa vitanda, uhaba wa vifaa vya kazi, uchakavu wa majengo, na zaidi ya yote, uhaba mkubwa wa madawa ni baadhi tu ya matatizo haya. Utafiti unaonesha kuwa zaidi ya 60% ya watoto wanaokufa chini ya umri wa miaka mitano hufia majumbani bila kufikishwa hospitali au zahanati angalau mara moja. Inakadiriwa kwamba katika kila watoto 100 wenye umri usiozidi miaka mitano, zaidi ya 40 wanakosa lishe bora na kwa hivyo wameathirika kwa utapiamlo. Watoto wanaokosa lishe bora hawajengi kinga ya mwili na ubongo wao haukuwi vizuri.

Ni lazima tuelewe kuwa maendeleo hayawezi kupatikana kwenye Taifa lenye idadi kubwa ya watu ambao hawana afya nzuri.Tunawajibika kujenga mazingira yatakayouhakikishia umma kuwa kuna nia ya dhati ya kuifufua na kuiboresha sekta ya afya. Tuandae madaktari na wauguzi kwa wingi zaidi na wapewe motisha wa kutosha ili wasilazimike kuikimbia nchi. Hospitali kuu zote kuanzia wilayani zipatiwe vifaa vya

kisasa vinavyohitajika kukidhi haja ya matibabu katika ulimwengu wa kileo. Madawa yapatikane kwa gharama nafuu. Ni lazima uandaliwe utaratibu utakaotuhakikishia kwamba Mtanzania yeyote hatakosa kupata matibabu kwa sababu tu ameshindwa kumudu gharama. Lakini lililo la msingi kabisa ni kufufua na kuimarisha huduma ya afya ya kinga. Uboreshaji wa mazingira ni sehemu muhimu kabisa katika utoaji wa huduma ya afya ya kinga. Ili kuzuia utapiamlo na maradhi mengine serikali isimamie na kuratibu uwekezaji wa virutubisho muhimu kama vile iodine kwenye chumvi, vitamin A na D kwenye unga na kadhalika.

Ni lazima tuondoe vyanzo vya maradhi; taka zizolewe na turejeshe utaratibu uliotoweka siku nyingi zilizopita wa kudhibiti wadudu wanaobeba vimelea vya maradhi, hususan mbu. Ni lazima tuweke utaratibu utakaotuhakikishia kuwa wananchi hawaishi na kufanyia shughuli zao kwenye maeneo yenye msongamano mikubwa. Ni lazima tufufue na kuimarisha huduma za ukaguzi za mabwana na mabibi afya, ili kuhakikisha kuwa migahawa, maduka, masoko, machinjio, makazi yetu nakadhalika, yanakuwa katika mazingira salama muda wote. Pamoja na haya yote ni lazima tuhakikishe kuwa suala la uhaba wa maji safi na salama kwa matumizi ya mjumbani linapatiwa ufumbuzi wa haraka. Aidha ni lazima kama Taifa kuliangalia upya suala la maambukizi ya UKIMWI kwa uzito unaostahili.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya Afya**

- Utaratibu wa kinga ya msingi kwa maradhi umepuuzwa kwa kiwango kikubwa. Huduma ya kuzoa taka na mfumo wa maji machafu ziko katika hali mbaya. Mkakati wa kuharibu vyanzo vya maradhi umeachwa muda mrefu uliopita.

- Wafanyakazi wa sekta ya afya wanafanya kazi katika mazingira ya hatari yanayoweza kuwaletea maambukizi, mishahara ni midogo ambayo hailingani kabisa na ugumu wa kazi. Wakilalamika

wanaitwa "wabinafsi" wasiojali "wito" wa kazi yao na kukumbushwa viapo walivyoapa. Matokeo yake madaktari na wauguzi wamekuwa ‘ombomba' na wagonjwa wasio na chochote cha kutoa wamejikuta wakitelekezwa. Nchi jirani zimekuwa ndiyo kimbilio kubwa la madaktari na wauguzi wetu.

- Zahanati, vituo vya afya na hospitali ni chache na hazikidhi hitajio la ukuaji wa idadi ya watu Tanzania.

- Huduma muhimu katika vituo vya afya na hospitali kama madaktari na wauguzi, madawa, vitanda na vipimo havitoshelezi mahitaji.

- Serikali imeendelea kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kutoa huduma bora ya afya nje ya nchi kwa kundi la watu wachache ambao ni viongozi waandamizi na familia zao.

- Utaratibu wa kuwalazimisha wananchi kulipia gharama za matibatu umeasabisha wananchi wengi kuathirika kwa kushindwa kumudu gharama hizo.

- Kuanzia mwaka 1985 hatua na mikakati kadhaa imechukuliwa yote ikilenga katika kuelimisha na kuhamasiha jamii juu ya athari za maambukizo ya UKIMWI na njia ya kudhibiti kuenea kwa maambukizi mapya. Hata hivyo pamoja na kampeni hizi, maambukizi ya Ukimwi bado yameshika kasi na wanaougua maradhi haya wanazidi kujitokeza. Pamoja na kujitokeza kwa hali hii Serikali ya CCM imeshindwa kubadili mwelekeo wa kampeni zinazofanyika ili ziweze ktufikisha kwenye malengo tuliyokusudia.

- Mpango wa bima ya afya ulioletwa na serikali ya CCM katika miaka ya hivi karibuni unafanya kazi katika maeneo machache na hivyo kuwasababishia usumbufu mkubwa wanachama wa mfuko huo. Hata hivyo kutokana na kuelemewa na idadi kubwa ya

wagonjwa mpango huo unaelekea kufilisika na imebidi yafanyike mabadiliko yanayolenga kupunguza aina ya magonjwa yanayotibiwa kwa bima.

- Hivi sasa hospitali nyingi za serikali zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa wagonjwa siyo kwa sababu wananchi wanaoumwa hawapo, bali kwa sababu wengi hawawezi kumudu gharama za matibabu.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF katika kuboresha sekta ya Afya nchini**

Kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo la afya kwenye jamii yetu, serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itatenga asilimia 15 ya bajeti yote ya serikali kwa ajili ya kuboresha huduma za afya. Miongoni mwa mambo yatakayotekelezwa ni haya yafuatayo:

- **Huduma za afya ya msingi bila malipo**

Huduma za msingi za afya zitakuwa ni haki ya kila Mtanzania. Mkazo maalum utawekwa katika tiba ya kinga ikiwa ni pamoja na chanjo za watoto, kuweka virutubisho katika vyakula (food fortification) hususn unga wa mahindi na unga wa ngano, na kutoa elimu ya afya kwa mapana na marefu. Tiba ya maradhi ya kimfumo (non cummunicable diseases) kama saratani, kisukari, figo na shinikizo la juu la damu, baadhi ya maradhi ya kuambukiza kama vile malaria, kifua kikuu, UKIMWI, cholera, kifua kikuu (TB), typhoid, na minyoo na zitapatikana bila malipo.

- **Huduma za upendeleo**

Kina mama wajawazito na wale waliotupa mimba, kina mama wenye mauvimbe tumboni, wazee kuanzia miaka sitini, wenye ulemavu na watoto wadogo wote walio na umri chaini ya miaka mitano watapata matibabu yote bure. Aidha, srikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF

itaendeleza utaraibu wa ugawaji wa vyandarua vyenye dawa na kuhakikisha kila mtanzania anapata chandarua cha aina hii, sanjari na kuwa na program endelevu ya kuangamiza mazalia ya mbu.

- **Utaratibu wa kuchangia gharama**

Pamoja na ongezeko kubwa katika bajeti ya afya bado bajeti hiyo itakuwa haitoshelezi kwa kulinganisha na mahitaji halisi. Ili kufidia pengo kuna umuhimu mkubwa kwa vyanzo vingine kuchangia katika huduma za afya. Uchangiaji huu utafanyika chini ya taratibu ufuatao:

- **Mpango wa bima ya matibabu**

Serikali itasimamia uboreshaji wa utaratibu wa bima ya matibabu nchini ambapo waajiri wote katika sekta rasmi watatakiwa kuwakatia wafanyakazi wao bima, na pia kuwawezesha wanachama wa mpango huo kupata huduma hiyo mahala popote humu nchini. Bima hiyo itagharimia matibabu ya wanayakazi na familiza zao, yasiyohusiana na huduma za msingi za afya au huduma za upendeleo. Bima hii haitakuwa mzigo kwa waajiri kwa kuwa itamezwa katika marekebisho ya viwango vya kodi yatakayofanywa na serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF.

- **Uchangiaji wa gharama wa moja kwa moja**

Utaratibu wa kuchangaia moja kwa moja gharama za matibabu yaliyo nje ya huduma za msingi za afya, au zile za upendeleo utaendelezwa kwa wananchi ambao watakuwa hawana bima na wenye uwezo wa kuchangia gharama. Kwa wagonjwa ambao watakuwa hawana uwezo kabisa gharama za matibabu yao yote zitabebwa na serikali.

- **Kuboresha miundo mbinu ya afya**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo mazingira ya hospitali zote nchini

kuanzia chini kabisa yameboreshwa na kufikia viwango vinavyokubalika. Fedha zaidi zitatumiwa kuhakikisha kuwa ifikapo mwishoni mwa kipindi hicho hakuna mgonjwa anayelala chini au kuchangi kitanda. Serikali pia itahakikisha kuwa vipimo vyote mahimu vinapatikana kuanzia wilayani, na kila hospitali kuanzia wilayani ina madaktari na wauguzi wa kutosha kuweza kutoa huduma bora. Serikali pia itahakikisha kuwa huduma zote za msingi ikiwemo maji na umeme vinapatikana kwa uhakika.

- **Kuboresha huduma ya matibabu**

Kila hospitali itabuni utaratibu wa kuongeza tija. Pamoja na wambo mengine utaratibu huu ni lazima uhakikishe kuwa kila mgonjwa atakayelazwa wodini ataanza kupata matibabu mapema iwezekeavyo. Kutafanyika ukaguzi wa mara kwa mara kwenye hospitali utakaohusisha kuwasaili wagonjwa mbalimbali kwa siri ili kupima ni kwa kiwango gani mahospitali yanazingatia utaratibu huu.

- **Kuimarisha huduma za kinga**

Taifa linaweza kuokoa fedha nyingi sana zinazotumika kwa matibabu iwapo watu watajikinga na maradhi. Ili watu waweze kujikinga na maradhi Taifa halina budi kuzingatia kanuni za afya ya msingi kama usafi wa mazingira na kuzuia vyanzo vya maradhi. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itashirikiana na serikali za mitaa kuhakikisha kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo vyanzo vyote vya maradhi ya kuambukiza kama mrundikano wa takataka, mazalia ya mbu, na kusambaa kwa maji taka vinadhibitiwa.

- **Nidhamu ya matumizi ya fedha za mfuko wa afya**

Serikali itafanya utaratibu wa kupunguza idadi ya wafanyakazi wa maofisini katika sekta ya afya na kuwahamishia katika ajira nyingine bila kuathiri huduma, na fedha zitakazookolewa zitaelekezwa kwenye kuboresha miundo mbinu na maslahi ya madaktari na wauguzi.

- Serikali itaboresha hospitali zetu kwa kuzipatia zana za kisasa, madaktari na wataalamu wenye uwezo ili kupunguza uwekekano wa viogozi waandamizi kutumia fedha nyingi za wananchi kwa ajili ya matibabu nje ya nchi.

- Ili kuongeza ufanisi baadhi ya huduma kwenye mahospitali ambazo hazina uhsiano wa moja kwa moja na tiba zitabinafsishwa.

- **Kupunguza gharama za madawa**

Serikali itafanya mazungumzo na wawekezaji zaidi ili kujenga viwanda vitakavyozalisha madawa ya kuiga (Generic Drugs) na vifaa vingine vya mahospitali kwa gharama nafuu zaidi nichini mwetu. Kupitia viwanda hivi madawa ya msingi yatazalishwa kwa wingi na kuwekwa nembo ya serikali ili kudhibiti matumizi mabaya.

- **Maslahi ya madaktari na wauguzi**

Kwa kuzingatia kuwa madaktari na wauguzi ni watu ambao wanafanya kazi ngumu na kwenye mazingira ya hatari, ni lazima Taifa lielewe kuwa maslahi yao yanahitaji kuboreshwa zaidi. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa maslahi ya wafanyakazi hawa yanaboreshwa angalau kufkia viwango vya wenzao katika nchi jirani. Serikali itaongeza mishahara na marupurupu kwa madaktari na wauguzi kwa kadri uchumi wa nchi unavyokua ili kuwafanya madaktari na wauguzi wajitume zaidi, wajiepushe na vitendo ya rushwa , na kujikita zaidi katika kuokoa maisha ya Watanzania yanayopotea wakati mwingine kwa sababu tu ya kushuka kwa ari ya kufanya kazi miongoni mwa madaktari na wauguzi.

- **Mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF pamoja na mambo mengine itaweka mkakati wa kitaifa utakaolenga kupunguza kwa kiasi kikubwa

uwezekano wa mtu ambaye hivi sasa hana virusi vya ikumwi, kuambukizwa. Mkakati huu utalenga katika kuishirikisha jamii katika mjadala wa kutunga sera mahsusi ya nchi itakayosimamia mapambano dhidi ya Ukimwi, kwa nia ya kufanikisha malengo yafuatayo:

- Kuondoa utaratibuu wa sasa unaofanya taarifa za maambukizi ya ukimwi kuwa ni siri na badala yake taarifa hizi ziwe za wazi kama ilivyo kwa magonjwa mengine.

- Kuweka utaratibu wa kutangazwa na kuchapishwa kila mwezi kwa takwimu za maambukizi ya ukimwi kuanzia katika ngazi za kata ili kumwezesha kila mwananchi kuwa na taarifa sahihi zinazohusu eneo analoishi.

- Kufikia makubaliano ya kitaifa ni nini kifanyike ili kudhibiti kwa kiwango cha juu kabisa uwekekano wa maambukizi kwa wananchi wetu ambao bado kuambukizwa.

- Kuanzisha utaratibu wa makusudi wa kuziunga mkono na kutoa kila aina ya msaada unaowezekana, juhudi za watafiti wa kizalendo ikiwa ni pamoja na waganga wa jadi katika kutafuta tiba au kinga dhidi ya maambukizo ya virusi vya ukimwi.

- Kuhakiki kuwa waathirika wote wa UKIMWI wanapatiwa madawa ya kungeza muda wa kuishi ili waendelee kutoa mchango muhimu katika malezi ya familia zao na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

- Kuendeleza na kuimarisha taasisi za kutoa elimu dhidi ya UKIMWI zitakazoweka msisitizo juu ya ukweli kwamba njia ya uhakika ya kujikinga dhidi ya maambukizo ni kuacha kufanya vitendo vya uasherati.

- Kujenga uchumi imara unaoongeza ajira, tija na neema kwa wote utakaopelekea jamii kujishughulisha zaidi katika masuala ya msingi na kujiepusha na vitendo vya ukahaba na uasherati.

### 3.1.23. ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI

Pamoja na kwamba Tanzania ina wizara nzima inayoshughulikia masuala ya Ardhi, ina Chuo kikuu kishiriki kinachoshughulikia masuala ya Ardhi tu na kuna Idara za Mipango Miji katika kila Halmashauri na Mabaraza ya Miji, hali ya makazi ya wananchi bado siyo nzuri. Gharama kubwa ya viwanja vilivyopimwa umewalazimisha wananchi wengi kujenga kiholela. Aidha kuna uhaba mkubwa wa huduma za msingi kama vile mitaro ya maji machafu, barabara zisizo na msongamano, vyoo vya umma, viwanja vya kuchezea watoto na sehemu za kuzikia za uhakika. Inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wakazi wote wa jiji la Dar es salaam wanaishi kwenye maeneo yaliyojengwa kiholela na yenye msongamano mkubwa. Aidha hali hii imewalazimisha baadhi ya Wananchi wengine kujenga sehemu za mabondeni na hivyo kuhatarisha usalama wa maisha na mali zao wakati wa kipindi cha mvua.

Ukosefu wa sehemu za uhakika kwa wafanyabiashara ndogondogo ‘Machinga' na uhaba wa vituo bora vya mabasi na maegesho rasmi kwa ajili ya vyombo vya usafiri hususan magari, umetokea kuwa ni kero kubwa kwa wananchi wengi, hususan katika jiji la Dar es salaam. Pamoja na yote haya pia kuna udhaifu mkubwa sana katika kusimamia sheria zinazotawala makazi.

Pamoja na matatizo haya, sheria ndogondogo zinazotungwa na halmashauri na mbaraza mengi ya miji hazizingatiii hali halisi ya kimaisha ya wakazi wa miji husika. Mathalani, katika baadhi ya miji kuna sheria inayowakataza wakaazi kufanyia matengenezo nyumba zao zinazochakaa kwa maelezo kwamba maeneo zilizoko nyumba hizo

yametengwa kwa ajili ya kujenga magorofa. Matokeo ya sheria hii ni kwamba katika miji mingi kuna nyumba nyingi chakavu zinazokaribia kuanguka huku wamiliki wake wakisubiri zianguke na wao kupoteza haki ya kumiliki viwanja husika, kwa sababu hawana uwezo wa kujenga maghorofa. Ni wazi kabisa kuwa sheria ya namna hii siyo tu kwamba ni ya kikandamizaji, lakini pia ni yenye kuongeza kiwango cha umasikini miongozi mwa wananchi.

**Hali ilivyo sasa**

- Shirika la nyumba la Taifa ambalo kinadharia lilianzshwa kwa malengo ya kutatua tatizo la makazi kwa wananchi, hususan wale wanaoishi mijini limeshindwa kabisa kutimiza azma hiyo. Kasi ya ujenzi wa majengo mapya imefifia kabisa, na majengo yake mengi ya zamani, ikiwemo yale liliyoyarithi kutoka kwa wamiliki wake halali baada ya kutaifishwa, yako katika hali mbaya sana kutokana na kutokuwa na uangalizi mzuri. Hivi sasa shirika hilo liko kwenye mgogoro mkbuwa na baadhi ya wapangaji wake kutokana na kupandisha kodi bila kuzingatia hali halisi ya uboreshaji wa makazi hayo.

- Pamoja na srikali kubuni mradi wa viwanja elfu ishirini (20,000) katika jiji la Dar es salaam, bei za viwanja hivyo ni za juu mno kwa watu wa kawaida kuweza kuzimudu. Matokeo yake ni kwamba vingi kati ya viwanja hivyo vimeangukia katika mikono ya watu wachache wenye uwezo, na wananchi wa kawaida (ambao ndio wengi) wanaendelea na ujenzi holela katika maeneo yasiyofaa.

- Kasi ya kuboresha maeneo ya makazi ambayo hayajapimwa kwa kujenga barabara, kuweka maeneo ya ujenzi wa shule, vituo vya afya, na viwanja vya kuchezea watoto ni ndogo mno. Matokeo yake ni kwamba huduma muhmu, mathalan za magari ya zima moto na

magari ya wagonjwa bado ni vigumu kuwafikia wakazi walio wengi katika maeneo hayo.

- Kuna udhaifu mkbuwa katika kuandaa maeneo ya wafanyabiashara ndogondogo ‘machinga' na maeneo mengine muhimu kama vituo vya mabasi ya daladala. Kutokana na hali hii kuna baadhi ya mitaa ambayo wakazi wake wanapata adha kubwa kutokana na msongamano mkubwa wa biashara hizo na wingi wa daladala zilizogeuza mitaa hiyo kuwa stendi za kupaia na kushusha abiria.

- Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa sheria ndogondogo zinazotawala makazi na hususan katika maeneo ya mijini, bila ya hatua zozote kuchukuliwa.
- Sheria katika baadhi ya miji na manispaa zinazokataza wakazi wa baadhi ya maeneo kufanyia matengenezo nyumba zao kwa kisingizio kuwa maeneo hayo yametengwa kwa ajili ya ujenzi wa maghorofa ni za udhalilishaji, zinalenga kuongeza umasikini katika jamii, na zinakiuka haki za binadamu.

- Serikali imeshindwa kabisa kukitangaza kitengo chake cha mradi wa utafiti wa nyumba za bei nafuu na matokeo yake ni kwamba wananchi walio wengi hawanufaiki na kuwepo kwa kitengo hicho.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

**Ili kuboresha makazi, serikali ya CUF itachukua hatua zifuatazo:**

- **Kubinafsisha shirika la nyumba la Taifa**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF intaweka utaratibu wa kuwarejeshea majumba yao wale wote waliokuwa wametaifishwa na hawakulipwa fidia, na baada ya zoezi hili italibinafsisha shirika la nyumba la Taifa.

- Baada ya kuibinafsisha NHC serikali itaanzisha utaratibu wa kutoa mikopo ya gharama nafuu kwa vyama vya ushirika wa nyumba "Housing cooperatives) ili kuwezesha wananchi waliojiunga katika vyama hivyo kupata makazi bora na kulipa kidogo kidogo.

**Upatikanaji wa viwanja vilivyopimwa**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kwamba katika kipindi cha miaka miwili tu, katika miji yote nchini viwanja vilivyopimwa na vinavyopatikana kwa bei nafuu ndivyo vitatafuta wajenzi, badala ya hivi sasa ambapo wananchi mbalimbali wenye nia ya kujenga ndio wanaohaha kutafuta viwanja hivyo. Huduma za barabara, maji ya umeme kwenye makaazi zitakwenda sambamba na upimaji wa viwanja vipya.

- **Uboreshaji wa mazingira ya miji**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itasitisha mara moja ukiukwaji mkubwa wa sheria za mipango miji uliopo hivi sasa. Aidha kwa kushirikiana na serikali za mtaa, serikali itaweka mkakati imara wa kuhakikisha kuwa kila penye makazi na hasa kwenye maeneo ambayo yemjengwa kiholela, barabara zinapitishwa, mitaro ya maji machafu inakuwepo au kufanyiwa ukarabati, vyoo vya umma vinasambazwa, taka zinazolewa kwa wakati na madimbwi yanayotuama maji wakati wa mvua yanashughulikiwa. Serikali pia itahakikisha kuwa uhaba wa sehemu za kuzikia, vituo bora vya mabasi na sehemu za uhakika kwa biashara za ‘Machinga', viwanja vya kuchezea watoto, na bustani za mapumziko unapatiwa ufumbuzi wa haraka.

- **Gharama za ujenzi**

Gharama za ujenzi zitapungua kutokana na azma ya serikali ya kurekebisha viwango vya kodi katika vifaa vya ujenzi. Serikali

itakiimarisha na kukitangaza kwa nguvu zote kitengo chake cha mradi wa utafiti wa nyumba za bei nafuu na kuwahamasisha wananchi wote wa mijini na vijijini wakitumie kujengewa nyumba bora kwa gharama nafuu. Aidha katika maeneo ya mijini makampuni zaidi yatahamasishwa kwa ajili ya kujenga nyumba za gharama nafuu na kuzigawa kwa wananchi mbalimbali kwa mikopo ya masharti nafuu.

- Sheria ndogo iliyotungwa na baadhi ya manispaa inayowakataza wakazi wa baadhi ya maeneo kufanyia matengenezo nyumba zao, kwa madai kwamba maeneo hayo yametengewa kwajili ya maghorofa itafutwa.

- **Kuondoa msongamano wa magari**

Kwa sababu wakazi wa miji mkubwa yote ndani ya nchi na hasa Dar es salaam wanakumbana na tatizo kubwa la msongamano ya magari, Serikali itahakikisha msongamano unamalizwa kwa kuanzisha barabara mbadala (alternative roads), kujenga madaraja ya juu (fly overs) kwenye makutano muhimu katika miji yenye msogamano pamoja na kupanua barabara zote za miji yenye msongamano kutoka kwenye "single roads" njia moja, hadi kuwa njia mbili.

- Lakini kubwa zaidi serikali itahakikisha kuwa barabara zote za miji mikubwa zinawekewa mfumo wa taa za barabarani ili kuwawezesha watu kufanya shughuli zao muda wote bila kuhofia usalama wao.

## 3.1.24. MAENDELEO YA MAKUNDI YA JAMII

### Wenye Ulemavu

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya la Dunia, katika kila watu kumi ulimwenguni mmoja ana ulemavu. Kwa kuwianisha, hii ina maana kwamba asilimia 10 ya watanzania wote wana ulemavu wa aina moja

ama nyingine. Kwa mtizamo wa aina yoyote ile idadi hii ni kubwa mno kiasi cha kuhitajika mipango maalum ya kuwahudumia.

**Hali ilivyo sasa**

- Baada ya miaka 56 ya uhuru taifa letu bado halina sera sahihi inayowalenga wenye ulemavu kuwahakikishia kuwa wanapata fursa sawa katika masuala yote yanayoihusu jamii.
- Mchakato mzima wa uendeshaji masula mbalimbali ni wenye kuwabagua na kuwapuuza wenye ulemavu. Juhudi za makusudi zinazofanywa kuwaondolea wenye uelmavu vikwazo mbalimbali wanavyokabiliana navyo hata pale ambapo mazingira ya kufanya hivyo yanaruhusu hazijitoshelezi.
- Serikali imeshindwa kujenga mazingara mazuri kushughulikia ulemavu unaoepukika na ule unaoweza kupunguzwa makali yake.
- Serikali imeshindwa kutekeleza sheria namba 2 na namba 3 za mwaka 1982 zinazolinda ajira na matunzo kwa watu wenye ulemavu. Aidha serikali ya CCM imeshindwa kutekeleza maazimio mbalimbali likiwemo lile la Umoja wa mataifa namba 149 la mwaka 1982 linalohusu wenye ulemavu pamoja na Mwongo wa watu wenye ulemavu 2000 - 2009 (African Decade).

**Dira ya Mabadiliko ya CUF kwa watu wenye ulemavu**

CUF inatambua kuwa ni vigumu kupata ufumbuzi muafaka wa matatizo ya wenye ulemavu bila kuwashirikisha kikamilifu. Aidha inatambua kuwa ukiondoa ulemavu wa kuzaliwa, kuna aina nyingi za ulemavu zinazoepukika iwapo hatua sahihi na za makusudi zitachukuliwa. Kwa kuzingatia utambuzi huu serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanya yafuatayo:

Kwa kushirikiana na wadau husika serikali itaandaa na kupitisha sera ya kitaifa itakayojulikana kama 'EQUALISATION OF OPPURTUNITIES POLICY' ambayo pamoja na mambo mengine itasimamia kikamilifu ushiriki wa wenye ulemavu katika masuala yahusuyo Utawala, Siasa, Ajira, Afya, Elimu, Na Michezo.

- Serikali itahakikisha kuwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, wakiwemo watu wenye ulemavu wenyewe, inapitia upya sheria mbalimbali zinazokwaza haki za kundi hilo na kupitia upya sheria namba 2 na namba 3 za mwaka 1982 kuhusu ajira na matunzo kwa watu wenye ulemavu, ili kuziboresha kabla ya utekelezaji kamilifu. Aidha, serikali itahakikisha kwamba maridhio yote ya kimataifa ya haki za watu wenye ulemavu yanatekelezwa ipasavyo.

- Serikali itasimamia kikamilifu kuhakikisha kuwa mazingira mbalimbali yanayosababisha ulemavu unaoepukika yanadhibitiwa. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na:

- Kudhibiti kikamilifu usalama katika viwanda, migodi, na maeneo mengine. Kutakuwa na sheria inayoagiza kuwepo na sera ya ndani inayosimamia usalama ambayo pamoja na mambo mengine itajumuisha na ukaguzi wa kila siku wa usalama wa mazingira ya kazi (safety audits).

- Kudhibiti kikamilifu ubora wa madereva na vyombo vya abiria, na njia vinakopita vyombo hivyo ili kupunguza ajali.

- Kutengeneza mazingira rafiki yatakayowasaidia sana wenye ulemavu kuzifikia huduma bila kutegemea msaada, kwa mfano kutengeneza njia maalum wanazoweza kupita wakiwa katika hospitali, shule, vituo vya mabasi na sehemu nyingine za utoaji huduma kwani sehemu zote hizi zimejengwa bila kujali kuwa kuna

walemavu. Mfano mzuri ni pale majengo yanapowekewa ngazi peke yake bila kukumbuka kuwa wenye ulemavu wa miguu hawataweza kupita.

- Serikali itasimamia kikamilifu kuhakikisha kuwa hatua muafaka za kitabibu zinachukuliwa kushughulikia ulemavu unaopunguzika. Hatua hizo ni pamoja na:
    - Utoaji bure wa viungo bandia, baiskeli za magurudumu rnatatu, vifaa vya kusikilizia (hearing aid devices), miwani ya jua, mafuta maalumu ya ngozi na vifaa vingine.
    - Kupitisha sheria inayoelekeza kuwa watoto wote wanaozaliwa wakiwa na athari zinazorekebishika wanapatiwa matibabu bila kuchelewa.
    - Kuhakikisha watu wenye ualbino wanajumuishwa kwenye makazi jumuishi na jamii/serikali kusimamia usalama wao.

**Wanawake**

Ingawa wanawake ni zaidi ya asilimia 51 ya wananchi wote wa Tanzania, mila na desturi, matatizo ya kihistoria na uzembe wa muda mrefu wa Serikali vimesababisha kuwe na tofauti kubwa ya kifursa kati ya Watanzania wanaume na Watanzania wanawake. Kipaumbele katika fursa zinazogusa masuala mengi muhimu katika jamii kimekuwa kikitolewa kwa wanaume zaidi. Hali hii imewajengea wanawake kutojiamini iwe ni katika masuala ya uongozi, elimu, kazi, na hata katika masuala ya kifamilia.

Kwa upande mwingine, hali hii imewajengea wanaume wengi mtizamo hasi juu ya uwezo wa wanawake. Wanaume wengi waliokumbatia mila na desturi, na hasa wale ambao hawakubahatika kupata elimu ya kutosha wamejenga mazoea ya kuwachukulia wanawake kama viumbe

duni na wasiokuwa na mchango wowote kifikra zaidi ya kuzaa watoto, kutafuta mahitaji ya familia, na kuwatumikia wanaume. Kwa muda sasa kumekuwa na juhudi za makusudi na hasa kutoka kwa kina mama wenyewe, zenye kulenga kujaribu kurekebisha hali hii. Sehemu kubwa ya juhudi hizi zimelenga zaidi katika kuhimiza kuwe na upendeleo maalum kwa wanawake. Pamoja na uzuri wa jitihada hizi, ni dhahiri kuwa hazitoshi na bado kazi kubwa inahitajika kufanyika ili hatimaye tofauti za kijinsia zisiwe ni tatizo tena katika upatikanaji wa fursa za kujiletea maendeleo.

**Maendeleo duni ya wanawake nchini**

- Kuna mapungufu juu ya kubuni mbinu sahihi zitakazotuhakikishia kuwa matatizo ya ubaguzi dhidi ya wanawake katika upatikanaji wa fursa yanapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

- Kuna mapungufu juu ya kuielimisha jamii katika ngazi zote juu ya umuhimu wa kukumbatia haki sawa kwa jinsia zote na hivyo kuwa ni kikwazo katika kuwaendeleza wanawake.

- Pamoja na uwakilishi walionao hivi sasa katika bunge -ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa nafasi za viti maalumu za wanawake - ushiriki wao mdogo katika vyombo mbalimbali vya kutoa maamuzi, unaonyesha kuwa bado hakuna nia ya dhati ya kuleta usawa wa kijinsia katika jamii. Hali hii isingetarajiwa ikizingatiwa kuwa hivi sasa idadi ya wanawake wenye elimu ni kubwa inayotosheleza kuweka uwiano mzuri wa kijinsia katika vyombo mbalimbali vya maamuzi.

- Pamoja na kuwepo kwa mifuko mbalimbali kwa ajili ya mikopo ya wanawake, uendeshaji wa mifuko hiyo ni wa kisiasa zaidi na hivyo kufanya wanawake walio wengi, hasa wa vijijini wasinufaike na

mikopo hiyo. Hadi sasa Benki ya wanawake iliyozinduliwa mwaka huu 2010 na ipo Dar es Salaam pekee.

- Wanawake wanakabiliwa na tatizo kubwa mno la afya ya uzazi, huduma za uzazi kutozwa fedha, ukosefu wa lishe bora wanapokuwa wajawazito na majukumu ya malezi. Vifo vya akina mama na watoto limekuwa ni jambo lililozoeleka sana na kuonekana ni kitu cha kawaida katika jamii ya Watanzania.

- Huduma duni ya maji. Wanawake wamekuwa wakitaabika sana katika kutafuta huduma ya maji na kutembea kwa mwendo mrefu, hasa katika maeneo ya vijijini. Pamoja na kwamba Tanzania huru imezaliwa miaka 56 iliyopita, wanawake wakati mwingine hulazimika kutembea umbali wa zaidi ya kilometa 10 kila siku kutafuta maji.

- Mfumo wa elimu uliopo nchini haumuandai mtoto wa kike kuweza kukabiliana na majukumu ya kijamii.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF**

Msingi mkuu wa sera za CUF ni 'Haki sawa na furaha kwa wote'. Hii inamaanisha kwamba pamoja na CUF kutambua tofauti za makundi mbalimbali ya watu katika jamii, inayatambua makundi yote kuwa ni sawa kutokana na uwananchi wa kila kundi.

Wanawake na wanaume ni makundi yenye kutegemeana na hakuna kundi linaloweza kuwa endelevu bila ya jingine. Kwa maana hii basi mfumo Dume uliojikita katika kila nyanja ya maisha nchini ni kikwazo cha maendeleo ya taifa letu. Sera za chama chetu kuhusu elimu, afya, na kuondoa umasikini kama zilivyoainishwa katika ilani hii ni kichocheo kikubwa katika suala zima la ukombozi wa mwanamke wa Kitanzania. Lakini pamoja na sera hizi nzuri, Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya

CUF pamoja na mambo mengine itachukua hatua zifuatazo ili kuboresha mazingira ya kujenga usawa wa kijinsia katika uwiano unaofaa:

- Itatunga sheria itakayotoa adhabu kali kwa mtu yeyote atakayetumia mamlaka yake kumdhalilisha kijinsia, na kumsababishia madhara ya namna moja ama nyingine, Mtanzania mwenye jinsia tofauti na ya kwake; ili kujinufaisha binafsi kwa njia moja ama nyingine. Pamoja na manufaa ya sheria hii katika maeneo mengine, sheria hii itasaidia hasa katika suala zima la kupambana na rushwa ya ngono, hususani kwa wanafunzi na waajiriwa wa kike.

- Itauboresha utaratibu ulioko hivi sasa ambao unatoa nafasi maalum za upendeleo kwa wanawake ili kuongeza ushiriki wao katika ngazi mbalimbali za maamuzi ya kisiasa, utawala, menejimenti na uongozi.

- Ili kuwanyanyua wanawake kiuchumi Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaiimarisha mifuko mbalimbali ya mikopo na kuisimamia kusudi iwanufaishe wanawake walio wengi wa mijini na vijijini, bila kujali itikadi zao za kisiasa.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itawaunganisha wanawake wote bila kujali itikadi zao, kuunda chombo chao huru ambacho kitasimamia maslahi yao.

- Hata hivyo kwa kuwa CUF inaelewa fika kuwa suluhisho la kudumu la matatizo ya kijinsia nchini liko katika kubadilisha mitizamo ya jamii kuliko katika kuweka mashinikizo ya kisheria na kutoa upendeleo, basi hatua zifuatazo za ziada zitachukuliwa:

    - Kwa kuwa tafiti zinaonyesha kuwa wasichana wanaosoma katika shule za peke yao mara nyingi wanajenga kujiamini kuliko wale wanaosoma katika shule mchanganyiko, Serikali

itahakikisha kuwa kunakuwa na marekebisho katika mashule ili kupata manufaa ya kitaaluma yanayotokana na utafiti huo.

  - Mitaala ya somo la uraia mashuleni itafanyiwa marekebisho ili pamoja na mambo mengine somo hilo lilenge katika kufifisha mitizamo ya vijana wa kiume dhidi ya wenzao wa kike kuwa ni viumbe duni,dhalili, na wasio na mchango wowote wa maana kifikra katika jamii.

- Serikali itaanzisha na kuhimiza mjadala wa kina na wa wazi kitaifa katika ngazi mbalimbali za jamii kuhusu mgawanyo wa wajibu, majukumu, na haki katika mahusiano ya kijinsia, kwa nia ya kuboresha mahusiano hayo.

- Mkakati maalumu wa kitaifa wa kuwainua wanawake kiuchumi ili waondokane na madhara mbalimbali wayapatayo kutokana na umasikini utaasisiwa kwa kuwashirikisha wanawake wenyewe.

**Vijana**

Vijana ndiyo kundi lenye mchango mkubwa katika uzalishaji kuliko kundi jingine lolote, na kwa maana hiyo umuhimu wa kundi hili kwa jamii ni mkubwa mno.

**Hali ilivyo sasa**

- Kauli mbiu ya vijana ni taifa la kesho imepelekea kundi kubwa la vijana kuendelea kusubiri bila mafanikio. Sehemu kubwa ya vijana hawana fursa za ajira za kueleweka, kitu ambacho kinawasababisha walio wengi kujikuta wakilazimika kuingia katika vitendo viovu kupambana na umasikini unaowakabili. Vijana wengi wamekata tamaa mno kiasi kwamba wanadhani kwamba njia pekee iliyobaki ya kujiletea maendeleo ni wao kuondoka nchini au kutafuta biashara za kuzalisha faida kubwa

za haraka hata ikiwa ni haramu, kama kuuza madawa ya kulevya, kujihusisha na biashara za magendo, na kadhalika.

Kwa kweli hali hii haiashirii mazingira mazuri kwa maendeleo ya nchi na juhudi za kuondoa umasikini. Vijana wamekuwa wakitumika katika kufanikisha malengo ya wanasiasa wakati wa uchaguzi pekee na hakuna sera sahihi za kuwainua vijana kushiriki katika kustawisha maendeleo ya taifa.

Vijana wengi wapo vijiweni na wenqine wamejiingiza katika utumiaji wa dawa za kulevya na ulevi wa kupindukia, na uvutaji wa bangi. Kwa kiwango kikubwa si wenye uwezo wa kuajirika kutokana na kwamba hawajaandaliwa vya kutosha kumudu ushindani wa soko la ajira katika karne hii ya sayansi na teknolojia.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF kwa vijana nchini**

- Pamoja na azma ya CUF ya kuhakikisha kuwa kila kijana anapata elimu ya darasani (formal education) kwa upeo wa uwezo wake, Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua pia hatua zifuatazo:

    - Itaongeza kwa kiasi kikubwa idadi ya vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi katika maeneo yote ya nchi kwa lengo la kuwashawishi vijana walioshindwa kuendelea na mfumo wa masomo ya darasani kujipatia ujuzi mbalimbali wa ufundi.

    - Itaanzisha huduma ya ushauri nasaha kuhusu chaguo la ajira na matatizo ya kijamii ili kukidhi matarajio ya vijana.

    - Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha vijana wote wanaojifanyia biashara ndogondogo maarufu kama 'wamachinga' wanapewa maeneo maalum ya uhakika na

yenye mzunguko wa kibiashara kufanyia shughuli zao bila kubughudhiwa.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itazuia kabisa utaratibu wa mgambo kuwapiga na kuwanyanyasa vijana wanaofanya biashara ndogondogo.

- Pamoja na azma ya CUF kuhakikisha kuwa kunakuwa na mkakati unaoigusa jamii nzima katika kuhakikisha kuwa afya za wananchi zinaboreshwa, serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF pia itachukua hatua za kuanzisha programu zitakazohusisha makundi ya vijana katika ngazi ya mtaa na kitongoji, kwa kushirikiana na asasi mbalimbali, kuelimishana juu ya njia bora za kuepukana na maambukizo ya UKIMWI na tatizo la matumizi ya dawa za kulevya.

- Pamoja na azma ya CUF kuhakikisha kuwa kunakuwa na mkakati unaoigusa jamii nzima katika kuhakikisha kuwa viwango vya ubora wa ushiriki wa Taifa letu katika medani za michezo na burudani vinapanda, Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF pia itachukua hatua zifuatazo:

  - Itaboresha huduma za burudani na michezo vijijini na mijini kwa kushirikisha wataalamu wa fani mbalimbali katika medani hizo ili kusaidia kutambua vipaji na kuviendeleza.

  - Itashawishi ushiriki zaidi wa sekta binafsi katika kuwekeza katika huduma za burudani na michezo.

  - Itashawishi vijana kuwa mstari wa mbele kuendeleza yale yote mazuri yanayopatikana katika tamaduni zetu, na kupiga vita tamaduni mbaya za kigeni.

- Itashawishi vijana kushiriki kwa hiari yao katika harakati mbalimbali za kijamii kama vile uboreshaji wa mazingira na kuwasaidia wagonjwa, watoto, wazee, na mayatima.

- Madhumuni makubwa ya uanzishwaji wa makambi ya JKT yalikuwa ni kutoa mafunzo ya awali ya ulinzi na uchapakazi kwa vijana ili kuwatayarisha kwa maisha yao ya baadaye. Lakini ni dhahiri kuwa kiutendaji madhumuni haya yalivurugwa kwani wale ambao kweli wanahitaji mafunzo ya awali ndio ambao hawakulazimika kushiriki na wale ambao walikuwa na uhakika wa ajira ndio waliolazimika kujiunga. Waliosamehewa ni wale wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne bila kujiunga na chuo chochote, wakati waliolazimika ni wale waliomaliza kidato cha sita ama wenye elimu ya juu zaidi. Ni wazi basi kuwa mfumo uliotumika haukuwa na tija.

Pili, uendeshaji wa programu mbalimbali katika makambi hayo ulilenga zaidi katika kukomoana na kudhalilishana na hivyo matumizi ya akili yalizingatiwa kwa kiwango kidogo. Haishangazi basi kuwa makambi ambayo kimsingi yalitakiwa yawe na uwezo wa kuzalisha kwa ajili ya kujiendesha na ziada, hatimaye yalionekana kuwa ni yenye kuliingizia taifa hasara kubwa na kulazimika kusitisha sehemu kubwa ya programu zake - hususan ile ya kuwachukua vijana kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo bado umuhimu wa utumishi kwa taifa upo ila kinachohitajika ni marekebisho ya msingi. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua zifuatazo ili kuleta marekebisho yenye tija:

- Utaratibu wa uendeshaji wa programu kwenye vituo hivi utabadilika ili kuondoa dhana kwa vijana, wazazi, na watoa mafunzo kuwa hivyo ni vituo vya 'mateso' kwa vijana wanaomaliza masomo yao. Katika kutekeleza azma hiyo, kwanza kabisa muundo wa awali utabadilishwa na badala

ya kujulikana kama makambi sasa yataitwa ni 'vituo vya maandalizi kwa vijana ili kulitumikia taifa.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itatenganisha kabisa masuala ya uajiri, fursa za masomo na suala la kujiunga na vituo hivi. Serikali itavifanya vituo hivi kuwa ni huduma muhimu ya miaka miwili katika kutoa mafunzo ya awali ya kijeshi, ukakamavu, kazi za uzalishaji, lugha ya Kiingereza, huduma ya mwanzo (First Aid), sanaa mbalimbali, udereva, michezo, pamoja na stadi zinazohusiana na shughuli za uokoaji (Rescue Operations).

- Serikali itatoa ruzuku mwanzoni wakati wa maandalizi, na mikakati itawekwa kukiwezesha kila kituo kiwe kinajiendesha chenyewe.

- Serikali itaweka vituo katika kila mkoa kwa ajili ya uandikishaji wa wale wote ambao wangependa kujiunga na vituo hivi na itawashauri vijana wanaomaliza darasa la saba na kidato cha nne na kukosa nafasi ya kuendelea na masomo katika shule za kawaida na vyuo wajiunge.

- Serikali itaweka utaratibu kuhakikisha kwamba fedha zote zitakazozalishwa na vijana kutokana na miradi mbalimbali ya uzalishaji baada ya kuondoa gharama za kuendeshea kambi inayohusika zitahifadhiwa kwa ajili ya kupewa vijana wakati wa kuhitimu ili ziwasaidie kununulia zana mbali mbali zinazohusiana na stadi walizojifunza.

- Mapinduzi ya kilimo na uanzishwaji wa viwanda utaongeza ajira ya vijana katika sekta rasmi. Pia serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa vijana, hasa wahitimu wa vyuo, wanatumia kikamilifu fursa ya kuwepo kwa mifuko ya kuwezesha

kuanzisha na kukuza haraka miradi ya kibiashara (Incubator and accelerator Funds) kuanzisha na kukuza haraka miradi ya kibiashara ambayo siyo tu kwamba itawatatulia wao wenyewe tatizo la ajira, lakini pia itasaidia kuajiri vijana wengine ambao hawana vigezo vya kupokea fedha kutoka katika mifuko hiyo.

**Wazee na Wastaafu**

Wazee wa Tanzania ndio waliokuwa wazalishaji wakubwa wa jana. Hawa wamelifikisha taifa hapa lilipo kupitia uzalishaji walioufanya kama wakulima, wafugaji, wavuvi, wajenzi, waalimu, madaktari, wanajeshi, nakadhalika. Kwa bahati mbaya, pamoja na mchango mkubwa walioutoa kwa taifa, leo hii wao ndio wanaoishi maisha magumu kupita makundi mengine yote. Miaka 56 tangu Tanzania izaliwe hakujawa na juhudi za dhati za kuwaenzi wazee.

**Ajenda ya CUF kwa wazee na wastaafu**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itafanya mambo yafuatayo ili kuimarisha maisha ya wazee na wastaafu:

- Itaboresha pensheni ya wastaafu katika sekta zote ili kukidhi mahitaji yao.
- Itawalipa wastaafu wote malimbikizo ya madeni wanayodai ili kuondoa mvutano uliodumu kwa miaka mingi kutokana na dhuluma waliyofanyiwa.
- Itawapatia wazee huduma muhimu za kijamii bila malipo na urasimu wowote.
- Itaanzisha utaratibu wa kuwalipa pensheni wazee wote ambao hawakuwahi kuajiriwa katika sekta rasmi na ambao kwa sasa hawapati malipo yoyote ya uzeeni. Kwa kuanzia tutaanza na

miradi ya mifano (pilot projects) kabla ya kusambaza huduma hii kwa wazee wote.

**Ustawi wa Watoto nchini**

Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itawekeza rasilimali nyingi katika kuhakikisha watoto wanajengewa mazingira thabiti yatakayowawezesha kukua vizuri kimwili na kiakili. Itawekeza katika maeneo muhimu yanayolinda utu na heshima ya mtoto. Miongoni mwa masuala ya msingi yatakayosimamiwa

na serikali ni:

- Kuunda, kusimamia na kuwezesha kitengo maalum huru kitakachokuwa na kazi ya kuishauri serikali juu ya nini kifanywe kuboresha mazingira mazuri katika ukuaji wa watoto.

Kitengo husika kitaundwa kwa kujumuisha asasi mbalimbali za kijamii zinazojihusisha na utetezi wa haki za watoto. Serikali itaanzisha na kusimamia mambo yote muhimu yatakayoshauriwa na kitengo hiki.

- Kuokoa maisha ya watoto dhidi ya majanga mbalimbali, na kuhamasisha upatikanaji wa lishe bora kwa watoto.

- Kutengeneza mifumo mizuri ya kuhakikisha kuwa siha na afya vinalindwa kikamilifu katika mazingira ya shule. Mifumo hii ni pamoja na upatikanaji wa maji safi na salama, uwepo wa vyoo bora vyenye kutosheleza mahitaji, pamoja na kuwepo kwa maafisa wa ushauri nasaha (counselors) waliofunzwa kushughulikia masuala ya watoto na vijana.

- Kuhakikisha kuwa watoto wadogo na watoto wa kike wanalindwa dhidi ya maambukizi ya VVU na kudhibiti upatikanaji wa mimba za utotoni.

- Kuwasaidia watoto wenye mahitaji maalum (wenye ulemavu).

**Wataalamu**

Tanzania haitaweza kupiga hatua za maendeleo iwapo wataalam katika nyanja mbalimbali hawatapewa kipaumbele. Japo nchi yetu bado haijawa na wataalamu wengi sana katika nyanja mbalimba, lakini hao waliopo bado hatujaweza kuwatumia ipasavyo katika kuwakomboa watanzania kutoka katika dimbwi la umasikini, ujinga, maradhi na matatizo mengine. Kwa mfano, tafiti zinaonyesha kuwa asilimia sitini (60%) ya wahitimu wa kozi za udaktari hawana ajira. Hii ni aibu kubwa ukizingatia kwamba uwiano wa daktari kwa wagonjwa hapa Tanzania ni mbaya sana. Hapa Tanzania uwiano wa daktari kwa wagonjwa ni 1: 25,000. Yaani kila daktari mmoja anahudumia wagonjwa 25,000.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF kwa Wataalamu wa fani mbalimbali**

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaanzisha tuzo maalum kwa ajili ya wataalam wote waliofanya kazi muhimu ya kitaalam na ikaleta tija kwa nchi.

- Serikali itatoa uhuru wa kujianzishia vyama vya kitaaluma na klabu mbalimbali za kitaaluma, ili wataalamu wa fani mbalimbali wakutane mara nyingi kadri wawezavyo, na kujadiliana mambo na mbinu mbalimbali ili kuinua taaluma zao na kulisaidia taifa kuharakisha maendeleo yake.

- Serikali itawapeleka wataalam wengi kadri inavyowezekana nje ya nchi ili wakaongeze taaluma na ujuzi wao kwa maslahi ya nchi. Hivi sasa wataalam wanaopelekwa nje ya nchi kuongeza mafunzo ya kitaalam ni wachache na hakuna uzingatiaji wa vigezo sahihi katika kuwateua.

- Serikali itawaongezea wataalamu vivutio zaidi na kuboresha maslahi yao ili wapende zaidi majukumu yao na kujitoa zaidi kulipambania taifa.

### 3.1.25. MICHEZO NA BURUDANI

Hali ya michezo na burudani nchini imekuwa siyo nzuri kwa muda mrefu sasa. Viwanja vya michezo vilivyoko katika mikoa yote vina hali mbaya sana; ahueni iko katika viwanja viwili tu vya Dar es salaam, yaani uwanja mpya wa Taifa na ule wa uhuru. Kutokana na sababu mbalimbali wawakilishi wetu mbalimbali kwenye michezo ya kimataifa wanaendelea kufanya vibaya kila mara. Pamoja na juhudi kubwa za makampuni ya biashara kama NMB na mengine kufadhili kwa kiasi kikubwa gharama za timu zetu za taifa na vilabu, bado kuna tatizo kubwa la serikali kutokuwa na usimamizi mzuri katika michezo. Aidha kumekuwa na udhaifu mkubwa katika kulinda haki na maslahi ya wasanii mbalimbali, pamoja na kuwasaidia ili waweze kunufaika ipasavyo na kazi zao. Kutokana na kukosekana kwa mazingira rafiki, kazi za wasanii zimekuwa zikinakiliwa hovyo mitaani na kuwasababishia hasara kubwa. Bl aserikali kuingilia kati na kusimamia upatikanaji wa haki za wasanii, wasanii wengi wataendelea kuwa maskini huku wajanja wachache wakiendelea kunufaika na kazi zao.

**Hali ilivyo sasa katika sekta ya Michezo nchini**

- Serikali ya CCM imekuwa na mtizamo wa kizamani kuhusu michezo, yaani kuichukulia kama suala la watu binafsi, badala ya kuwa ni suala la jamii nzima. Kutokana na mtizamo huu, serikali imeshindwa kabisa kuona jinsi ambavyo michezo imekuwa ikibadilika taratibu kutoka kuwa ni burudani tu na kuwa ni ajira na biashara kubwa inayohusisha mamilioni ya dola.

- Kumekuwa na matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kisingizio cha kuhudumia masuala ya michezo, burudani na dini wakati

katika hali halisi hakuna huduma za namna hiyo zinazotolewa, na kama zinatolewa ni kidogo sana.

- Juhudi za kuendeleza vipaji vya vijana hazijawekewa mikakati inayopimika na yenye kuzaa matunda.

- Viwanja karibuni vyote vilivyojengwa kwa nguvu ya wananchi baada ya uhuru vimechukuliwa na kumilikishwa Chama cha mapinduzi. Hivi sasa viwanja hivi vipo katika hali mbaya, vikiwa vimekosa ukarabati na uboreshaji wa kuviendeleza viwanja hivyo.

- Vifaa vya mazoezi na michezo vinauzwa kwa gharama ya juu sana kiasi kwamba wananchiwalio wengi wanashindwa kuvinunua na kuvitumia. Hali hii haiko sawa ukizingatia kwamba wananchi wanahitaji wahamasishwe kufanya mazoezi na kushiriki michezo kama njenzo ya kulinda siha na kuboresha afya zao ili kuliondolea taifa mzigo mzito wa kutibu magonjwa ya kimfumo.

- Serikali ya CCM imeshindwa kutimiza wajibu wake ipasavyo katika kulinda na kuendeleza haki za wasanii.

**Dira ya Mabadiliko ya CUF katika sekta ya michezo**

Ili kuboresha mazingira ya michezo nchini na kuhakikisha kuwa viwango vya uchezaji vya wanamichezo wetu vinakua na kufikia ngazi ya usnindani wa kimataifa, Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itachukua hatua zifuatazo:

- Serikali itahimiza ujenzi wa viwanja vipya vya michezo na uboreshaji wa vile ambavyo tayari vipo. Jukumu la kukamilisha azma hii litakabidhiwa kwa mabaraza ya manispaa, miji na halmashauri za wilaya ambapo kila mkoa utapaswa kujenga uwanja mkubwa wa michezo yote, kila manispaa itapaswa kujenga kiwanja kimoja kikubwa kitakachotumika kwa michezo yote, huku

Serikali kuu ikiwa na jukumu la kujenga viwanja vya kimataifa na kisasa vinne vyenye uwezo wa kutumika kwa michezo yote mikuu. Viwanja hivyo vitajengwa katika kanda ya kusini, kanda ya ziwa, kanda ya kaskazini na kanda ya kati. Pamoja na vyanzo vingine vya fedha, mamlaka hizi zitatafuta wabia wa kushirikiana nao kukamilisha jukumu hilo.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa maeneo yote ya wazi yanatunzwa ipasavyo, huku yale mengi yaliyouzwa katika mazingira tata yanashughulikiwa.

- Ili kuongeza ushindani zaidi katika michezo, Serikali kwa kushirikiana na vyama vya michezo mbalimbali itabuni mashindano ya ziada nje ya ligi za kawaida, ikiwa ni pamoja na kutafuta wadhamini wa uhakika wa kudhamini mashindano hayo katika ngazi za wilaya, mkoa na Taifa.

- Ili wanamichezo waweze kushindana kikamilifu taifa halina budi kukubali kuwa mabadiliko ya msingi ni lazima yafanyike katika sekta ya michezo ili wanamichezo wetu waweze kuitegemea michezo wanayocheza kama ajira. Serikali itawatumia wataalamu mbalimbali wa masuala ya michezo ili kupata mkakati bora wa kuasisi mabadiliko hayo.

- Hivi sasa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam kinatoa mafunzo ya elimu ya michezo katika kitivo chake cha elimu. Wahitimu wa mafunzo haya wanatarajiwa kuwa waalimu wa michezo shuleni. Hata hivyo wahitimu hawa ni wachache sana ikilinganishwa na mahitaji. Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itapanua zaidi idara inayohusika na mafunzo haya na kuongeza idadi ya wanafunzi wa fani ya michezo. Aidha itayaimarisha mafunzo yanayotolewa ili yalenge katika kutoa wahitimu bora zaidi. Katika kuendeleza vipaji vya wachezaji wadogo wa michezo mbalimbali,

Serikali itajenga shule za sekondari kadhaa za mchepuo wa michezo. Shule hizi zitakuwa vituo muhimu vya kuwaandaa wawakilishi wetu mbalimbali katika michezo ya kimataifa.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itahakikisha kuwa timu za taifa zinazojiandaa kwa mashindano mbalimbali ya kimataifa zinakuwa chini ya udhamini wa Serikali. Aidha Serikali itachukua hatua za makusudi na kuweka mkakati mahsusi kwa kushirikiana na TFF kuhakikisha kuwa timu ya Taifa ya mpira wa miguu inashiriki mashindano ya kombe la Afrika na kombe la dunia mwaka 2022.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itawapeleka nchi za nje vijana wengi wenye vipaji vya michezo mbalimbali ili wakajifunze michezo katika vituo vya michezo (Sports Academy), huku wakiendelea na masomo. Vijana hao watakaporejea nchini watatumika kama waalimu wa michezo katika vyuo mbalimbali vya ualimu.

- Serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itaziunga mkono kikamilifu juhudi za wadhamini mbalimbali ambao wanajitokeza kukuza vipaji vya wasanii na kuwaendeleza. Aidha Serikali itafanya marekebisho mbalimbali ya kisheria ili kulinda kikamilifu haki za wasanii wetu. Kabla ya kufanya marekebisho ya sheria husika serikali itakutana na wasanii na kupokea mapendekezo yao juu ya njia sahihi za kudhibiti uharamia wa kazi zao.

Imetolewa na Baraza kuu la Uongozi La Taija,

**THE CIVIC UNITED FRONT**

**(CUF-Chama Cha Wananchi)**